

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 27 Mei, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### *D U A*

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:**

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Taarifa za Mwaka za Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na 2017/2018 (*The Annual Reports and Audited Accounts of the Roads Fund Board for the Financial Year 2016/2017 and 2017/2018*).

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA – MAKAMU MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BUNGE YA HESABU ZA  
SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu

zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtando)*

Na. 346

**Barabara za Kuelekea Mlimani - Jimbo la Arumeru Mashariki**

**MHE. DKT. JOHN D. PALANGYO** aliuliza:-

Barabara zote zinazoelekeea Mlimani katika Jimbo la Arumeru Mashariki kutoka barabara kuu ya Moshi - Arusha hazipitiki kwa muda mrefu na sasa hali imekuwa mbaya zaidi baada ya mvua nydingi zilizonyesha tangu Oktoba, 2019:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzifanya matengenezo barabara hizo ili ziweze kuitika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi, kujenga kwa kiwango cha lami na kufanya *by pass* barabara ya Malula Kibaoni – Kingori – Maruvango – Leguruki – Ngarenanyuki – Ngabobo - Uwiro hadi Oldonyosambu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Palangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*)imeidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 200 ili kulfanya matengenezo barabara ya Ambureni - Nkoanrua - Kimundo - Seela yenye urefu wa kilomita sita ambayo pia ni sehemu ya barabara za milimani, hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, barabara ya Leganga – Mulala yenye urefu wa kilomita tatu imefanyiwa matengenezo kwa gharama ya Shilingi milioni 15.0 ili kuhakikisha inapitika wakati wote. Vilevile, kiasi cha shilingi milioni 50 za dharura zimetengwa ili kuboresha barabara ya Sangisi-Ndoombo yenye urefu wa kilomita 5.2 iliyoharibiwa na mvua.

(b) Mheshimiwa Nailbu Spika, kuhusu barabara ya *by pass* ya Malula Kibaoni – Kingori – Maruvango – Leguruki – Ngarenanyuki – Ngabobo - Uwiro hadi Oldonyosambu yenye urefu wa kilomita 12 kupandishwa hadhi, napenda kutoa maelezo kuwa baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*), Serikali imesitisha upandishaji hadhi barabara za Wilaya kuwa barabara za Mikoa. Serikali itaendelea kuboresha barabara hiyo ili iendelee kupidika muda wote.

Na. 347

**Barabara Inayounganisha Mkoa wa Geita, Shinyanga,  
Tabora na Katavi**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Masumbwe, Mwabomba, Nyankende, Bugomba, Ulowa hadi Kaliua inayounganisha Mikoa wa Geita, Shinyanga, Tabora na Katavi itapandishwa hadhi kuwa ya Mkoa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*), Serikali imesitisha upandishaji hadhi barabara za wilaya kuwa barabara za mikoa. Serikali itaendelea kuboresha barabara ya Masumbwe - Mwabomba – Nyankende – Bugomba - Ulowa ili iendelee kuitika muda wote.

Na. 348

**Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma  
Wenye Ulemavu**

**MHE. AMINA S. MOLLEL aliuliza:-**

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma wenye Ulemavu imeelezwa bayana umuhimu wa kukusanya na kutunza takwimu za watu wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma:-

(a) Je, mpaka kufikia sasa kuna watu wenye ulemavu wangapi kwa kuzingatia aina zao za ulemavu ambao wana ajira katika Utumishi wa Umma?

(b) Je, kati ya Watumishi hao ni Watumishi wangapi ambao wamepata fursa ya kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za kiuteuzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Serikali mwaka 2005 ilibainika kuwa pamoja na mambo mengine haukuwepo utaratibu wa kukusanya na kutunza takwimu za watu wenyewe ulemavu katika Utumishi wa Umma. Kufuatia changamoto hiyo, mwaka 2012 Serikali iliamua kuingiza kipengele cha kuwatambua watumishi wake wenyewe ulemavu kwenye mfumo wake wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara na hivyo kuiwezesha kuwa na takwimu sahihi za watumishi wenyewe ulemavu.
- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2007, watu wenyewe ulemavu waliokuwa wameajiriwa katika utumishi wa umma walikuwa 689. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Agosti, 2019 kulikuwa na watumishi 2,900 wenyewe ulemavu wa aina mbalimbali. Kati ya watumishi hao, watumishi 2,859 wamo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara na watumishi 41 wako nje ya Mfumo. Takwimu hizi zinaonesha kuwa Serikali imekuwa ikifanya juhudhi kubwa katika kuongeza idadi ya watumishi wenyewe ulemavu katika Utumishi wa Umma ili kuwapa nafasi katika ujenzi wa Taifa kupitia ajira zao.
- (c) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya watumishi 2,859 wenyewe ulemavu waliopo katika Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara, watumishi 46 wenyewe ulemavu waliokidhi sifa za msingi wameteuliwa kushika nafasi mbalimbali za kiuteuzi.

Na. 349

**Vivutio vya Kihistoria, Mikindani-Mtwara**

**MHE. MAFTAH A. MACHUMA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikiingiza fedha nydingi za kigeni kupitia Sekta ya Utalii nchini na kwamba imekuwa ikiboresha na kutangaza maeneo na vivutio mbalimbali nchini:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwalishwa Watanzania na dunia kwa ujumla kuwa Mtwara Mjini, Tarafa ya Mikindani kuna vivutio vya kihistoria ambavyo havipatikani popote nchini kama vile soko la kwanza la watumwa?

(b) Je, Serikali iko tayari kukarabati vivutio hivyo na kuvitangaza ili wana Mtwara wapate ajira kupitia vivutio hivyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika manipaa ya Mtwara Mikindani kuna mji maarufu wa kihistoria wa karne 18 ambao kwa kutambua umuhimu wake, Serikali imeuhifadhi kama Kumbukumbu ya kihistoria na urithi wa utamaduni wa Taifa kwa Tangazo la Serikali Na.308 la mwaka 2017 kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale. Mji huu una vivutio vingi vya urithi wa utamaduni ambavyo ni: Majengo ya kihistoria 79, maeneo matatu ya wazi (bustani), ufukwe wa bahari, soko la kihistoria la kumbukumbu ya biashara ya utumwa na visima vitatu vya kihistoria. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua uwepo wa vivutio mbalimbali vya urithi wa utamaduni vyenye sifa za kipekee katika mji wa kihistoria wa Mikindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Trade Aid*, imekuwa ikifanya ukarabati wa baadhi ya majengo ya kihistoria mfano; *Old Boma*, *Livingstone* na nyumba ya Gavana. Naomba nitoe rai kwa wamiliki wa majengo ya kihistoria Mikindani kuchukua jukumu la kufanya ukarabati wa majengo yao ya kihistoria mara kwa mara ili kulinda yasibomoke na kuhifadhi mandhari asili ya Mji wa Mikindani. Wizara itashirikiana na wananchi katika kutoa elimu ya uhifadhi kwa vitendo kwa mafundi wa ukarabati wa majengo ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara kuptitia Bodi ya Utalii Tanzania imekuwa inatangaza Mji wa kihistoria wa Mikindani kama kivutio cha utalii. Aidha, Wizara imeanzisha Tamasha la Urithi *Festival* ambalo husherehekewa pamoja na Siku ya Mikindani kila mwaka mwezi Septemba. Matamasha haya yamesaidia sana kutangaza na kutoa elimu ya uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Mikindani ili kulinda historia ya Taifa na kama kivutio cha utalii Kanda ya Kusini.

Na. 350

**TFS Kuzuia Usafirishaji Mazao ya Misitu Baada ya  
Saa 12 Jioni**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

- (a) Je, kwa nini *TFS* inazuia mazao ya misitu kama mbao, fito, mijengo, mabanzi na nguzo kusafirishwa baada ya saa 12 jioni?
- (b) Ili kusafirisha mazao ya misitu kihalali; je, mwananchi anatakiwa kuwa na vibali gani?
- (c) Kwa utaratibu huo; je, kwa gari la zaidi ya tani 15 itamgharimu mwananchi kiasi gani cha fedha?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, usafirishaji wa mazao ya misitu kama mbao, fito, mijengo, mabanzi na nguzo hauruhusiwi kati ya saa 12 jioni na saa 12 asubuhi. Hii ni kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 68 la tarehe 17 Machi, 2000. Usafirishaji huo umepigwa marufuku ili kuongeza udhibiti wa uvunaji na usafirishaji holela wa mazao ya misitu unaosababisha uharibifu wa maliasili na mazingira na kuikosesha Serikali mapato.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili mwananchi asafirisha kihalali mazao ya misitu anatakiwa kuwa na vibali vifuatavyo: (i) Hati ya kusafirishia mazao (*Transit Pass*). Kwa mujibu wa Kanuni za Misitu za mwaka 2004, kifungu Na.13 hati hiyo itakuwa imetaja kampuni, mfanyabiashara au mmiliki binafsi wa mazao yanayosafirishwa na vielelezo vyote vya umiliki wa mazao hayo; na (ii) Stakabadhi ya manunuzi au malipo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 255 la tarehe 28 Julai, 2017 katika jedwali la 14 sehemu ya tatu ya Tangazo hilo, itamgharimu mwananchi kiasi cha Sh.15,400 kusafirisha mazao ya misitu kwa chombo cha usafiri cha tani 15 au zaidi na Sh.7,700 kwa gari lenye uzito wa tani saba au chini ya hapo.

Na. 351

### **Kuvuna Mamba Ziwa Ilamba – Busokelo**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Ziwa Ilamba katika Jimbo la Busokelo limekuwa na mamba wengi na wananchi wengi wamepoteza maisha na wengine kujeruhiwa na mamba hao:-

Je, ni lini Serikali itawavuna mamba hao ili wananchi wa maeneo yanayozunguka ziwa hilo waishi kwa amani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini hususani mamba. Kutokana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kunusuru maisha ya wananchi ikiwa ni pamoja

na kushughulikia matukio yanayohusu mamba kwa haraka iwezekanavyo pindi yanapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo, Wizara imeunda kikosi kazi cha kufanya tathmini ya kina ili kuainisha idadi ya mamba watakaojunwa nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na Ziwa Ilamba katika Wilaya ya Busokelo. Aidha, Serikali za Vijiji na Wilaya zinashauriwa kujenga uzio maeneo ambayo shughuli za kibinadamu kama kuoga, kuchota maji na kufua zinafanyika ili kupusha wananchi kupata madhara yanayosababishwa na mamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Wizara kuwa tathmini itakapokamilika, uvunaji kwa njia ya minada utafanyika ili kupunguza adha kwa wananchi.

Na. 352

**Ujenzi wa Barabara Zinazounganisha Kyerwa na Nchi za Uganda na Rwanda**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliliza:-

Kyerwa ina barabara mbili, barabara ya Omugakorongo – Murongo na barabara ya Omurushaka – Murongo. Aidha, barabara hizo zinaungana na Nchi za Rwanda na Uganda na vilevile Rais wa Awamu ya Tano aliahidi ujenzi wa barabara hizo:-

Je, ni lini barabara hizo muhimu zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Innocent Sebha Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Omugakorongo-Kigarama- Murongo (kilomita 110.1) pamoja na barabara ya Omurushaka-Murongo (kilomita 112.26) ni barabara ambazo zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Kagera. Barabara hizi ni za changarawe lakini zinapitika vizuri wakati wote kutokana na kufanyiwa matengenezo mbalimbali kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi milioni 993.072 zimetengwa na katika mwaka wa fedha 2020/2021, shilingi milioni 747.059 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili barabara hii iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, tathmini ya athari ya mazingira na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (kilomita 110.1) imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga shilingi milioni 8,000 kwa ajili ya kulipa fidia na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara ya Omurushaka – Murongo (kilomita 125), taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, shilingi milioni 180.0 zimetengwa kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Shilingi milioni 350 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 891.445 na katika mwaka wa fedha 2020/2021, shilingi milioni 763.707 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili barabara hii iendelee kupitika majira yote.

Na. 353

## **Kujenga Uwanja wa Ndege wa Tunduru**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mpango wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Tunduru?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Injinia Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili, 2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini – *TAA*) ilitembelea na kufanya tathmini ya Viwanja vya Ndege vya Mikoa ya Kusini ambavyo ni Tunduru, Nachingwea, Newala, Masasi, Songea, Njombe na Iringa ili kubaini mahitaji halisi kwa lengo la kuviboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia zoezi hilo, ilibainika kuwa kiwanja cha ndege cha Tunduru kimezungukwa na makazi ya watu ikiwemo Hospitali ya Wilaya na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya. Pamoja na changamoto hiyo, Kiwanja hiki bado kinafaa kwa matumizi ya ndege za abiria isipokuwa kinahitaji kujengewa uzio ili kuimarisha usalama wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege Mikoa ya Kusini kwa kuanza na mikoa ya Mtwara na Songea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wake uitwao *DCTP (Development Corridor Transport Programme)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ili iweze kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tunduru.

Na. 354

**Hitaji la Hospitali ya Kanda ya Magharibi**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA** aliuliza:-

Licha ya juhudni za Serikali kuendelea kuboresha Hospitali za Mikoa, bado Hospitali za Mikoa zina mzigo mkubwa wa wagonjwa na kushindwa kumudu mzigo huo:-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Kanda ya Magharibi ili kupunguza mzigo katika Hospitali za Mikoa ya Katavi, Tabora na Kigoma?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kujenga Vituo vya Afya vipatavyo 352 nchi nzima, Hospitali za Rufaa za Mikoa tano kwenye Mikoa Mipya na Hospitali za Wilaya 70 nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Katavi, Serikali imeanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa ambapo ikikamilika majengo ya sasa ya hospitali ya Mkoa yatakabidhiwa kwa Halmashauri ya Mpanda. Aidha, Serikali ina kusudio la kujenga Hospitali ya kanda ya Magharibi Mkoani Tabora ambayo inategemewa kuhudumia wakazi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Tabora na Kigoma.

Na. 355

**Mradi wa Viwanja 20,000 Jiji la Dar es Salaam**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Wizara ya Ardhi kupitia mradi wa viwanja 20,000 iliuza viwanja kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Katika Jimbo la Kawe Mradi huo ulitekelezwa katika kata za Mbweni na Bunju; wananchi walilipia viwanja kwa maelekezo kwamba gharama za viwanja zingetumika kuboresha miundombinu mbalimbali katika eneo husika, lakini ahadi hiyo haikutekelezwa kwa ufasaha hali inayopelekea kero kubwa ya mafuriko na kutuama kwa maji hususan kipindi cha mvua, kero kubwa ikiwa ni Mtaa wa Mbweni Feta na Mbweni Malindi:-

Je, ni lini Serikali itatatua kero hii?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika mwaka 2003 na 2008 Serikali ilitekeleza mradi wa upimaji viwanja 20,000 katika maeneo mbalimbali katika Wilaya za Jiji la Dar es Salaam. Maeneo hayo ni pamoja na Bunju, Mivumoni, Mbweni JKT na Mbweni Malindi katika Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Wizara lilikuwa ni kufungua barabara kwa mujibu wa michoro ya mipango miji na upimaji. Baada ya barabara hizo kufunguliwa zilikabidhiwa katika Halmashauri husika ambako viwanja hivyo viro ili waziendeleze zaidi na kuzihudumia. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa mitaa ambayo viwanja hivyo vimepimwa inapitika wakati wote ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imanzishwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini ambapo mamlaka hiyo imeendelea kutekelezwa zoezi la urekebishaji wa miundombinu kwa maeneo yanayohitajika mfano zoezi linaloendelea katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni

katika viwanja vya mradi katika eneo la Mwongozo. Wajibu wa Serikali ni kuwaonesha watekelezaji ramani za viwanja ili kuweka miundombinu kuendana na mpango.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019**

**NAIBU SPIKA:** Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, taarifa ya Kamati kuhusu taarifa ya Mdhibiti Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019. Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 Ibara ya 17 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza, maelezo ya jumla kuhusu shughuli za Kamati, ninakushukuru kwa ridhaa ya kuwsilisha Bungeni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *CAG* kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya serikali za Mitaa nchini kwa mwaka wa fedha ilioishia tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kukushukuru tena kwa kuiwezesha *LAAC* na Bunge kwa

ujumla kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, naomba kukupa pole kufuatia vifo vya Wabunge wenzetu Mheshimiwa Dkt. Augustine P. Mahiga Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare Mbunge na Mheshimiwa Richard M. Ndassa Mbunge, Mwenyezi Mungu azijaalie roho zao marehemu pumziko jema peponi amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhu kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kumteua Mjumbe wa *LAAC* Mheshimiwa Godwin A. Mollel kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tangu tarehe 16 Mei, 2020. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mollel Mbunge kwa uteuzi huo na kumtakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo naomba sasa uridhle taarifa ya Kamati inukuliwe katika Taarifa Rasmi za Bunge Hansard kama yalivyo katika taarifa kuu ambayo nakala yake ipo katika vishikwambi yaani (*tables*).

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yalitokelezwa na Kamati, msingi wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge umebainishwa katika Ibara ya 96(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, majukumu ya kila Kamati ikiwemo *LAAC* yamefafanuliwa zaidi katika Kanuni za Kudumu za Bunge za matoleo mbalimbali, jukumu mahususi la *LAAC* ni kufuatiliana kushauri kuhusiana na matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia hoja za ukaguzi wa *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio katika utekelezaji wa shughuli za *LAAC*, katika kipindi cha miaka mitano ya maisha ya Bunge la Kumi na Moja tangu Novemba 2015 hadi Mei 2020 *LAAC* imetekeliza wajibu wake kikamilifu na kupata mafanikio yafuatayo:-

(i) Iliweza kuwasilisha Bungeni kwa wakati taarifa za maoni na mapendekezo kuhusu taarifa zote za *CAG* zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi chote cha maisha ya Bunge la 11;

- (ii) Iliweza kufuatilia kikamilifu utekelezaji wa mapendekezo yake katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusiana na ukusanyaji wa mapato ya ndani, udhibiti wa matumizi yasiyokuwa na tija na uboreshaji wa mifumo mbalimbali ya katika mamlaka hizo;
- (iii) Iliweza kuishawishi Serikali kufuta madeni yaliyokuwa yakizikabili halmashauri kutoka na malimbiliko ya michango katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;
- (iv) Iliweza kuishauri Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982 ili halmashauri ziweze kuchangia asilimia kumi ya mapato yao ya ndani kwa vikundi vya maendeleo ya wanawake, vijana, watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria;
- (v) Iliweza kuishawishi Serikali kuharakisha uteuzi na usibitisho wa Wakuu wa Idara mbalimbali katika halmashauri. Hivyo kuchochaea uwajibikaji mionganini wa watumishi hao;
- (vi) Iliweza kushirikiana vyema na vyombo vya habari na Asasi mbalimbali za kirai kwa njia ya semina warsha;
- (vii) Iliweza kutumia ipasavyo teknolojia ya Bunge Mtandao yaani (*e-parliament*) katika kutuma na kupokea taarifa hivyo kuwa na kichocheo kwa Taasisi zingine za Umma nchini kuendesha shughuli zao kidigitali;
- (viii) Kupitia ushirika wa viongozi wake *LAAC* ilishiriki kikamilifu vikao vyote vya Kamati ya uongozi hivyo kuwa sehemu ya maamuzi na mafanikio yaliyopatikana katika uendeshaji wa shughuli za Bunge la 11;
- (ix) Illichangia kudumisha mahusiano mema ya kazi kati ya mihimili ya Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo

kuchangia pia katika kuboresha nidhani ya matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa na;

(x) Iliweza kutekeleza majukumu yake kwa umoja na mshikamano mionganoni mwa Wajumbe wake bila kujali tofauti za kiumri, makabila, jinsia, itikadi za kisiasa na elimu, hivyo kufanikiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge imetupasa kuyaeleza mafanikio haya ili Bunge lako na Umma kwa ujumla wafahamu tulichofanikiwa kukipata katika muda wote ambao tulitumwa kazini. Kwa msingi huo haya ni mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja kwa ujumla wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili uchambuzi wa taarifa za CAG na matokeo ya majadiliano. Katika mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya halmashauri 185 zilikaguliwa na CAG, kati ya halmashauri hizo 176 sawa na asilimia 95 zilipata hati safi za ukaguzi, halmashauri tisa sawa na asilimia tano zilipata hati zenyenye mashaka. Baada ya mahojiano na LAAC imejiridhisha kuwa kwa matokeo ya ukaguzi wa CAG yalizingatia miongozo stahiki ya ukaguzi wa fedha za Umma kama vile masharti ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Sheria za Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008 na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, Sheria za Fedha za Umma za mwaka 2001, Sheria zingine na za nchi na viwango zilivyowekwa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifungu cha 10 cha Sheria ya ukaguzi ya Umma ya mwaka 2008 kimeweka sharti kuwa ukaguzi wa CAG katika Taasisi za Umma nchini ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwa niaba ya Bunge. Hivyo basi ninayoheshima kukuarifu kuwa hoja zilizoibuliwa na CAG katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 zinaakisi uwalisia ulipo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na zilijengwa katika misingi ya Kikatiba, Sheria, Kanuni na Taratibu za ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa sasa. Nidhamu ya matumizi ya fedha Umma katika halmashauri nchini inazidi kuimarika ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita. Mahitaji ya huduma za jamii kama vile, elimu, afya, ulinzi, usalama, usafirishaji na uchukuzi vimezidi kuboreka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya rushwa mionganoni mwa watumishi wa halmashauri vimezidi kupungua, kutokana na hali hii shirika la *Transparent International, (The Global Coalition Against Corruption)*katika taarifa yake ya mwaka 2019 iliyojulikana kama kwa jina la *Overviews of Corruption and Anti-corruption Tanzania* iliripoti kuwa kiasi cha rushwa mionganoni mwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini Tanzania kimepungua kutoka asilimia 25 ya mwaka 2015 mpaka kufikia asilimia 10 mwaka 2019, huku asilimia ya wananchi waliotoa rushwa ili kupata huduma katika mamlaka hizo ikipungua kutoka asilimia 25 mwaka 2015 hadi asilimia 18 mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya changamoto katika matumizi ya fedha. Pamoja na maelezo yaliyotolewa hapo juu bado kuna baadhi ya halmashauri zenyet matatizo katika matumizi ya fedha za Umma, sababu za matatizo hayo zimeweza kugawanywa katika makundi makuu mawili kama inavyoonekana katika sehemu hii ya pili ya taarifa hii. Kuna matatizo ambayo chimbuko lake ni kutokana na taratibu za Serikali Kuu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na matatizo ambayo chimbuko lake ni kutokana na mwenendo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe, faraja iliyopo ni kwamba endapo Serikali itakubali kuzingatia ushauri utakaotolewa na Kamati matatizo haya yatarekebishika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, maoni na mapendekezo uchambuzi uliofanyika katika sehemu ya pili ya taarifa hii umebainisha maeneo manane yenye changamoto katika mapato na matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kimsingi maeneo hayo

ndiyo yenye hoja za ukaguzi katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, maeneo hayo yanahusu:-

(i) Fedha za ruzuku ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutopelekwa ipasavyo katika halmashauri;

(ii) Kutofungamanishwa kikamilifu kwa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato, ufungaji wa hesabu za Serikali;

(iii) Urasimu katika kupitisha hati za malipo kwa wakandarasi;

(iv) Upotevu wa mapato ya halmashauri kutokana na kutorejeshwa ipasavyo gharama za matibabu kwa njia ya bima ya afya kutoka *NHIF*;

(v) Baadhi ya halmashauri kutowasilisha ipasavyo michango yao kutokana na makato ya kila mwezi ya mishahara ya watumishi katika mifuko ya hifadhi ya jamii;

(vi) Baadhi ya halmashauri kutozitumia ipasavyo mashine za kukusanya mapato vituoni yaani (*POS*);

(vii) Baadhi ya halmashauri kutozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za fedha na manunuzi ya Umma katika kutekeleza miradi ya maendeleo; na

(viii) Baadhi ya halmashauri kushindwa kudai vati katika miradi ya maendeleo inayotekelawa kwa kutumia fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto nilizoorodheshwa hapo juu Kamati inaliomba Bunge liafiki maoni na mapendekezo yafuatayo ili yaweze kutekeleza na Serikali:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Serikali Kuu kutowasilisha ipasavyo ruzuku ya fedha za maendeleo katika halmashauri:-

KWA KUWA LAAC imetoa ushahidi usiyo na shaka kwamba ruzuku ya fedha za maendeleo haipokelewi ipasavyo katika halmashauri, zipo halmashauri zinapelekewa fedha nyingi kuliko kiasi kilichoombwa wakati zingine zinapelekewa fedha pungufu kwa kuchelewa;

NA KWA KUWA kitendo hicho kinaathiri utekelezaji wa mipango ya mamlaka husika katika kuboresha huduma za jamii;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali idumishe utaratibu wa kupeleka fedha za maendeleo katika halmashauri kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria ya matumizi inayotungwa na Bunge katika mwaka husika wa bajeti ili mamlaka hizo ziweze kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso hili linakusudia kuhimiza Serikali kuongeza juhudhi katika ukusanyaji wa mapato na kupeleka ipasavyo fedha zinazokusanywa ili zikaboreshe maisha ya wananchi kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu urasimu katika kupitisha hati za malipo ya wakandarasi:-

KWA KUWA ni dhahiri kuwa Serikali imekuwa imeweka urasimu mkubwa katika kuhakiki hati za malipo ya wakandarasi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hati zikishawasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji zinapelekwa Mkoani kwa (*RAS*), kutoka Mkoani zinapelekwa kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kisha Wizara ya Fedha na Mipango Hazina;

NA KWA KUWA, urasimu huu ni mionganini mwa sababu kubwa za kuchelewesha ukamilishaji wamiradi ya maendeleo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali ione uwezekano wa kupunguza urasimu huu kwa kupunguza mamlaka za uchambuzi wa tathimini za hati hizo, kwa mfano hati hizo zingeweza kupelekwa moja kwa moja Ofisi ya Rais,

TAMISEMI kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI izipeleke katika Wizara ya Fedha na Mipango Hazina huku (*RAS*) akipata nakala ya ushahidi wa mchakato ulivyoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linakusudia kuweka mazingira yatakayochangia kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri kwa wakati. Kuhusu hoja ya mifumo wa *EPICOR* kutofungamanishwa kikalifu na mifumo mingine ya udhibiti wa mapato na uandaaji wa taarifa za fedha:-

KWA KUWA *LAAC* imetoa ushahidi usio na shaka kwamba katika baadhi ya halmashauri mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliji, udhibiti wa mapato na ufungaji wa hesabu za mwisho za Serikali yaani (*Government Final Account*) haijafungamanishwa kikamilifu;

NA KWA KUWA, kitendo hicho kinachochaea upungufu wa mapato na udhaifu katika ufungaji wa hesabu za Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaitaka Serikali kufungamanisha kikalifu mifumo ya *EPICOR*, *PRANREP*, *LAWSON*, *FFARS* na *Got-HoMIS* ili iweze kupashana habari za kifedha kwa uwazi na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linakusudia kusaidia Serikali kupata manufaa mapana zaidi kutohana na matumizi ya mifumo hiyo ambayo kutofungamanishwa kwake kunapunguza kiasi cha manufaa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kukiukwa kwa Sheria za Fedha za Manunuzi:-

KWA KUWA *LAAC* imetoa ushahidi usio na shaka, kuhusu baadhi ya Halmashauri zilizohusika na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi ya huduma na bidhaa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

NA KWA KUWA ukiukwaji huo ni uvunjifu wa sheria za nchi na ni miongoni mwa mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Umma nchini;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuzingatia sheria za nchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo na kuwachukulia hatua za kinidhamu Watendaji ambao katika maeneo yao pamedhihirika kuwepo kwa uvunjifu huo wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso hili linakusudia kuongeza uwazi, uwajibikaji na uzalendo katika matumizi ya Fedha za Umma, kila senti iweze kuleta tija katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hoja ya baadhi ya Halmashauri kutorejeshewa ghamama za Matibabu kutoka *NHIF* (hana naomba maneno *CHF* yaondolewe).

KWA KUWA *LAAC* imetoa ushahidi usio na shaka kwamba *NHIF* imekuwa haizirejeshei baadhi ya Halmashauri nchini ghamama za matibabu yanayotolewa na mamlaka hizo kwa wananchi wanaotumia Bima ya Afya ya *NHIF*;

NA KWA KUWA kitendo hicho kinasababisha hasara ya kifedha kwa Halmashauri husika huku *NHIF* ikinufaika;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuandaa na kutumia utaratibu wa kisasa zaidi unaowezesha fomu za wagonjwa wanaotumia huduma za Bima ya Afya ya *NHIF* kujazwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso hili likitekelezwa kikamilifu litapunguza upotevu wa fedha katika Halmashauri kutokana na kitendo cha *NHIF* kutorejesha fedha hizo kwa madai kwamba fomu husika zimejazwa vibaya. Pia pendekeso hili linakusudia kupunguza hoja ya ukaguzi katika Halmashauri kutokana na madai ya fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja kwamba baadhi ya Halmashauri zinashindwa kutumia ipasavyo Mashine za *POS* katika kukusanya mapato ya ndani:-

KWA KUWA *LAAC* imetoa ushahidi wa Halmashauri ambazo *POS* hazitumiki ipasavyo;

NA KWA KUWA kutumia kikamilifu mashine hizo ni sawa na kufanya hujuma dhidi ya mapato ya Serikali;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuimarisha ufuatiliaji na uwajibikaji katika matumizi ya mashine hizo ili ziweze kusaidia ipasavyo katika ukusanyaji, ufuatiliaji na udhibiti wa mapato katika Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linakusudia kuhimiza ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kudhibiti mianya ya upotevu na kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja kwamba baadhi ya Halmashauri haziwasilishi ipasavyo michango ya kila mwezi inayotokana na makato ya mishahara ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii:-

KWA KUWA *LAAC* imetoa mifano ya Halmashauri nchini zisizowasilisha ipasavyo michango ya kila mwezi inayotokana na makato ya mishahara ya watumishi kwenye mifuko husika ya hifadhi za jamii;

NA KWA KUWA kitendo hicho huleta usumbufu kwa watumishi husika pindi wanapostaafu kazi na ni kinyume cha sheria husika;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa michango ya kila mwezi kutoka katika makato ya mishahara ya Watumishi wa Umma iwasilishwe ipasavyo katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linakusudia kuwapa nafuu ya maisha Watumishi wa Umma wanapostaafu utumishi huo lakini pia kuziepusha Halmashauri dhidi ya adhabu ya riba kutoka mifuko hiyo pindi zinapowasilisha michango hiyo katika mifuko husika kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hoja ya Upotevu wa fedha kutokana na baadhi ya Halmashauri kutodai marejesho ya Kodi ya Ongezeko la thamani (*VAT*) katika miradi inayotekelawa na wafadhili:-

KWA KUWA *LAACimebainisha* mifano ya Halmashauri zilizokwama kunufaika na Agizo la Serikali Kuu la kudai *VAT* katika miradi ya maendeleo inayotekelawa kwa fedha za wafadhili;

NA KWA KUWA kitendo hicho kinazifanya mamlaka husika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa gharama kubwa zinazojuisha *VAT*;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maagizo yake katika Halmashauri kwa kuondoa *VAT* katika miradi inayofadhiliwa na wafadhili kwa lengo kupata tija inayokusudiwa katika maagizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linakusudia kuhimiza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati katika Halmashauri. Lina kusudia pia kusaidia Halmashauri ambazo vifaa vyao vimekwama bandarini kwa sababu ya kutolipiwa *VAT* ziweze kusaidiwa kupata vifaa hivyo bila ya kodi. Kwa ujumla wake pendekezo hili linakusudia kupunguza gharama za Serikali katika utekelezaji wa miradi ili fedha zinazookolewa zitumike kuboresha huduma nyingine za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii yamezingatia Hoja za Ukaguzi wa *CAG* kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoa na majibu ya baadhi ya Maafisa Masuuli waliohusika

katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo yanakusudia kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo kwa wananchi. Kamati inaliomba Bunge lako lijadili na kuyaafiki maoni na mapendekezo yaliyotolewa ili Serikali iweze kuyapa uzito unaostahili katika kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashukuru kwa Uongozi wako ulioiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inakushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wao. Aidha, Kamati inaishukuru Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa umakini na ufanisi wake katika kuratibu na kushauri vyema utekelezaji wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba shukrania zangu ziwafike Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Dismas Muyanja na Ndugu Dickson Bisile, Ndugu Waziri Kizingiti na Watumishi wote wa Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Watendaji wa Serikali kutoka katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Divisheni ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa Ofisi ya Rais TAMISEMI hususani Kitengo cha Ukaguzi na Ufuatililaji wa Fedha katika Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufanuzi wa hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa *LAAC* kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapa kazi na naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifutavyo:-

- (1) Mhe. Abdallah Dadi Chikota -Makamu Mwenyekiti  
(2) Mhe. Ahmed Ally Salum - Mijumbe

- |     |                            |   |        |
|-----|----------------------------|---|--------|
| (3) | Mhe. Azza Hamad Hillal     | - | Mjumbe |
| (4) | Mhe. Conchesta L. Rwamlaza | - | Mjumbe |

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngombale, hayo majina yataingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kikanuni hutakiwi kuyasoma.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mapato na Matumizi ya Fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

## 1.0           **SEHEMU YA KWANZA**

### 1.0       **MAELEZO YA JUMLA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, ninakushukuru kwa ridhaa ya kuwasilisha Bungeni<sup>1</sup> Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Hesabu

---

<sup>1</sup> Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kukushukuru sana kwa kuiwezesha LAAC na Bunge kwa ujumla kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, naomba kukupa pole kufuatia vifo vya Wabunge wenzetu; Mhe. Dkt. Augustino P. Mahiga (Mb), Mhe. Dkt. Gertrude P. Lwakatare (Mb) na Mhe. Richard M. Ndassa (Mb). Mwenyezi Mungu azijaalie roho za marehemu pumziko jema peponi. Amina.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kumteua Mjumbe wa LAAC Mhe. Dkt. Godwin A Molleli (Mb) kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hapo tarehe 16 Mei, 2020. Ninampongeza sana Mhe. Dkt. Molleli (Mb) kwa uteuzi huo na kumtakia mafanikio mema.

### **1.1 MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa majukumu ya kamati za kudumu za Bunge ni lbara ya 96(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977). Majukumu haya yamefafanuliwa kwa kina katika Kanuni za Kudumu za Bunge. Jukumu mahsusila la LAAC ni kufuatilia na kushauri kuhusiana na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Hoja za Ukaguzi wa CAG.

Utekelezaji wa majukumu haya hufanyika kwa njia mbalimbali kama vile vikao vya mahojiano ya kiuwajibikaji kati ya Kamati na maafisa masuuli, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kwa njia ya semina na warsha.

### **1.2 MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Miaka mitano ya Maisha ya Bunge la Kumi na Moja tangu Novemba, 2015 hadi Mei,

2020, LAAC imetekeleza Wajibu wake kikamilifu na kupata mafanikio yafuatayo:

- (a) Iliweza **kuwasilisha Bungeni kwa wakati Maoni na Mapendekezo** yake kuhusu Taarifa ZOTE za CAG zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi chote cha Maisha ya Bunge la Kumi na Moja;
- (b) Imeweza **kufuutilia kikamilifu utekelezaji wa mapendekezo yake** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusiana na ukusanyaji wa mapato ya ndani, udhibiti wa matumizi yasiyokuwa na tija na uboreshaji wa mifumo mbalimbali katika Mamlaka hizo hivyo kuchangia katika kuokoa fedha na mali za Serikali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (a) Iliweza **kuwasilisha Bungeni kwa wakati Maoni na Mapendekezo** yake kuhusu Taarifa ZOTE za CAG zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi chote cha Maisha ya Bunge la Kumi na Moja;
- (c) Iliweza kuishawishi Serikali **kufuta madeni** yaliyokuwa yakizikabili Halmashauri kutokana na malimbikizo ya michango katika Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ili Halmashuri zianze upya uchangiaji katika vikundi hivyo kwa mujibu wa Sheria;
- (d) Iliweza kuishauri Serikali **kufanya marekebisho ya Sheria** ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 ili Halmashauri ziweze kuchangia 10% ya mapato yao ya ndani katika Vikundi vya maendeleo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria;

- (e) Iliweza kuishawishi Serikali **kuharakisha uteuzi na uthibitisho wa Wakuu** wa Idara mbalimbali katika Halmashauri hivyo kuchochea uwajibikaji mionganii mwa Watumishi hao;
- (f) Iliweza **kushirikiana vyema na Vyombo** *vya Habari na Asasi* Mbalimbali za Kiraia kwa njia ya semina na Warsha hivyo kutekeleza kwa vitendo Dira ya *Bunge kuwa Imara na Sikivu kwa Wananchi* kwa kupata maoni ya Wananchi kupitia Asasi hizo;
- (g) Iliweza **kutumia ipasavyo teknolojia ya Bunge Mtandao (e- Parliament)** katika kutuma na kupokea taarifa hivyo kuwa kichocheo kwa taasisi zingine za umma nchini mathalani Halmashauri kuendesha shughuli zao kidijitali hivyo kuchangia katika kuokoa gharama za uendeshaji wa shughuli za Bunge na Serikali kwa ujumla;
- (h) Kupitia ushiriki wa Viongozi wake, **LAAC ilishiriki kikamilifu Vikao vyote** *vya Kamati ya Uongozi* hivyo kuwa sehemu ya Maamuzi na Mafanikio yaliyopatikana katika uendeshaji wa shughuli za Bunge la Kumi na Moja;
- (i) Ilichangia kudumisha **mahuiano mema ya kazi** kati ya Mhimilli wa Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango hivyo kuchangia pia katika kuboresha nidhamu ya matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa nchini; na
- (j) Iliweza kutekeleza majukumu yake kwa **umoja na mshikamano mionganii mwa Wajumbe wake** bila ya kujali tofauti za kiumri, makabila, jinsia, itikadi za kisiasa na elimu hivyo

kufanikiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa Kamati za Kudumu za Bunge ni Sehemu ya Bunge, imetupasa kuyaeleza mafanikio haya ili Bunge lako na umma kwa ujumla wafahamu tulichofanikiwa kupata katika muda wote ambao tulitumwa kazini. Nina imani kuwa mafanikio haya ni mafanikio ya Bunge kwa ujumla.

### 1.3 ***MUUNDO WA TAARIFA***

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ni hii ya Utangulizi. Sehemu ya Pili inabainisha Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya CAG (2018/19) pamoja na Mahojiano kati ya Kamati na baadhi ya Maafisa Masuuli wa Halmashauri.

Sehemu ya Tatu inaelezia Maoni na Mapendekezo ya LAAC kwa kila eneo liliobainika kuwa chanzo cha matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri.

### 2.0 ***SEHEMU YA PILI***

---

### 2.0 ***UCHAMBUZI WA TAARIFA YA CAG NA MATOKEO YA MAJADILIANO***

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, jumla ya Halmashauri 185 zilikaguliwa na CAG. Kati ya Halmashauri hizo, 176 sawa na 95% zilipata Hati Safi za Ukaguzi, Halmashauri 9 sawa na 5% zilipata Hati zenyе Mashaka. LAAC ilichambua kwa kina Taarifa ya Halmashauri hizo na kufanya mahojiano na Sampuli ya Maafisa Masuuli wa Halmashauri Kumi na Nne (14). Sampuli hii ilijumuisha Halmashauri zilizopata Hati Safi na Halmashauri zilizopata Hati zenyе Mashaka.

Baada ya mahojiano, LAAC imejiridhisha kuwa matokeo ya ukaguzi wa CAG yalizingatia miongozo stahiki ya ukaguzi wa fedha za umma kama vile masharti ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), *Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008* na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009, Sheria ya Fedha za Umma (2001), Sheria zingine za nchi, na viwango vilivyowekwa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kifungu cha 10 cha *Sheria ya Ukaguzi wa Umma (2008)* kinatamka kuwa ukaguzi anaoufanya CAG katika Taasisi za Umma nchini zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwa niaba ya Bunge, hivyo ninayoheshima kukuarifu kuwa hoja zilizoibuliwa na CAG katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 zinaakisi uhalisia uliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na zilijengwa katika misingi ya Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu za Ukaguzi wa hesabu za Serikali kitaifa na kimataifa.

## 2.1 *MWENENDO WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA*

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya jumla ya uchambuzi wa Taarifa ya CAG, mahojiano kati ya LAAC na baadhi ya Maafisa Masuuli na uhalisia uliopo katika utendaji wa Halmashauri vinaonesha kuwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri nchini inazidi kuimarika. Hali kadhalika mahitaji ya huduma za jamii kama vile elimu, afya, ulinzi, usalama, usafirishaji na uchukuzi vinazidi kuboreka. Vitendo vya rushwa mionganoni mwa Watumishi wa Halmashauri vinazidi kupungua.

Kutokana na hali hii, Shirika la *Transparency International* (*The Global Coalition Against Corruption*) katika Taarifa yake ya Mwaka 2019 inayojulikana kwa Jina *Overview of Corruption and Anti- Corruption in Tanzania* limeripoti kuwa kiasi cha rushwa mionganoni

mwa Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini Tanzania kimepungua kutoka 25% mwaka 2015 mpaka kufikia 10% mwaka 2019 huku asilimia ya Wananchi waliota rushwa ili kupata huduma katika Mamlaka hizo kikipungua kutoka 25% mwaka 2015 hadi 18% mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa vitendo vya rushwa kunaenda sanjari na ongezeko la uwazi na uwajibikaji mionganoni mwa Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hali hii imesababisha kupungua kwa matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha na mali za umma katika Mamlaka hizo. Ndiyo maana hoja za mishahara kwa watumishi hewa, miradi ya maendeleo kutekelezwa kwa muda mrefu na kesi za Wakurugenzi kushtakiwa kwa ubadhirifu vimepungua sana. Mazingira haya yamechangia sana ongezeko la idadi ya Hati Safi za Ukaguzi mionganoni mwa Halmashauri katika mwaka wa fedha wa 2018/2019.

## **2.2 *SABABU ZA MATUMIZI MABAYA YA FEDHA ZA UMMA KATIKA HALMASHAURI***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za CAG katika kipindi cha Miaka Mitano ya Uhai wa Bunge la Kumi na Moja unaonesha kuwa sababu za kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kugawanywa katika maeneo makubwa mawili. Kwa maana ya sababu zinazotokana na taratibu za Serikali Kuu na sababu zinazotokana na mwenendo wa Halmashauri zenyewe. Kwa kutumia mifano ya mwaka wa fedha 2018/19, sababu hizo zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:

### **2.2.1 *Sababu zinazotokana na Serikali Kuu***

**Mheshimiwa Spika**, taratibu za Serikali Kuu zinazochangia kuwepo kwa matumizi mabaya ya

fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ni pamoja na:

(a) **Kutowasilisha ipasavyo Ruzuku ya Fedha za Maendeleo katika Halmashauri**

**Mheshimiwa Spika**, LAAC imebaini kuwa katika mgao wa fedha za ruzuku ya maendeleo, zipo halmashauri zinazopokea fedha zaidi ya kiasi kilichotengwa, zipo halmashauri zinazopokea kiasi punghufu cha fedha zinazotengwa na zipo pia halmashauri zinazopewa kiasi stahiki lakini kwa kuchelewa.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Halmashauri 26 (**Kiambatisho A**) zilipokea jumla ya shillingi 22.8 billioni ziliwa ni zaidi ya fedha zilitengwa kutumika katika miradi yote ya maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na 31% ya bajeti nzima ya fedha za maendeleo iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri zote nchini<sup>2</sup>. Hoja ya LAAC ni kwamba halmashauri husika mara nyingi zinakuwa hazikujipanga kutumia kiasi hicho cha fedha na mara nyingine zinakuwa hazina rasilimali watu ya kutosha kusimamia matumizi hayo.

Aidha, katika Mwaka huo huo 2018/19, halmashauri 157 hazikupelekewa jumla ya shilingi 556.8 billioni za ruzuku ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha **2015/16** kiasi cha Tsh. 620 billioni sawa na 61% hakikupelekwa, katika mwaka **2016/17** kiasi cha Tsh. 532.2 billioni sawa na 51% ya bajeti ya maendeleo hakikupelekwa, katika mwaka **2017/18** kiasi cha Tsh. 480 billioni sawa na 49% ya bajeti ya maendeleo hakikupelekwa. Katika hali kama hiyo ni vigumu kwa Halmashauri husika kutekeleza kikamilifu mipango yao ya maendeleo. Lakini pia Halmashauri zinaonekana

---

<sup>2</sup> Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2018/19). Hoja Na. 4.4.1

kuwa zimetumia vibaya kiasi kidogo cha fedha zilizopokea kwa sababu kinakuwa hakitoshi kukamilisha miradi hiyo

Vilevile, katika mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya TZS.258.6 bilioni zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hazikutumika kwa sababu zilipelekwa mwishoni mwa mwaka husika wa fedha<sup>3</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inaona hii ni hoja ya msingi kwa sababu ucheleweshaji huo umesababisha shughuli husika zisitekelezwe kwa wakati; na Halmashauri husika zimepata hoja za ukaguzi kwa kutokutumia kikamilifu fedha walizotumiwa kufikia mwisho wa mwaka husika wa fedha.

- (b) **Urasimu katika Kukamilisha Malipo ya Wakandarasi Mheshimiwa Spika**, miradi mbalimbali katika Halmashauri inatekelezwa na Wakandarasi ambao hulipwa madai yao baada ya Serikali kuhakiki usahihi wa madai hayo. Utaratibu uliopo sasa kwa ajili ya kuhakiki hati za madai yao huanzia kwa **Mkandarasi** kwenda kwa **Mkurugenzi Mtendaji** wa Halmashauri husika kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa (**RAS**), RAS hupeleka **OR- TAMISEMI** kisha kwenda **HAZINA**. Kamati inaona kuwa utaratibu huo una urasimu mkubwa unaochangia miradi husika kutotekelezwa kwa wakati. Miradi kadha wa kadha katika halmashauri mbalimbali imechelewa kutekelezwa kutokana na urasimu huo. Mfano dhahiri ni kuchelewa kwa ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Mji wa Bariadi.
- (c) **Mfumo wa EPICOR kutofungamanishwa kikamilifu na mifumo mingine muhimu ya uandaaji wa taarifa za fedha.**  
**Mheshimiwa Spika**, pamoja na masuala mengine, Mfumo wa EPICOR ni msaada mkubwa katika

---

<sup>3</sup> Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2018/19). Hoja Na. 4.6.2

kuimarisha ufuutiliaji na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za umma nchini; na pia katika uandaaji wa Taarifa za Mwisho za Fedha (*Final Accounts*). Hata hivyo, LAAC imebaini kuwa Mfumo huu haujaunganishwa kikamilifu na mifumo mingine, ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Halmashauri (LGRCIS), Mfumo wa Bajeti (PLANREP), Mfumo wa Taarifa za Fedha unaotumiwa katika ngazi za chini za Serikali (FFARS), na mfumo wa kielectroniki wa malipo ya mishahara ya watumishi(LAWSON).

Sanjari na hoja hii, LAAC imebaini pia kwamba katika bahadhi ya Halmashauri, makusanyo ya fedha yanafanyika kwa kutumia stakabadhi za kawaida, na malipo ya manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali yanapokelewa kwa kutumia risiti za kawaida zisizo za kielectroniki. Hali hii inachochea udanganyifu na wizi katika mapato yanayokusanya na inachangia kwa Halmashauri kutoa taarifa za fedha zisizo sahihi hivyo kuwapotosha watumiaji wa taarifa hizo katika maamuzi muhimu.

## **2.2.2 Sababu zinazotokana na Mwenendo wa Halmashauri Zenyewe**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) zipo sababu za aina mbalimbali zinazochangia matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Sababu hizo ni pamoja na upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali, udhaifu wa vitengo vya ukaguzi wa ndani, utaalam mdogo wa watumishi katika baadhi ya Halmashauri katika kutathmini na kuibua fursa za maendeleo katika maeneo yao, mila na desturi za wakaazi wa baadhi ya maeneo, vitendo vya rushwa na majanga ya asili. Hata hivyo, Taarifa hii itaangazia zaidi maeneo matano yafuatayo ambayo Taarifa ya CAG 2018/19 iliyajengea hoja zaidi:

(a) **Kukiukwa kwa Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi ya umma vipo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa manunuzi hayo yanakuwa na tija kwa nchi. LAAC imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zinakiuka miongozo hiyo. Kutowana na ukiukwaji huo, Taarifa ya CAG kwa Mwaka 2018/19 inaonesha kuwa jumla ya Tsh. 9.2 bilioni zilitumika kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa mbalimbali bila idhini ya bodi ya zabuni katika halmashauri 47 (**Kiambatisho B**).

Taarifa ya CAG kwa mwaka 2018/19 inaonesha pia kuwa, jumla ya Halmashauri 43 zilifanya manunuzi ya bidhaa zenye thamani ya Tsh. 5.01 bilioni na kuzitumia bidhaa hizo kabla ya kukaguliwa na Kamati za Ukaguzi na Upokeajji wa Bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inaona kuwa suala hili ni hoja ya msingi kwa sababu kiasi cha manunuzi ya bidhaa zinazotumika bila kukaguliwa kinazidi kukua na kutia shaka kama kweli bidhaa hizo zinakuwa zimenunuliwa au la!. Kwa mfano<sup>4</sup> katika mwaka 2016/17 Halmashauri 25 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Tsh. 0.6 bilioni, Mwaka 2017/18 Halmashauri 31 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Tsh. 1.4 bilioni na Mwaka 2018/19 Halmashauri 43 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Tsh. 5.01 bilioni na kuzitumia bila kukaguliwa ukiukwaji huu unasababisha hasara kubwa kwa Serikali.

(b) **Baadhi ya Halmashauri kutokutumia ipasavyo Mashine za POS katika kukusanya mapato ya ndani.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa ujumla imetumia gharama kubwa kununua mashine za kielektroniki kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika

---

<sup>4</sup>Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2018/19)  
Jedwali Namba 9-11

vituo mbalimbali (POS) kwenye Halmashauri. LAAC imebaini kuwa kuna udhibiti mdogo wa mashine katika kukusanya mapato. Baadhi ya Halmashauri zinashindwa kufikia maoteo kutokana na uvujaji wa mapato kutokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa kutosha katika matumizi ya mashine hizo. Ni vema OR-TAMISEMI ikaimarisha ufuatailiaji katika suala hili ili matumizi hayo yaweze kuwa na tija zaidi kwani kwa sasa kuna changamoto zifuatizo:

- i. Baadhi ya Halmashauri za Wilaya kama vile Lushoto, Mbulu, Tarime na Siha zinaendelea kukusanya mapato kwa njia ya risiti za vitabu vyta kawaida ambazo makusanyo yake hayawezi kufuatiliwa na kubainika kirahisi katika mifumo ya mapato. Makusanyo kwa kutumia njia kama hizo mara nyingi hayafikishwi katika Halmashauri kutoka katika vituo vyta makusanyo.
- ii. Katika baadhi ya Halmashauri kuna idadi kubwa ya mashine hizo ambazo zimesajiliwa lakini hazionekani kwenye mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano; Katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha mashine 65 hazikuonekana kwa muda wa siku zaidi ya mia moja. Halmashauri zingine ni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, mashine 22 hazikuonekana zaidi ya siku thelathini, na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ambako mashine 12 hazikuonekana kwa zaidi ya siku mia moja. Maana yake ni kwamba upo uwezekano wa mashine hizo kutumika kukusanya mapato ambayo hayataonekana katika mfumo hivyo kusababisha uvujaji wa mapato katika Halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inaona suala hili ni hoja muhimu kwa sababu inachangia

sana katika kudorora kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani hatimaye udhaifu katika utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi.

(c) **Halmashauri kutorejeshewa Gharama za Matibabu kutoka NHIF**

**Mheshimiwa Spika**, halmashauri zinatoa fedha kwa ajili ya kupata dawa na vifaa tiba kutoka kwenye Bohari ya Dawa (MSD). Vifaa na dawa hizo hutumika katika matibabu kwa wananchi wanaotumia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Changamoto kubwa katika utaratibu huu ipo katika marejesho ya gharama za matibabu kutoka NHIF kwenda kwa Halmashauri zillzotoa huduma. Halmashauri nyingi zimekuwa hazirejeshewi gharama hizo kwa hoja ya NHIF kwamba *Form za Matibabu zimejazwa vibaya*. Katika mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya Tsh. 2.02 billioni hazikurejeshwa katika Halmashauri zote nchini. Baadhi ya Halmashauri na hasara zilizopata ni: Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe (Tsh. 298.9 milioni), Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe (Tsh. 118.8 milioni), Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali (Tsh.116.4 milioni) na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela (Tsh.104.5 milioni)

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inaona suala hili ni hoja muhimu inayopaswa kushughulikiwa kwa sababu limeanza kuwa eneo jipya la upotevu wa mapato ya halmashauri linalokua kwa kasi na kuathiri mapato ya halmashauri na lina mwelekeo wa kuathiri ubora wa huduma za matibabu kwa wananchi. Aidha, suala hili linakuwa zito zadi kutokana na mwenendo uliobainika kuwa MSD pia haipeleki katika Halmashauri kiasi cha dawa kulingana na

fedha zinazotolewa na HAZINA hivyo kuchangia uhaba wa dawa katika Halmashauri.

- (d) **Baadhi ya Halmashauri kutowasilisha Makato ya Kisheria ya Mishahara ya Watumishi katika Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii.**

**Mheshimiwa Spika**, ni takwa la kisheria kwa Waajiri kupeleka makato ya kila mwezi ya mishahara ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Lengo ni kuwawekea akiba watumishi hao kwa siku za baadae hususani baada ya kustaafu utumishi. LAAC imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri haziwasilishi makato hayo au zinachelewa kuwasilishi. Tabia hii imekuwa ikikomaa badala ya kupungua. Kwa mfano: mwaka 2016/17 hazikuwasilishwa Tsh. 0.96 billioni, mwaka 2017/18 hazikuwasilishwa Tsh. 1.05 billioni, mwaka 2018/19 hazikuwasilishwa Tsh. 1.5 billioni.

**Mheshiniwa Spika**, LAAC inaona kuwa hoja hii ni ya msingi kwa sababu inahusu mustakabali wa Watumishi na familia zao wanapostaaifu. Hoja hii pia ni ukiukwaji wa Sheria za nchi na ni hasara kwa Halmashauri husika pale zinapotakiwa kulipa riba kwa kupeleka makato hayo nje na muda husika.

- (e) **Baadhi ya Halmashauri kutodai marejesho ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) katika miradi inayoteklezwa na wafadhili**

**Mheshimiwa Spika**, kuititia Waraka Namba 6 Kumb. Na. CLA 321/369/02 wa tarehe 22 Januari, 2018, kutoka HAZINA na Maagizo ya OR- TAMISEMI kuititia barua Kumb. Na. CCE. 383/ 509/01 ya tarehe 15 Februari, 2018, Halmashauri nchini zilielekezwa kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani

katika miradi yote inayofadhiliwa na wafadhili nchini.

Kutokana na Waraka huo Halmashauri mbalimbali kama vile Halmashauri ya Mji wa Bariadi ziliingia Makubaliano na Wafadhili mathalani Shirika la Maendeleo Duniani (UNDP) kwa lengo la kutekeleza miradi yao kwa gharama nafuu. Hali iliyopo kwa sasa ni kwamba Wizara ya Fedha inasita kutoa msamaha wa kodi hiyo kwa hoja kwamba msamaha huo siyo sehemu ya makubaliano yake na Benki ya Dunia.

Kwa msingi huo Halmashauri zilizoanza miradi kwa kutegemea ufadhili huo zimeshindwa kusonga mbele. Baadhi ya Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Mji wa Bariadi kuititia Mradi Namba 00099419 iliyokubaliana na UNDP kupata Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Tsh. 747.5 milioni ikitegemea kusamehewa VAT.

Halmashauri zingine ni pamoja na Kyerwa ambayo katika utekelezaji wa Mradi chini ya Mkataba Na. LGA/137/2017/2018/ADMIN BLOCK/W/04 haikurejeshewa kiasi cha Tsh. 118.9 milioni ambazo zingeisaidia kujenga vyumba kadhaa vya madarasa. Halmashauri ya Wilaya ya Monduli katika utekelezaji wa Mkataba Na. LGA/004/2016-2017/RWSSP/W/01 hajarejeshewa kiasi cha Tsh. 164.7 milioni ambazo zingeisaidia katika ujenzi wa matundu kadhaa ya vyoo shulenii. Halmashauri ya Mji wa Nzega katika kutekeleza Mkataba Na. LGA/170/2017-18/06 haikurejeshewa kiasi cha Tsh. 66.8 milioni ambazo zingeisaidia kuchimba visima kadhaa vya maji katika maeneo yenye uhaba wa maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona changamoto iliyoelezwa hapo juu inachangia

sana ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo kama vile miradi ya maji safi na salama na usafi wa miji katika Halmashauri mbalimbali nchini.

### **3.0 SEHEMU YA TATU**

---

#### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanyika katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii umebainisha maeneo Nane (8) yenye changamoto katika mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kimsingi, maeneo hayo ndiyo yenye Hoja za Ukaguzi katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Maeneo hayo yanahuusu:

- (1) Fedha za ruzuku ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutopelekwa ipasavyo katika Halmashauri;
- (2) Kutokufungamanishwa kikamilifu kwa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato na ufungaji wa hesabu za Serikali;
- (3) Urasimu katika kupitisha Hati za Malipo ya Wakandarasi;
- (4) Upotevu wa mapato ya Halmashauri kutokana na kutorejeshewa ipasavyo gharama za matibabu kwa njia ya bima ya afya kutoka NHIF;
- (5) Baadhi ya Halmashauri kutowasilisha ipasavyo michango inayotokana na makato ya kila mwezi ya mishahara ya watumishi katika mifuko ya hifadhi za jamii;
- (6) Baadhi ya Halmashauri kutozitumia ipasavyo mashine za kukusanya mapato vituoni (POS);

- (7) Baadhi ya Halmashauri kutozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha na manunuzi ya umma katika kutekeleza miradi ya maendeleo, na
- (8) Baadhi ya Halmashauri kushindwa kudai VAT katika miradi ya maendeleo inayotekelawa kwa kutumia fedha za wafadhiri.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizo orodheshwa hapo juu, Kamati inaliomba Bunge liafiki maoni na mapendekezo yafuatayo ili yaweze kutekeleza na Serikali

3.1 **Kuhusu Hoja ya Serikali Kuu kutowasilisha ipasavyo ruzuku ya fedha za maendeleo katika Halmashauri**

**KWAKUWA** LAAC imetoa ushahidi usio na shaka kwamba ruzuku ya fedha za maendeleo haipelekwi ipasavyo katika Halmashauri. Zipo Halmashauri zinazopelekewa fedha nyingi kuliko kiasi kilichoombwa, wakati zingine zinapelekewa fedha pungufu na kwa kuchelewa, **NA KWAKUWA** kitendo hicho kinaathiri utekelezaji wa mipango ya Mamlaka husika katika kuboresha huduma za jamii,

**KWAHIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali idumishe utaratibu wa kupeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria ya Matumizi inayotungwa na Bunge katika Mwaka husika wa Bajeti ili Mamlaka hizo ziweze kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekazo hili linakusudia kuihimiza Serikali kuongeza juhudini katika ukusanyaji wa mapato na kupeleka ipasavyo fedha

zinazokusanywa ili zikaboreshe maisha ya Wananchi kwa wakati.

**3.2 Kuhusu Urasimu katika Kupitisha Hati za Malipo ya Wakandarasi.**

**KWAKUWA** ni dhahiri kuwa Serikali imeweka urasimu mkubwa katika kuhakiki hati za malipo ya Wakandarasi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hati zikiwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji zinapelekwa Mkoani (RAS), kutoka Mkoani zinapelekwa OR-TAMISEMI kisha Wizara ya Fedha na Mipango (HAZINA).

**NA KWAKUWA** urasimu huu ni mionganini mwa sababu kubwa za kuchelewesha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaishauri Serikali ione uwezekano wa kupunguza urasimu huu kwa kupunguza mamlaka za uchambuzi na tathimini ya Hati hizo. Kwa mfano; Hati hizi zingweza kupelekwa moja kwa moja OR-TAMISEMI kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji ili OR-TAMISEMI izipeleke katika Wizara ya Fedha na Mipango (HAZINA) huku RAS akipata nakala za ushahidi wa mchakato unavyoendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekezo hili linakusudia kuweka mazingira yatakayo changia kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri kwa wakati.

**3.3 Kuhusu Hoja ya Mfumo wa EPICOR kutofungamanishwa kikamilifu na mifumo mingine ya udhibiti wa mapato na uandaaji wa taarifa za fedha.**

**KWAKUWA** LAAC imetoea ushahidi usio na shaka kwamba katika baadhi ya Halmashauri

mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya usimamizi, ufuutiliaji, udhibiti wa mapato na ufungaji wa hesabu za mwisho za Serikali (*Government Final Accounts*) hajafungamanishwa kikamilifu,

**NA KWAKUWA** kitendo hicho kinachochaea upotevu wa mapato na udhaifu katika ufungaji wa hesabu za Serikali,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaitaka Serikali kufungamanisha kikamilifu mifumo ya EPICOR, PLANREP, LAWSON, FFARS na Got HoMIS ili iweze kupashana habari za kifedha kwa uwazi na ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekazo hili linakusudia kuisaidia Serikali kupata manufaa mapana zaidi kutohana na matumizi ya mifumo hiyo ambayo kutofungamanishwa kwake kunapunguza kiasi cha manufaa hayo.

#### 3.4      **Kuhusu Hoja ya kukiukwa kwa Sheria za fedha na Manunuzi.**

**KWAKUWA** LAAC imetoa ushahidi usio na shaka kuhusu baadhi ya Halmashauri zilizohusika na ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya huduma na bidhaa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo,

**NA KWAKUWA** ukiukwaji huo ni uvunjifu wa sheria za nchi na ni mionganoni mwa mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma nchini,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaitaka Serikali kuzingatia sheria za nchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo na na kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji ambao katika

maeneo yao pamedhihirika kuwepo kwa uvunjifu huo wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekazo hili linakusudia kuongeza uwazi, uwajibikaji na uzalendo katika matumzi ya fedha za umma ili kila senti iweze kuleta tija katika maendeleo ya taifa

**3.5 Kuhusu Hoja kwamba Baadhi ya Halmashauri hazirejesewi Gharama za Matibabu kutoka NHIF**

**KWAKUWA LAAC** imetoa ushahidi usio na shaka kwamba NHIF imekuwa haizirejeshei baadhi ya Halmashauri nchini gharama za matibabu yanayotolewa na Mamlaka hizo kwa Wananchi wanaotumia bima za afya chini ya NHIF,

**NA KWAKUWA** kitendo hicho kinasababisha hasara ya kifedha kwa Halmashauri husika huku NHIF ikinufaika,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaitaka Serikali kuandaa na kutumia utaratibu wa kisasa zaidi unaowezesha form za Wagonjwa wanaotumia huduma za bima ya afya chini ya NHIF kujazwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekazo hili likitekelezwa kikamilifu litapunguza upotevu wa fedha katika Halmashauri kutokana na kitendo cha NHIF kutorejesha fedha hizo kwa madai kuwa form husika zimejazwa vibaya. Lakini pia Pendekazo hili linakusudia kupunguza hoja za ukaguzi katika Halmashauri kutokana na madai ya fedha hizo.

**3.6 Kuhusu Hoja kwamba Baadhi ya Halmashauri zinashindwa kutumia ipasavyo Mashine za POS katika kukusanya mapato ya ndani.**

**KWAKUWA** LAAC imetoa ushahidi wa Halmashauri ambamo POS hazitumiki ipasavyo,

**NA KWAKUWA** kutotumia kikamilifu mashine hizo ni sawa na kufanya hujuma dhidi ya mapato ya Serikali,

**KWA HIYO BASI** Bunge linaitaka Serikali kuimarisha ufuatiliaji na uwajibikaji katika matumizi ya mashine hizo ili ziweze kusaidia ipasavyo katika ukusanyaji, ufuatiliaji na udhibiti wa mapato katika Halmashauri nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekezo hili linakusudia kuhimiza ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kudhibiti mianya ya upotevu na kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na huduma zingine za kijamii katika Halmashauri.

3.7     **Kuhusu Hoja kwamba Baadhi ya Halmashauri haziwasilishi ipasavyo michango ya kila mwezi inayotokana na makato ya Mishahara ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii.**

**KWAKUWA** LAAC imetoa mifano ya Halmashauri nchini zisizowasilisha ipasavyo michango ya kila mwezi inayotokana na makato ya mishahara ya watumishi kwenye mifuko husika ya hifadhi za jamii,

**NA KWAKUWA** kitendo hicho huleta usumbufu kwa watumishi husika pindi wanapostaafu kazi na ni kinyume na sheria husika,

**KWAHIYO BASI** Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa michango ya kila mwezi kutoka katika makato ya mishahara ya

Watumishi wa umma inawasilishwa ipasavyo katika Mifuko husika ya hifadhi za Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekezo hili linakusudia kuwapa nafuu ya maisha watumishi wa umma wanapostaafu utumishi wao lakini pia kuziepusha Halmashauri dhidi ya adhabu ya riba katika mifuko hiyo pindi zinapowasilisha michango katika Mifuko husika kwa kuchelewa.

- 3.8     **Kuhusu Hoja ya Upotevu wa fedha kutokana na baadhi ya Halmashauri kutodai marejesho ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) katika miradi inayotekelizwa na wafadhili**

**KWAKUWA** LAAC imebainisha mifano ya Halmashauri zilizokwama kunufaika na Agizo la Serikali Kuu la kudai VAT katika miradi ya maendeleo inayotekelizwa kwa fedha za Wafadhili,

**NA KWAKUWA** kitendo hicho kinazifanya Mamlaka husika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa gharama kubwa zinazojuisha VAT,

**KWAHIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maagizo yake katika Halmashauri kwa kuondoa VAT katika miradi inayofadhiliwa na Wafadhili kwa lengo kupata tija inayokusudiwa katika maagizo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekezo hili linakusudia kuhimiza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati katika halmashauri. Lina kusudia pia kuzisaidia Halmashauri ambazo vifaa vyao vimekwama bandarini kwa sababu za kutolipiwa VAT ziweze kusaidiwa kupata vifaa hivyo bila ya kodi hiyo. Kwa ujumla wake pendekezo hili linakusudia kupunguza

gharama za Serikali katika utekelezaji wa miradi ili fedha zinazookolewa zitumike kuboresha huduma zingine za jamii.

#### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii yamezingatia Hoja za Ukaguzi wa CAG kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 pamoja na majibu ya baadhi ya Maafisa Masuuli waliohusika katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka huo. Mapendekezo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo kwa wananchi. Kamati inaliomba Bunge liyajadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa illi Serikali iweze kuyapa uzito unaostahili katika kuyatekeleza.

#### **5.0 SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakushukuru kwa Uongozi wako ulioiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inamshukuru pia Naibu Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson, Mb na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wao. Aidha, Kamati inaishukuru Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bw. Stephen Kagaigai kwa umakini na ufanisi wake katika kuratibu na kushauri vema utekelezaji wa shughuli za Bunge. Hivyo, naomba shukrani zangu zimfike Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndg. Dismas Muyanja, Ndg. Dickson M. Bisile, Ndg. Waziri Kizingiti na Watumishi wote wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru sana Watendaji wa Serikali kutoka katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi hususani Divisheni ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa Ofisi ya Rais TAMISEMI hususani Kitengo cha Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Fedha katika Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara

ya Fedha na Mipango (HAZINA) kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufanuzi wa hoja mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa LAAC kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapa kazi, na ninaomba kuwatambua kwa majina yao kama ifutavyo:-

- |     |                                    |                     |
|-----|------------------------------------|---------------------|
| 1.  | Mhe. Vedasto Edgar Ngombale, (Mb), | <b>MWENYEKITI</b>   |
| 2.  | Mhe. Abdallah Dadi Chikota, (Mb)   | <b>M/MWENYEKITI</b> |
| 3.  | Mhe. Ahmed Ally Salum, (Mb)        | Mjumbe              |
| 4.  | Mhe. Azza Hamad Hillal, Mb         | Mjumbe              |
| 5.  | Mhe. Conchesta L. Rwamlaza, (Mb)   | Mjumbe              |
| 6.  | Mhe. Ezekiel Magolyo Maige, (Mb)   | Mjumbe              |
| 7.  | Mhe. Faida Mohammed Bakar, (Mb)    | Mjumbe              |
| 8.  | Mhe. Alex Raphael Gashaza, (Mb)    | Mjumbe              |
| 9.  | Mhe. Juma Kombo Hamad, (Mb)        | Mjumbe              |
| 10. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, (Mb)   | Mjumbe              |
| 11. | Mhe. Martin Mtonda Msuha, (Mb)     | Mjumbe              |
| 12. | Mhe. Prof. Norman A. S. King, Mb   | Mjumbe              |
| 13. | Mhe. Rose Kamili Sukum, (Mb)       | Mjumbe              |
| 14. | Mh. Tauhida Cassian Gallos, (Mb)   | Mjumbe              |
| 15. | Mhe. Anastazia J. Wambura, (Mb)    | Mjumbe              |
| 16. | Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb    | Mjumbe              |
| 17. | Mhe. Dkt Godwin O. Mollel (Mb)     | Mjumbe              |
| 18. | Mhe. Edward F. Mwalongo, (Mb)      | Mjumbe              |
| 19. | Mhe. Eng. Christopher Chizza (Mb)  | Mjumbe              |
| 20. | Mhe. Mangungu Ali Issa, (Mb)       | Mjumbe              |
| 21. | Mhe. Mary Pius Chatanda, (Mb)      | Mjumbe              |
| 22. | Mhe. Seif Ungando Ally, (Mb)       | Mjumbe              |
| 23. | Mhe. Selemani J Zeddy, (Mb)        | Mjumbe              |
| 24. | Mhe. Tunza Issa Malapo, (Mb)       | Mjumbe              |
| 25. | Mhe. Yussuf Kaiza Makame, (Mb)     | Mjumbe              |
| 26. | Mhe. Zainab Mussa Bakar, (Mb)      | Mjumbe              |

## **6.0 HOJA**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo

ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

.....  
Vedasto Edgar Ngombale, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU  
ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**

27 Mei, 2020

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti ameshawasilisha, kwa hiyo, ni muda wetu sasa wa kuchangia. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia, lakini kabla hamjaanza kuchangia kama tulivyoanza na CAG, wakati tukijadili Taarifa ya Kamati ya PAC, CAG bado yupo kwa ajili ya kusikiliza yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wanazungumza.

Kwa hiyo, tutambue uwepo wa CAG na Timu yake yote, yeye yupo pale *Speakers Gallery* na Wasaidizi wake pia wapo humu Bungeni kwa ajili ya kusikiliza maelekezo ambayo Bunge litatoa. *(Makof)*

Tutaanza na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Engineer Christopher Chiza ajiandae. *(Makof)*

Wakati huo huo niwasome Waheshimiwa Wabunge ambao watachangia kutokea Msekwa ili kama wapo humu ndani waende Msekwa. Mheshimiwa Ahmed Salim, Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Tunza Malapo watachangia kutokea Msekwa. Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Kamati ya *LAAC*. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe, kwa kazi nzuri, pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake kwa kazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi Kamati hii naifahamu miaka mingi sana. Nampongeza sana *CAG* kwa kazi nzuri. Sasa hivi ni Halmashauri chache ambazo zinapata Hati chafu. Halmashauri nyingi zinapata Hati safi. Zamani haikuwa hivyo, Halmashauri nyingi zilikuwa zinapata Hati chafu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu ya ukaguzi wanakwenda kuwekwa ndani. Zamani ilikuwa ni Kamati moja ya *PACinakagua* na hesabu za Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, naziomba sana Halmashauri zisilalamike kwamba kwa nini wanapata Hati chafu. Halmashauri ambazo zinapata Hati chafu, zinashindwa kujibu Hoja za Ukaguzi. Wanashindwa kabisa. Utakuta Halmashauri ina hoja za Ukaguzi 20 wanajibu hoja mbili, lazima watapata Hati chafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya kuna baadhi ambazo mapato yake ya ndani ni chini ya asilimia 50. Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa tulishaagiza, Halmashauri zijitajidi kukusanya mapato ya ndani, wasitegemee sana ruzuku ya Serikali, kwani inachelewa kufika katika Halmashauri na wakati fulani fedha ambayo inafika ni kidogo sana. Sasa nilikuwa nashauri kwamba wakusanye haya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, mwaka huu 2020, Waziri wa TAMISEMI aligawa mashine 7,227 kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato. Mpaka leo kuna Halmashauri ambazo zinatumia risiti za vitabu. Kwa mfano, Halmashauri ya Lushoto, Mbulu na Tarime bado wanatumia risiti za vitabu. Zile mashine ambazo Mheshimiwa Waziri aligawa hazitumiki. Sasa hapa lazima kuwe na upotevu mkubwa sana wa fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI awachukulie hatua Halmashauri hizi. Kwa nini hawatumii zile mashine za kukusanya mapato? Utekelezaji wa Miradi mingi sana umekwama, ni kwa sababu mapato yanayokusanya hayawezi kukamilisha ile miradi. Kuna baadhi ya Halmashauri ambao wanategemea misaada ya wafadhili, wanakwama kutekeleza miradi au wanategemea sana fedha za Serikali Kuu, ambayo inafika kidogo au inachelewa au haifiki kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri, wakusanye mapato yao ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji katika Halmashauri; Halmashauri inapofanya vibaya, kwa mfano Halmashauri imepata Hati chafu mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na mwaka wa tatu, yule Mkurugenzi achukuliwe hatua, siyo ahamishiwe Wilaya nyngine. Sasa unafanya vibaya katika Wilaya hii, unahamishiwa Wilaya nyngine. Kwa hiyo, wachukuliwe hatua pale pale Wakurugenzi walipo badala ya kupelekwa katika Halmashauri nyngine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Kamati za Fedha na Mipango na Uongozi. Hizi Halmashauri zinasimamiwa na Madiwani. TAMISEMI walishatoa kibali kwamba Kamati ya Fedha na Mipango ikae kila mwezi ili kuona mapato na matumizi ya Halmashauri. Bahati mbaya kuna baadhi ya Watendaji wanatumia hizo fedha vibaya halafu wanapeleka Taarifa katika Halmashauri. Naomba sana Kamati za fedha wakatae kuzibariki zile Taarifa na wahoji kwa nini Mkurugenzi ametumia fedha vibaya? Naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niendelee tu kuzipongeza Halmashauri zile ambazo zinafanya vizuri. Serikali za Mitaa ni Serikali kamili. Katiba Ibara ya 146 na zinapaswa kukusanya mapato, zinapata ruzuku. Naiomba Serikali, kama vyanzo vingi nya mapato vilichukuliwa na Serikali Kuu, basi Serikali ipeleke zile fedha kufidia lile pengo ambalo vyanzo vyake Serikali ilichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kodi ya majengo hivi sasa inakusanya na *TRA*, sasa mwaka mzima fedha haziwasilishwi na Halmashauri wana miradi mbalimbali. Kwa hiyo, naomba angalau miezi sita *TRA* wakashakusanya kodi ya majengo, basi wapeleke zile fedha kwenye Halmashauri ili ziweze kutekeleza ile miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kumpongeza Mwenyekiti na Kamati yake kwa kazi nzuri na nimpongeze *CAG* kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng. Christopher Chiza* na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya ambapo naendelea leo katika vipindi hivi nya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Spika, Mheshimiwa wetu na wewe pia kwa kunituea katika vipindi viwili mfululizo kuhudumia katika Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejifunza mengi, nilivyoingia tofauti na ambavyo naondoka. Pia namshukuru Mheshimiwa Spika kwa malezi yake aliyonipa nikiwa Mbunge

wakati natekeleza majukumu yake. Pia sisi kama Kamati tunamshukuru kwa kutupa ushirikiano wa aina mbalimbali. Tumejengewa uwezo kupitia Taasisi mbalimbali ikilwemo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na Mdhhibit (CAG), Mradi wa LSP // na Asasi nyingine tumejengewa uwezo wa namna ya kuzisimamia na kuzikagua Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu imekuwa na mafanikio mengi katika kipindi chote cha miaka mitano. Moja ya mafanikio toka tunaanza, kulikuwa kuna tatizo la Watumishi wa Halmashauri ambao walikuwa wanakaimu kwa kipindi kirefu. Tatizo hilo limepatiwa ufumbuzi Watumishi wengi wameweza kuteuliwa na kuthibitishwa kuwa Wakuu wa Idara. Hiyo imesaidia kuchochaea ubora katika utendaji kazi wao na ili tu pia limesaidia kupunguza madeni yanayotokana na posho ya kualimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuongeza fedha za miradi. Fedha za miradi zimeongezeka mara dufu tofauti na tulivyokuwa tunaanza mwaka 2016. Hii imechangiwa na Serikali kuamua 40% ya bajeti ielekezwe katika miradi ya maendeleo na 60% ibaki katika shughuli za kawaada zikiwemo mishahara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Mitaa kipindi cha nyuma ni 5% tu ilikuwa inapelekwa katika Miradi ya Maendeleo. Leo hii hata Halmashauri ya Serikali za Mitaa 40% inatengwa kupelekwa katika Miradi ya Maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fedha nyingi zinazopelekwa kuna changamoto ya baadhi ya halmashauri kupelekewa fedha nyingi kuliko halmashauri zingine. Kwa mfano nataja halmashauri tatu, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ilipelekewa fedha za miradi ya maendeleo kwa zaidi ya asilimia 139, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma walipelekewa kwa zaidi ya asilimia 163 na Manispaa ya Sumbawanga walipelekewa zaidi kwa asilimia 132.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zote zina changamoto sawa na halmashauri zingine. Wananchi ni walewale, miradi wanayotekeleza ni ile ile, lakini kuna halmashauri utakuta inapelekewa fedha za miradi ya maendeleo chini ya asilimia 80. Tunaomba Serikali iangalie kuwe na msawazisho halmashauri zote zipelekewe sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukagua taarifa za hesabu kumekuwa na hoja ilijojitokeza ya upotevu wa mapato yanayotokana na marejesho ya Bima ya Afya ya Mfuko wa Afya *NHIF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura 2015 aliyahaidi wananchi atakapoingia madarakani sasa itakuwa basi mwananchi anapoenda hospitali na kuandikiwa karatasi tu bila kupata huduma yoyote au dawa; maneno aliyoaongea ameyatekeleza. Tumeona upelekwaji wa fedha wa zaidi ya asilimia 90 katika halmashauri zetu. Lakini kuna kitu ambacho kinaleta mkanganyiko; kumekuwa na tatizo halmashauri hizi zimekuwa hazifanyiwi marejesho kutokana na ujazwaji mbaya wa fomu. Kwa mfano halmashauri ya Wilaya ya Liwale milioni 71 kwa mwaka huo uliokaguliwa hazikurejeshwa na Bima ya Afya kwa sababu ya ujazaji wa fomu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naweza kusema hapa kunaweza kuwa na hujuma ya kutengeneza mazingira ya kupotea kwa fedha za afya ili kurudisha nyuma juhudzi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais. Hebu tuangalie, sidhani kama kuna hospitali ya binafsi au maduka ya dawa ambao wanakubali fedha zisirudi kutokana na ujazwaji mbaya wa fomu. Hili limeshamili sana katika halmashauri nyingi na ndio maana limekuwa tatizo hata kwenye taarifa yetu. Mimi nashauri hatua madhubuti zichukuliwe kwa watumishi watakaosababisha fedha zisirudishwe. Milioni 71 Liwele ziwengeweza kununua mashuka au zingeweza kununua vitendea kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulivyokuwa tunaanza hatukuanza na tatizo hilo lakini mwishoni haoa kumeshamili

kutowasilisha michango katika Mifuko ya Jamii na makato katika taasisi mbalimbali. Tatizo hili linajikita zaidi kwa watumishi ambao wanalipwa mishara yao kutokana na mapato ya ndani. Tatizo hili si tu litakuwa usumbufu kwa wanaostaafu bali hata hao watumishi ambao wanalipwa kwa mapato ya ndani kutokana na kususua kwa mapato wanakosa haki ya kupewa mikopo na taasisi za fedha kwa sababu hakuna uhakika wa kurudisha yale makato katika taasisi zilizowakopesha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mfano halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inadaiwa shilingi milioni 200 ya makato ambayo hayakupelekwa *LAPF*, hiyo ni *principle*, lakini liba ni milioni 600; inatokana na mishahara inayolipwa kwa watumishi wanaolipwa kwa mapato ya ndani. Mimi nashukuru kwa kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Tunajua dhahiri kabisa asilimia 40.....

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa tu taarifa mzungumzaji anayeendelea kuchangia kwamba kwa takribani sasa miaka mitano na tumeshatoa taarifa kwenye Wizara ya Utumishi tuna watumishi 38 wanaolipwa kwa mapato ya ndani ambayo inatugharimu halmashauri ya Lushoto zaidi ya shilingi milioni 26 kila mwezi tunayolipa kama sehemu ya mishahara nampa tu hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa naipokea kwa asilimia 100. Aliyoyasema Mheshimiwa Shangazi ni kweli, kwa sababu tukumbuke asilimia 40 ya mapato ya ndani imeenda kwenye miradi ya

maendeleo, asilimia 10 imeenda kuwezesha vile vikundi, kuna gharama ya uendeshaji na kuna gharama ya kulipa Waheshimiwa Madiwani. Kwa hiyo inaleta tatizo kwa watumishi wanaolipwa mishahara ya ndani inafikia mahali wanalipa tu *net salary* ile *basic* ambayo inatakiwa iende kwenye makato mbalimbali inashindwa; na halmashauri nyininge zinafikia mahali zinakopa fedha katika Mfuko wa Amana au fedha za maendeleo kwa ajili ya kulipa hiyo mishahara, kwa hiyo tunatengeneza deni lingine katika mkopo katika Mfuko wa Amana au fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza niipongeze Serikali; sasa hivi inaa jiri watendaji wa kata na wengine wanaingizwa katika Fungu la *GS2 and above* ambapo wanalipwa luzuku ya Serikali lakini watumishi hawa ni ambao walijirilwa kabla Serikali haijanza kuajiri yenye, ni halmashauri zilikuwa zinaajiri zenye. Naishauri Serikali ione namna sasa iweze basi kuwarithi hawa watumishi ili wasiingie kwenye matatizo haya. Wengine wanapopokea mishahara tarehe 21 hawa wengine hawajui uhakika wa mishahara yao italipwa lini. Ninaishauri sana Serikali ianze kuwarithi polepole na kuwapunguzia mzigo halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Engineer Christopher Chiza atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza ni-declare *interest* na mimi ni mjumbe wa Kamati ya *LAAC*. Mimi nashukuru kwamba kwa muda wote niliokuwa Bungeni sikuwa kuwa katika Kamati ya *LAAC*. Hata niliporejea mwaka 2018 nikapangiwa *LAAC* nilijaribu kukataa lakini baadae Mheshimiwa Spika akaniambia wewe umekaa huko kilimo, maji kila siku hebu nenda *LAAC* ujifunze mambo mapya. Kwa

kweli muda huu wa miaka miwili na nusu nimejifunza mambo mengi mapya katika Kamati hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais. Unajua msingi wa ukaguzi, Bajeti ni fedha kupatikana zitumike halafu ndio muone mianya ile ambayo inaleta ubadhilifu ndio wanakagua. Sasa kwa nini nampongeza Mheshimiwa Rais halmashauri zinakusanya mapato yake ya ndani, Serikali Kuu pia inakusanya pesa zake wakati mwingine na si wakati mwingine sisi wenyewe ndio tunatunga sheria inapeleka fedha kwenye halmashauri hasa za maendeleo. Sasa jana nimefarijika kweli niliposikia kwamba tayari *Bark Gold* wamechangia dola milioni 100, bilioni 250. Hizi ni fedha ambazo baadaye ukitazama zitakwenda tena kuingizwa katika mfuko wab Bajeti ndio hizo tena zitakwenda kwenye halmashauri zetu; kazi yetu sasa ni kuhakikisha kwamba fedha hizi ziklenda kule zitumike vizuri. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake wote na wale wote waliokabidhiwa mamlaka ya kumshauri ili waendelee kumshauri na kwa miaka mingine mitano aendelee kutuongoza namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijasahau kukupongeza wewe na Mheshimiwa Spika kwa jinsi kiti chako kinavyoongoza Bunge hili; nimeshuhudia mara nyngi kiti chako kikirekebisha. Na nawashukuru waliotangulia kuchangia katika Bajeti hii ya leo na nyngine zilopita si Bajeti, katika mjadala huu. Kiti chako siku zote kimekuwa kinatusaidia namna ya kuchangia; kama ni Muswada wa Sheria kwamba jikite kwenye Muswada, kama ni hoja kama hii jikite hapo, kama ni Bajeti Kuu jikite hapo, kwa kweli nakushukuru sana kwa kuwa huchoki wewe kila wakati watu wakipotoka wewe unawaelekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningeshauri tu kwamba Bunge ijalo inshaalaah na Mwenyezi Mungu anasikia huko aliko wote kuanzia wewe na Mheshimiwa Spika tunarudi tu. Sasa muandae utaratibu ili Waheshimiwa Wabunge wapate hiyo dozi. Ukitazama kuanzia *day one*

watu wengine wakianza kuchangia mtu anahama anakwenda huku badala ya kuchangia hoja iliyoko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ningeshauri tukirudi tena hata kama haturudi lakini Bunge litarudi lazima basi muandae utaratibu hata kama ni semina Waheshimiwa Wabunge wafundishwe wajue kabisa namna ya kuchangia ni moja, mbili, tatu ili tuwe *very efficient* katika kuchangia. Nawapongeza waliotangulia wote leo wamekwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijasahau, naomba nimpongeze Mwenyekiti wangu kwa uwasilishaji mahiri, amewasilisha vizuri sana, na naomba Waheshimiwa Wabunge mkubali, mzipokee hizo hoja na mpitisha maazimio yake. Nimalizie pongezi kwa kumpongeza ndugu yetu CAG Kichele; kwa kweli sisi kama Kamati ya AAC tuna kila sababu ya kumshukuru. Ametangulia kusema Mheshimiwa Leah Komanya; mimi nataka niseme ametujengea uwezo sikuwa katika Kamati hii lakini mara ya kwanza tulikuwa tunakwenda kukagua miradi hujua hata unaanza wapi kuhoji, lakini Ndugu Kichele huyu akasema hebu niwafundishe namna ya kuhoji maswali ya kuuliza mpaka mbinu zote za kumhoji Afisa Masuuli ili angalau afunguke wakati sisi tunamhoji. Kwa nakushukuru sana Mheshimiwa Kichele kwa kuwa umetujengea uwezo na nina hakika Kamati hii ya AAC baadaye utakayoyaona yatakuwa makubwa au bora zaidi kuliko taarifa uliyoionna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwa upande wa CAG. Mimi nimekuwa najiuliza kila tukipitia *reportza CAG*, nyingi tu, ambazo zinatuibulia mambo mengi ubadhilifu wa fedha, matumizi mabaya, kutokufuata taratibu za manunuzi *financial discipline* na wakati mwingine ni pesa nyingi tu zimepotea, lakini sasa ukija kuuliza kwamba inakuwaje; zamani sisi tulizoea *auditor anapofika* akifika tu *auditor watu wanaanza* kutetemeka, kwa sababu *auditor* anaweza akaondoka na mtu; lakini sasa nikawa najiuliza inakuwaje *CAG* anakagua anaibua mambo mengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yanapotufikia huku unakuta mengine yameshapita miezi mingi tu mingine ni ya miaka miwili iliyopita lakini watu wale bado wapo wamepata nafasi ya kujijandaa kama si kujibu au kutengeneza mambo mengine ambayo hayastahili. Nilipouliza nikaambiwa sisi tunatumia mfumo wa *West Minister (West Minister model)* katika ukaguzi, tofauti na wenzetu kama Uganda ambao wao CAG akienda kukagua akiona madudu anakagua hapo hapo akiwa na polisi na *TAKUKURU*. Kwahiyo kwa wao akiona madudu hangojei mpaka miaka mitatu, minne anaanza kuya-*arrest* na kuyashuhugulikia yale mambo halafu ndipo anampelekea taarifa yule aliyemtuma ili hatua nyingine za kinidhamu zichukuliwe. Sisi kidogo bado ni tofauti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda katika eneo hili mimi ni maamuma, lakini ungeniuliza niseme nini sasa, mimi ningesema; kwa nini basi tutsitunge sheria Bunge limruhusu CAG; inawezekana kuna *process* ngumu lakini kwani kuna kinachoshindikana? sielewi ni *article* gani lakini kama nilivyokuwa nafuatilia ni kama *article* 1432; CAGapate meno mambo mengine aweze kuya-*arrest* pale pale tusije kuyagundia baada ya miaka mitatu, minne? Kwahiyo mimi nafikiri na nashauri kabisa ikiwezekana kama ni marekebisho katika sheria hiyo inayompa Mamlaka CAG basi ifanyiwe marekebisho au tutunge sheria impe mamlaka CAG aweze kukabiliana na matukio kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika jana nilivyosikia kwamba CAG alikagua hata yale mashirika na makampuni makubwa ambayo zamani hakuweza kuyakagua; makampuni ambayo Serikali ama ina hisa au ina *interest*; jana mimi nilifarjika kusikia kwamba anafanya hivyo. Kwahiyo mimi ningefurahi zaidi kama Serikali au kama Bunge tukiishauri Serikali ikamuongezea meno CAG ili aweze kupambana na matukio kama hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, naomba nichangie eneo la matumizi mabaya ya fedha za Serikali; ukisoma *report* nafikiri ni 2.2. Kwakweli bado matumizi mabaya yapo; kuna

*improvement* kubwa tu lakini matumizi mabaya ya fedha yapo. Kwa mfano taarifa ya CAGinabainisha kwamba shilingi bilioni 9.2 zilitumika kinyume; yaani hazikutumika kwa utaratibu, yaani zote hizo bado zina hoja. Ni watu tu wamefanyia maamuzi fedha za Serikali, bilioni 9.2 mtu anafanya tu maamuzi. Wakati mwengine ukiwaliza Maafisa Masuhuli wengine hata zile tunazozita *the dos and don'ts* hawajui. Taratibu hizi unakuta hawajui na mwengine ukimhoji zaidi anasema aha ningejua mambo ni haya basi uteuzi huu nisingeukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi nafikiri bado liko tatizo katika matumizi mabaya ya fedha za Serikali; na ukienda zaidi utakuta ni maeneo kama ya mikataba. Mikataba ni mingi ambayo ukiitazama kwa undani haina viwango. Tullikuwa tunaangalia halmashauri moja juzi tu hapa wametoa mkataba wa vibanda kwa miaka 144. Sasa unajiliza, kama hawa watu wangekuwa na Mwanasheria anayeweza kusoma tu aka-*interpret*, hivi unaweza ukampa mkataba mtu eti nimekukabidhi hii utaendesha kwa miaka 144, hata ye ye mwenyewe hatokuwepo nafikiri. Lakini hii ni kwa sababu unakuta hawana wataalamu pale, hata wanasheria wa kuwa- *guide* hawapo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia eneo lingine juzi tu tukaangalia kuna mkataba Halmashauri ya Bariadi imeingia na *UNDP* na wakatoa shilingi milioni 700 tayari *upfront* wamezitoa kwa ajili ya manunuzi ya magari na vifaa fulani nafikiri ya vitendea kazi, fedha hizo mpaka sasa hazijatumika, vifaa vimelala bandarini na wameshindwa kuvi-clear. Sababu ni moja tu katika mkataba ule ambao Bariadi imeingia na *UNDP*, hawakuweza kuingiza *close* ile kwamba *tax exemption* lazima iwepo. Sasa nimekwenda Serikalini *tax exemption* hakuna, milioni 700 zimetolewa, badala ya kutumikia wananchi fedha zile zimelala na mashine zile bado zipo kule katika bandari. Sasa ni eneo ambalo kama hawa watu wangekuwa na wataalam haya mambo yasingejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri ya 43 katika taarifa ya CAG imetumia shilingi bilioni 5.01 kufanya manunuzi kiholela, *this is the lots of money*. Yaani mtu hafuati taratibu za manunuzi zilizowekwa kwa utaratibu wake, lakini fedha hizo ametumia na hawezhi hata kuzirejeshi. Sasa hii inaonyesha dhahiri kwamba bado kuna matumizi mabaya ndani ya halmashauri, halmashauri zetu zinahitaji kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini naishauri Serikali; mimi ushahauri wangu ni kwamba Serikali kama tulivyokuwa tunafanya huko nyuma wakati wa kuanzisha hizi Serikali za Mitaa tukasema tufanye *decentralization*, tupeleke watalaam tujenge *capacity* kwenye ngazi ile. Serikali ifanye hiyyo wawekwe maafisa mipango ndani ya halmashauri wanaoweza kupanga kwamba bwana nikitoa mkataba huu nisitoe mkataba wa miaka 144 wenye uwezo; maana pale ndipo Bajeti ya Serikali inapoanza kupanga. Tuwe na wakaguzi wa ndani (*internal auditors*), hao ndio wanaoweza kutazama sasa haya madudu yanayotokea kule ili kabla hayajatokea waweze kuya-*arrest*, lakini watu hao ukienda unakuta mara nyingi wenyewe ndio hoja zimejikita kwao, kwamba kitengo cha ndani hakipo *efficient* au hakina watalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi mimi ushauri wangu ni kwamba Serikali ijenge *capacity* kwenye halmashauri zetu, watalaam wote waliobobea kama ni Maafisa Mipango, ni Wanasheria, wote ukiwatazama ni wazuri *experience* wako juu hawako ndani ya halmashauri na ndio maana tunapata hoja nyingi ambazo hazijibiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia hili la NHF lakin sasa Mheshimiwa Leah amelizungumzia; naomba nimalizie kwa jambo moja tu la mwisho ambalo ni suala la makato ya kuchangia mifuko ya jamii kutoka kwenye halmashauri. Kwa kweli eneo hili limekuwa ni sugu na nadhani halipo kwenye halmashauri tu hata waajiri wengi hawapeleki makato michango ile ya watumishi matokeo yake watumishi hawa wana-*suffer* wakati wanapostaafu. Watumishi hawa wana wake zao, wana familia, wana wajukuu.

Ameshastaafu hana mbele wala nyuma tena anategemea pesa zake hizi lakini anakwenda kule anakuta fedha hizo hazijapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano makato ya mishahara ambayo watumishi mpaka leo bado hajjapelekwa. Mwaka 2016/2017 nafikiri zilikuwa milioni 0.96, sikumbuki, nadhani ni halmashauri ya Ukerewe, sikumbuki, 2017/2018 pia kuna bilioni 1. 05, 2018/2019 bilioni 1.5; hizo ni halmashauri kama tatu, jumla ya bilioni 3.51. Sasa halmashauri zote kama kila moja itakuwa hivi, hawapeleki, watumishi wote hawa wa halmashauri watakapostaafu wanakuta fedha zao hazijapelekwa wakienda kudai. Sisi Waheshimiwa Wabunge hawa watu wanatulilia kila wakati, unapokwenda Bungeni naomba fedha zangu, sijalipwa hiki na kile, wanakupa na makaratasi chungu mzima. Naomba Wizara au Serikali isimamie halmashauri, ipeleke michango ya wastaafu, hawa watu wameshakuwa watu wazima, wanahitaji kuanzisha miradi yao na wale ambao hawajajenga wanahitaji kujenga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa kwa kweli niwaombe Wabunge wenzangu wote, haya mapendekezo ambayo tunayafanya kazi Bunge liyaidhinishe na naomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mezani ya taarifa yetu ya mwaka ukizingatia kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC na katika kipindi changu cha miaka mitano katika Bunge hili nimetumika katika Kamati ya LAAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kusema kwamba tunashukuru kuwa katika Kamati

hii, tumejifunza mambo mengi na kusema ukweli Kamati hizi ni darasa na tunatoka huku tukiwa tumefuzu kabisa. Wengine siyo ma-auditor lakini tumeweza kukagua halmashauri, tumeweza kuhoji Maafisa Masuuli ni kwa sababu tumewezeshwa kabisa na Ofisi ya Spika pamoja na CAG. N inaposema CAG nasema Ofisi nzima ya CAG, siwezi kutamka fulani na fulani lakini Ofisi nzima ya CAG wametusaidia sana katika kuhakikisha wanatuwezesha, wanatujengea uwezo kabisa wa kuweza kufanya kazi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumeweza kupata afya njema mpaka siku ya leo na nina uhakika tunakwenda kumaliza Bunge hili vizuri kabisa, licha ya mambo ambayo yanajitokeza. Hizi naziita *gymnastic* za kisiasa, lazima tuzikubali tukijua kwamba hiyo ndiyo siasa, hakuna woga, tunakwenda mbele, hivyo, twende kupambana huko kwenye uchaguzi mkuu na *Insha Allah* Mungu ataturudisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokagua halmashauri hizi huwa tunakuwa *guided* na CAG katika taarifa yake na ziko hoja mbalimbali ambazo tunazifanyia kazi. Kwa hiyo, tutajaribu kuangalia hoja ambazo wengine wamesema, lakini mimi nitasema kwanza hoja moja ambayo ni sugu yaani tuseme kwamba ni donda ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja ambayo Kamati imesema ya Serikali kutopeleka fedha za ruzuku katika halmashauri na ukumbuke kwamba halmashauri hizi zilinyang'anywa kabisa mapato mengi au vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vinaziwezesha kufanya kazi. halmashauri zilizo nydingi sasa hivi ni maskini, baada ya kunyang'anywa vyanzo vyake, tulitegemea kwamba Serikali itaweza kupeleka ruzuku ya maendeleo katika halmashauri ili halmashauri hizi ziweze kutoa huduma kwa wananchi kwa sababu hizi ndizo zilizo karibu na wananchi, zinatoa service, lakini pia zinatekeleza Sera za Serikali Kuu. Kwa hiyo ni lazima zipate pesa ya kutosha ili ziweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii katika halmashauri haiwezi kujibiwa na halmashauri zenyewe. Hoja hii inapaswa kujibiwa na Serikali Kuu ili halmashauri ziweze kufuta hoja hii, maana yake halmashauri zinaposhindwa kufuta hoja basi kwao inabaki kwa kweli siyo kitu kizuri. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itimize na ifute hoja zake ndani ya halmashauri ambazo ni wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zinapofanya Bajeti huwa kuna kitu kinaitwa *ceiling* yaani ukomo wa bajeti. Kwa hiyo, ina maana halmashauri zinaweka bajeti kutokana na *ceiling* ya Serikali ambayo mimi inanipa imani kwamba kama Serikali imeweka *ceiling* ni kwamba itatimiza bajeti ile, vinginevyo basi wasingekuwa wanaweka *ceiling* au tafsiri yake ni kwamba, Serikali inaweka *ceiling* ambao haina uwezo basi wa kutimiza bajeti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa yetu tumejaribu kuonesha ni namna gani Serikali imeshindwa kupeleka pesa kwa ajili ya maendeleo. Mwaka 2015/2016 Serikali imeshindwa kupeleka bilioni 620 za maendeleo katika halmashauri zetu, mwaka 2016/2017 imeshindwa kupeleka bilioni 532; mwaka 2017/2018 imeshindwa kupeleka bilioni 880; mwaka 2018/2019 imeshindwa kupeleka bilioni 556.8. Kutokana na hali hii halmashauri zetu hazina uwezo wa kutekeleza miradi ya maendeleo na haziwezi kuhudumia wananchi, kama Serikali inashindwa kupeleka pesa hizi ndani ya halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishauri Serikali, kama haina uwezo wa kupeleka pesa hizi basi iweke *ceiling* ambayo ina uwezo wa kuitekeleza. Tusiweke bajeti ambayo hatuna uwezo wa kupata pesa za kupeleka. Hoja hizi zinaelemea halmashauri na sisi inatupa kazi, wale Wajumbe wa Kamati ya LAAC waliopo sisi na wengine watakaokuja watakuta maendelezo ya hoja hizi ambazo haziwezi kujibika. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe inapeleka pesa kwenye halmashauri zetu. Kwenye halmashauri ndiko kuna watu, kwenye halmashauri ndiko kunatolewa huduma, kwenye halmashauri ndiko kuna miradi ya maendeleo, sasa kama

Serikali inashindwa kupeleka pesa hizo tunachotegemea ni nini katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kutoka katika almashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuacha kuongelea juu ya halmashauri kushindwa kupeleka makato katika mifuko ya kijamii. Tulichokigundua halmashauri hizi zina madeni mengi sana na ni makubwa, lakini tukaona kwamba halmashauri inashindwa kuyalipa kwa sababu kuna *interest* au riba ambazo zinatolewa na Mifuko ya Jamii, yaani zinatolewa kama *penalty* pale ambapo halmashauri imeshindwa kupeleka zile pesa. Katika taarifa ya mwaka jana tulisema wazi kwamba Serikali ikakae na Mifuko hii ili waone kama wanawenza waka-*come to the compromise*, kwamba madeni hayo ambayo ni *interest* yafutwe ili halmashauri hizi ziweze kulipa madeni haya kuwawezesha wananchi au wastaa fu waweze kulipwa pesa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyokwambia wako Walimu wamestaifu miaka miwili, mitatu iliyopita, lakini hawajalipwa; kwa kweli lazima tuwaonee huruma. Mtu amefundisha watoto wa nchi hii miaka nenda, rudi, miaka 30 au 40, anastaifu halafu anakwenda kuwa ombo ombo. Halipwi kwa sababu Mifuko hii haina pesa za kuwalipa kwa sababu halmashauri hazi peleki pesa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu Madiwani kutopewa pesa zao, yaani kutolipwa posho, kutolipa madeni yao ambayo wanakatwa kihalali katika mishahara yao. Narudia hili, tuliweka katika taarifa ya mwaka jana, pamoja na kwamba Waziri alitoa tamko hapa, lakini nakwambia mpaka sasa hivi ziko halmashauri ambazo Wajumbe wao au Madiwani wana zaidi ya mwaka hawajalipwa posho; kwa kweli tunawanyanyasa. Kama sisi hapa tunalalamika, ni kwa nini Madiwani wanatendewa hivyo? Serikali basi ilibebe hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kwamba kama watu hawa wameshindwa kulipwa posho zao na mahali pengine hata vikao havikai. Unaweza kujiuliza halmashauri hii inaendeshwaje kama vikao havikai, maamuzi

yanatokana na nani? Kama kweli Madiwani hawa ambao wanapaswa kwenda kusimamia miradi mbalimbali ambayo kusema ukweli ni pesa nyingi ambazo wanapaswa kusimamia, watasimamiae wakati wenyewe wamekaa kilofa lofa, hawapewi pesa yao? Kwa kweli jambo hili, Bunge hili kabla hatujafunga tulisimamie kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasi wasi kwamba hata Madiwani watashindwa kupewa viinua mgongo vyao. Madiwani wanateseka, kwa mfano, ukienda kule Mkao wa Kagera, Halmashauri ya Kyerwa wana zaidi ya miezi 10 na zaidi hawalipwi. Inawezekana na Madiwani wengine wanaamua kunyamaza, mimi sinyamazi kwa sababu lazima tutetee wananchi, tunatetea watu wote na Bunge hili kazi yake ndiyo hiyo. Tuna-*dialog* halafu baadaye *we come to the consensus*, kwa hiyo najua kwamba ni lazima tuendeshe mjadala hapa ili tuwatetee wananchi, halafu baadaye chombo hiki sasa kiweze kuishinikiza Serikali na Serikali iweze kuwaambia Wakurugenzi ili waweze kuwasaidia na kuhakikisha kwamba Madiwani hawa wanalipwa pesa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni manunuzi ambayo hayafuli utaratibu ndani ya halmashauri. Hii imesemwa vizuri katika taarifa yetu, lakini kuna kitu kingine ambacho tumegundua kwamba hata wale watekelezaaji ndani ya halmashauri hawana uwezo na hata baadhi ya Wakurugenzi hawana uwezo wa kufanya hizi kazi kwa sababu wameteuliwa wengine kisiasa siasa tu. Tunategemea kwamba mtu ambaye anakuwa Mkurugenzi japokuwa wengine wame-*coup*, lakini anapaswa awe na uzoefu katika *local government* na ndiyo maana kuna Chuo pale Hombolo sijui mnakifanyia nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu ni lazima wawe *trained*, waweze kuhakikisha kwamba kazi ya *local government* iko tofauti na Serikali Kuu mimi nilivyoiona, kwa sababu ina-*deal* na wananchi na Mkurugenzi mara nyingi anakuta Madiwani wako wengine labda elimu ni ndogo ndogo na nini, kwa hiyo wanapaswa kuwa na uwezo wa

kuhakikisha wanaendesha *local government* jinsi sheria na utaratibu wake ulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiseme mengi najua Wanakamati watachangia, hatuwezi kusema wote hoja moja, hivyo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Pius Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala ajiandae

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Kamati yetu ya *LAAC* na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kumpongeza sana Spika na wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa namna ambavyo mmeweza kutulea na kutuongoza katika utendaji kazi na majukumu ambayo mmetukabidhi katika Kamati hii katika kipindi chote cha miaka mitano. Tumejifunza mambo mengi ambayo sisi wengine tulikuwa hatuyajui, tumefanya kazi na *CAG*, tunampongeza sana, sana, *CAG* wetu Kichere pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya *CAG* kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika kutusaidia sisi Kamati tulipokuwa tunakwenda kuzikagua hizi halmashauri na kuzihoji hizi halmashauri kwa sababu sisi hatuwezi tukafanya jambo lolote bila taarifa ile ya *CAG*. Maelekezo yale ya *CAG* ndiyo yanatusaidia sisi kubaini baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza katika halmashauri zetu. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Ofisi ya *CAG* kwa ushirikiano wao na kutuwezesha sisi kufanikiwa haya ambayo leo tunayazungumza ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa namna ambavyo imeweza kupeleka fedha za ruzuku ya maendeleo katika halmashauri zetu. Imekuwa ni tofauti na huko nyuma, miaka ya 2016 lakini miaka hii imeweza kupelekwa fedha za miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zetu na maendeleo yameonekana. Miradi

ambayo imefanyika kwenye halmashauri zetu inaonekana, lakini kumekuwepo na upungufu. Upungufu huu unatokana na utekelezaji kwa wenzetu wa Serikali Kuu. Kama ambavyo wenzangu wengine wametangulia kusema, Serikali Kuu imekuwa ikipeleka fedha kwenye halmashauri zingine kwa zaidi ya bajeti ambayo ilikuwa imetengwa. Hivyo zinazisababishia halmashauri hizo kuonekana zinakuwa na hoja za ukaguzi kwa sababu wamepewa fedha zaidi ya bajeti yao. Kwa hiyo, zile fedha zikishakwenda huko hawaelewi wazitumie namna gani, zinabaki zinarandaranda na wengine wanazitumia kwa kufanya ubadhirifu wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali Kuu ihakikishe kwamba inazi peleka fedha kulingana na Bajeti ilikuwa imetengwa kwa halmashauri hizo badala ya kupeleka zaidi ya fedha ambazo zillikuwa zimetengwa kwenye bajeti ya Halmashauri husika. Hata hivyo, kuna halmashauri zingine ambazo zinapelekewa fedha pungufu, matokeo yake wanababishiwa hoja kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba wameshindwa kutimiza au kukamilisha ile miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa imepangwa kwa sababu tu wanapelekewa fedha pungufu. Kwa hiyo, tuiombe Serikali Kuu inapopeleka fedha ipeleke fedha ya kutosha kulingana na bajeti ambayo walikuwa wametengewa ili waweze kutekeleza ile miradi na kuondokana na hoja za ukaguzi wa CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu kwenye halmashauri nyingine inapeleka fedha za maendeleo mwisho wa mwaka. Sasa unapopeleka fedha mwisho wa mwaka maana yake ni nini? Ni kwamba hao watashindwa kutekeleza ile miradi ya maendeleo, matokeo yake wanawatengenezea hoja za ukaguzi kwa CAG. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu kwamba jambo hili lirekebishwe ili kusudi basi halmashauri zote ziweze kuwa zinapelekewa fedha kwa mpango mzuri, siyo ule wa kucheleweshwa, mtu anapelekewa kipindi ambacho mwaka umeisha, halafu fedha zile zinavuka mwaka na hatimaye hawa wenzetu wengine, CAG anawajengea hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengine ambayo tumeyabaini ni pamoa na suala zima la ukusanyaji wa mapato. Niipongeze Serikali hususani TAMISEMI, hivi karibuniwalinunua *POS*za kutosha, wakazigawia halmashauri kwa ajili ya kukusanya mapato. Hata hivyo, ziko baadhi ya halmashauri mpaka sasa zinashindwa kuzitumia *POS*hizo kwa uaminifu, wanazichezesha *POS* hizo na kuzisababishia halmashauri kukosa mapato. Haya mambo tumeyabaini, tumeyaona kwenye ukaguzi wenzetu wa ukaguzi wametuonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuiombe TAMISEMI na wenyewe wana kitengo chao pale TAMISEMI, hebu waendelee kuzifua tilia hizi halmashauri ambazo wamepeleka hizi *POS*halafu zinatumika tofauti. Kwa kufanya hivyo wanapoteza mapato na ndiyo wanasababisha sasa halmashauri zingine zinashindwa hata kuwalipa Madiwani wao kwa kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hapa bila kumumunya maneno; Halmashauri ya Korogwe imeshindwa kuwalipa Madiwani wake miezi 10 na haifanyi vikao vya Kamati ya fedha. Inashindwa kuwalipa Madiwani posho zao za vikao. Halmashauri hiyo Madiwani walikatiwa Bima wameshindwa kupeleka fedha za Bima, Madiwani wanashindwa kutibiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe TAMISEMI halmashauri kama hizi zifuatiliwe kwa ukaribu. Sasa hivi wameshatoa Waraka TAMISEMI kwamba tarehe 10 Juni, 2020 ndiyo Mabaraza yanavunjwa, sasa je, hawa Madiwani ambao hawakulipwa miezi 10, hawa Madiwani ambao Bima zao hazikufanya kazi, haki zao watazipataje? Tuiombe TAMISEMI iendelee kufuatilia halmashauri hizi ambazo zimesababisha hao Madiwani, viongozi wenzetu hawa kushindwa kupata haki zao. Siyo jambo jema sana. Nimeona niliseme hili kwa mfano bila kumumunya maneno kwa sababu Madiwani wenzetu wanateseka, viongozi wenzetu wanateseka katika kupata haki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nani anataka kunipa taarifa? Anataka kunipa taarifa huyu mwenye halmashauri yake lakini ndivyo inavyokwenda, ndivyo ilivyo lazima ni seme kwa sababu niko kwenye Kamati hiyo na naona kinachofanyika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Naona pacha wako aliyezaliwa wakati mwingine anataka kukupa taarifa hapa. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba, siyo tu kulipwa na Bima ya afya, lakini tunapozungumza leo, wiki moja iliopita Madiwani 36 wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe wamepewa barua na Benki ya CRDB kutakiwa walipe mikopo na wasipolipa watakamatiwa mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali taarifa yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda unaipokea taarifa hiyo? (*Kicheko*)

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Naipokea, naipokea kwa sababu anayoyasema ndiyo tunayoyaona sisi kwenye ukaguzi wa hesabu zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe sana TAMISEMI hebu iliangalie jambo hili kwa sababu tunaelekea sasa kumaliza kuvunja bunge na kuvunja hizo mabaraza la madiwani hawa viongozi wenzenzu ambaao ni madiwani hatuelewi hatima yao itakuwa ni vipi kwa hiyo niombe sana Ofisi ya TAMISEMI ilione

jambo hilo na ione kwamba ni muhimu sana kwa wenzetu nao haki zao zikasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa sina mengi ilikuwa ni hayo kwa sababu yaliyo mengi ni haya tuliyoyazungumza kwenye Kamati yetu nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai ambayo leo nasimama mbele ya Bunge lako tukufu nikichangia hoja hii ya Kamati yetu ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana wewe kwa kutuongoza katika vikao ndani ya Bunge lakini nikushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunitfea kuingia kwenye kamati hii ya *LAAC* ambayo nimekuwepo huko kwa muda wa miaka mitano nimejifunza mengi, lakini niwapongeze sana wenyeviti wetu wa kamai ya *LAAC*. Lakini pia niwapongeze sana na kuwashukuru sana wanakamati wenzangu ambao tumeshirikiana vizuru kweli kweli katika kamati yetu ya *LAAC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze *CAG* nao ofisi yake wametuongoza vyema katika kamati yetu wametupa mafunzo na wametusaidia sana tuweze kufanya kazi yetu vizuri mpaka leo tunafika hapa tunawasilisha taarifa yetu mbele yako. Katika kufanya kazi zetu yapo mambo ambayo tumeyaona ambayo ni vizuri tukaishauri Serikali ikaendelea kuyafanya kazi na kusimamia vizuri halmashauri hizi za mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni suala linalohusiana na marejesho VATkwenye halmashauri ambazo zina miradi mkakati ziko halmashauri ambazo zinatekeleza miradi mikubwa ambayo inatokana na mkopo kutoka *World*

*Bank.* Ni jambo la kusikitisha sana kwamba suala la VAT kwenye hizi halmashauri linasumbua sana, utadhani kwamba Serikali halongei yaani utadhani kwamba Wizara ya TAMISEMI siyo wizara ndani ya Serikali yetu na wizara ya Fedha siyo wizara ndani ya Serikali yetu kwa sababu wanatumiana mpira kiasi ambacho kuna miradi imesimama, kuna miradi haitekelezeki yaani imefika mahala wakandarasi wameicha kwa sababu VAT hawarejeshewi, nan i TAMISEMI walienda semina kwa Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri hizi kwamba miradi hii itakayofadhiliwa kutokana na fedha za *World Bank* haitakuwa na VAT miradi imetekelvezwa wakandarasi wamefanya kazi VAThairejeshwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inafika mahala ukifuatilia ile *memorandum of understanding* kati ya Serikali ya Tanzania na *World Bank* kwenye kipengele cha VAT ipo *silent* kwenye kipengele cha kodi na wenyewe watu wa kodi kwa tafsiri kwamba ikiwa *silent* maana yake kodi inatakiwa ilipwe sasa fedha TAMISEMI watatoa wapi maana inhabidi Wizara ya Fedha iipe TAMISEMI fedha zipeleke halmashauri, halmashauri zimrejeshee mkandarasi vinginevyo itakuwa ni shida sana kwa hii miradi. Sasa miradi hii inakwenda mingine ina miaka mitano mingine miaka miwili, na inatofautiana hii miradi kunawengine wali *import* mashine kwa mfano Halmashauri ya Bariadi. Halmashauri ya Bariadi wame-*import* vifaa vya mji vimeduwa kama bandarini kwa sababu ya VAT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai ni kwenye Halmashauri yangu ya Mji Njombe, tunajenga stendi na soko, wakandarasi wanakwenda pole pole sana miradi imeshapitwa na wakati hadi muda ule tuliokulaliana wamalize hawamalizi kwa sababu VAT hakuna hairejeshwi. Sasa ukitaka Halmashauri kama ya Mji ilipe VAT hii ya hii miradi maana yake inatakiwa itowe zaidi ya bilioni tatu, halmsahauri bilioni tatu itatoa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba hapa Bunge tuishauri Serikali iongee na ikamilishe jambo hili ifike mahali wakubaliane nani anatoa hizo fedha na fedha

zitoke wakandarasi wapewe ili hii miradi iende vizuri vinginevyo miradi itaharibika na mraidi ukiaribika unamadhara menge sana, fedha ile ni ya mkopo inakuwa pale imelala wananchi hawapati huduma bora, lakini pia mkandarasi huyu anaafilisika na tunasema kwamba tuna taka wakandarasi wazawa waweze kufanya kazi vizuri watafanyaje kazi vizuri, watafanyaje vizuri kama wanafanya miradi inafika mahala miradi ile inakuwa haiwezi kuendelea kwa hiyo tuombe sana Serikali ilione hilo. Wizara ya fedha na Wizara ya TAMISEMI wakae waongee wafikie hatima ya VAT kwenye hii miradi ya kimkakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo tumeliona katika kufanya kazi yetu ni jambo la wahandisi ilipoanzishwa *TARURA* wahandisi kwenye halmashauri waliamishwa wakapelekwa *TARURA* kwa hiyo halmashauri zimebaki hazina wahandisi na kuna ule mpango wa ujenzi wa *force account* halmashauri zina majengo mengi sana zinajengwa unapita mnakagua mnakuta kuna mapungufu mengi yanajitokeza, lakini mapungufu haya yanajitokeza kwa sababu halmashauri hazina wahandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nijukumu la Serikali kuhakikisha kwamba zinaajiri wahandisi wenye sifa ili kusudi wazibe mapengo ya wale waliohamishiwa *TARURA*. Ninashanga sana kwa sababu *TARURA* ilipo anza ilitakiwa iajiri wahandisi kusudi wale walioko halmashauri wabaki halmashauri ili kusudi waendelee kusimamia ile kazi. Kuna majengo mengi tunajenga na hizi halmashauri, hayajengwi na kusimamiwa na wahandisi kwa sababu wahandisi wote wamehamishiwa *TARURA*, utaona tu wakati wa kujibu maswali anaazimwa mhandisi kutoka *TARURA* aje ajibu maswali. Sasa mwandisi wa kumuazima kwa ajili ya kuja kujibu maswali ya kiufundi ni kwamba huyo siyo mhandisi anayesimamia hizo kazi. Kwa hiyo, ni jambo gumu sana ushauri tunaoweza kuutoa kama Kamati, Serikali iajiri wahandisi ili kusudi waende wakasimamie halmashauri hizi katika masuala ya kiufundi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa hizi kazi ambazo zimefanyika kwa *force account*, halmashauri nyingi zimefanya kazi vizuri sana tumetembelea halmashauri ya Manispaa ya Iringa tumeona pale wana hospitali yao *FRELIMO* imejengwa vizuri sana. Lakini nimetembelea Halmashauri ya Makambako kuna Hospitali Mlowa imejengwa vizuri sana, imetembelea Halmashauri ya Lupembe imejengwa hospitali yake vizuri sana. Sasa na hospitali hizi zimejengwa kwa *force account*, ni hospitali nzuri zinaonekana zimekamilika lakini vifaa hakuna kwa hiyo, tuombe Serikali ifanye kila linalowezekana ipeleke vifaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hilo hilo na sisi katika mji wa Njombe tumejenga zahanati zetu katika Kata za Makovo na sisi tupelekewe vifaa kwa ajili ya zahanati hizi kwa sababu ni nguvu za wananchi na ni fedha za Serikali zimetumika pale. Kama majengo haya yataendelea kukaa kule bila vifaa maana yake ile thamani ya fedha itakuwa imepotea lakini pia wananchi hawatapata huduma waliokusu kuipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naweza kulisema ni suala la 10% za vikundi, halmashauri nyingi zinafanya vizuri sasa kwamba ile 10% ya mapato ya ndani inakwenda kwenye vikundi lakini zipo halmashauri zimeanza kuteteraka, zimeanza kutengeneza tena shimo kwa sababu madeni ya nyuma tulitoa ushauri na tukaiomba Serikali ifute madeni ya nyuma na ikafuta, lakini kuna halmashauri zimeanza kuchimba shimo jipya tunaomba sana Serikali isimamie zile halmashauri zisitengeneze mashimo kwenye fedha za vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine kwenye hizi fedha za vikundi leo tunasema hapa halmashauri zitoe 10% lakini nafikiri kuna haja ya kuangalia ukomo uwe wapi? Kwa sababu ziko halmashauri zinafedha nyingi sana, mfano mdogo tu ni Halmashauri ya Jiji Dodoma, Halmashauri ya Jiji Dodoma inabilioni sita makusanyo ya ndani ina maana fedha za vikundi ni bilioni 6.0 kutoka asilimia 10 ya bilioni 6.0 ni bilioni 6.0. Sasa bilioni sita zitaingia kwa mfululizo miaka

mingapi na kama Serikali inataka kwamba hizi fedha tuendelee kama sheria inavyotaka maana yake vile vitengo viimarishe, unaona kitengo cha huduma ya Maendeleo ya Jamii ambacho kinasimamia hii asilimia kumi kinawatumishi watatu. Mwaka huu mmewapelekea bilioni 6.0 za vikundi, mwaka mwingi bilioni 6.0 tayari zimeshakuwa bilioni 12, mwaka mwingine bilioni 6, bilioni kumi na nane watu watatu watasimamiae? Wasimamie kuchambua vikundi, wasimamie marejesho, kwa hiyo matokeo yake fedha hizi zinapotea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nishauri kwamba tuweke utaratibu ambao utafikia mahali utakuwa na ukomo kwamba halmashauri iingize katika mfuko huo fedha zifike kiasi gani kutokana na halmashauri jinsi ilivyo lakini kusema kwamba miaka yote kuendelea ku-pump hizo fedha kwenda huko unaweza kukuta kuna huduma nyingine muhimu sana kama hizo bilioni 6.0 zingeenda kufanya ingeweza kusaidia halmashauri lakini zinakwenda kwenye vikundi alifu hakuna utaratibu wa kukusanya vizuri kwa sababu watumishi walioko kwenye hizo halmashauri kwa kusaidia kukusanya ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalize kwa kusema ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini kwa ushirikiano walionipa kama Mbunge wao lakini ninawaomba tuendelee kushirikiana Njombe ni yetu na Tanzania ni yetu ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Ahmed Salim ajiandae.

**MHE. DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia taarifa muhimu kutoka kamati ya LAAC, kwanza kabisa naomba niipongeze kamati ya LAAC kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya na matunda ya kazi hiyo tumeanza kuyaona kwenye halmashauri mbalimbali kama taarifa ilivyoeleza tunaona

hati safi zimeongezeka kwa hiyo nashukuru sana kamati hii ya *LAAC* kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nimshukuru *CAG* kwa kazi nzuri ambayo ameifanya pia na nimeletewa taarifa dakika chache zilizopita nilikuwa nauliza mwenyekiti wangu wa halmashauri kama miradi yetu yote ya maendeleo ilikaguliwa na wakaguzi walipoenda amenihakikishia amesema Mheshimiwa Mbunge kwa kweli hawa wakaguzi kwa mara hii wamefanya kazi ambayo haijawahi kufanyika wamekwenda kila mradi wamekagua na tunatarajia watatoa taarifa yao. Kwa hiyo, *CAG* nakushukuru sana kwa kazi hiyo ambayo umeifanya na kwa kufanya hivyo maana yake tunauhakika ukaguzi sasa ile kitu tunaita *value for money audit* itafanyika vizuri na imefanyika vizuri nah ii itatusaidia kuona dhamani ya pesa inavyo tumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kueleza taarifa niliyoipokea ndani ya dakika tano zilizopita tayari Halmashauri ya Misenyi mapato ya ndani tumeweza kufikisha bilioni 1.5 hata kabla mwaka wa fedha haujakamilika. Hii maana yake ni nini, hii maana yake unapoweza kukusanya fedha za ndani ukavuka lengo maana yake hata ile asilimia 10 ya vijana, akinamama na walemvu wataweza kupata fedha yao kama ilivyokusudiwa. Na sina shaka halmashauri yangu inavyosimamiwa iklongozwa na Mbunge na Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi, sina wasi wasi wowote ule kwa jinsi ambavyo mwaka jana katika Mkoa wa Kagera tumeweza kupewa nishani ya kuweza kutoa fedha yote ya miradi ya maendeleo kama tulivyokuwa tumejipangia na Mifuko ya akinamama, vijana na walemvu na sasa kwa kweli akinamama, walemvu na vijana wakae mkao wa kula kwa sababu mwaka wa fedha haujaisha tayari fedha tumeshazikusanya sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati kwa ushauri na mapendekezo waliyoyatoa yote ni mazuri nayaunga mkono kwa asilimia 100 lakini kuna hili pendektezo la kwamba tupunguze ukiritimba wa malipo kwa

wakandarasi. Kwa kweli inabidi tuangalie jinsi ambavyo tutatekeleza ushauri huo wa kamati kwa sababu unapochelewesha malipo kwa mkandarasi maana yake huyu mkandarasi saa nyingine anakuwa amekopa kutoka kwenye benki. Kwa hiyo, unapomcheleweshea malipo maana yake unafanya kazi yake iwe ngumu na wengine wanaweza kufilisiwa na benki bila sababu. Kwa hiyo, naungana na kamati ilivyoshauri na niseme ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumzia pia miradi ya kimkakati, ile miradi ni muhimu sana tuangalie jinsi ya kuiwezesha. Kwa sababu ile miradi ya kimkakati itatusaidia kuongeza mapato ya halmashauri, na halmashauri yetu ya Misenyi tuna mpango wa kutoka bilioni 2.5 kwenda hadi bilioni 12 na tutaweza kufikia huko kama na Serikali pia itatusaidia kuwezesha Halmashauri zetu kuweza kuwa na miradi inayoweza kuongeza mapato ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa jinsi mnavyosimamia Bunge letu, nikushukuru wewe pia kwa sababu kuna kila dalili kwamba utachukua hatua sehemu fulani ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba niseme kwamba nakuunga mkono na wala usiogope kwa sababu woga ni silaha dhaifu katika kupambana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeweza kuendelea na Bunge mpaka saa hizi tunashukuru Mungu. Kuna rafiki yangu alinipigia simu akiwa mbali sana akasema Mheshimiwa Dkt. Kamala nakushauri sasa ukweli Bungeni hapo panaonekana pamechafuka ondoka mara moja. Nikamwambia rafiki yangu, kama sisi tukikimbia vita hii nani atapitisha bajeti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikasema hebu sasa tufanye hii kazi ya wananchi waliotutuma na Mwenyezi Mungu atasaidia na Mwenyezi Mungu kwa kweli ametusaidia tunaelekea kumaliza, lakini ninachokisema nilimwambia rafiki

yangu yule pia kwamba woga ni silaha dhaifu katika mapambano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Tunza Malapo atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Salim, hao wote wanachangia kutoka Msekwa, halafu Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema mpaka jioni ya leo nasimama kwenye Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu. Nina mambo machache, kwanza ni mjumbe wa LAAC hivyo moja kwa moja naunga mkono hoja ya kamati kwa asilimia 100, lakini nina mambo ambayo natamani niyaseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, suala la halmashauri zetu kushindwa kujaza fomu za bima inayopelekea halmashauri hizo kutorejeshewa fedha kutoka kwenye Mfuko wa Bima. Fomu tunayoijua fomu tangu Mfuko wa Bima uanzishwe mpaka leo hasara inapatikana ya bilioni mbili kwa sababu Halmashauri zimeshindwa kujaza fomu haiingii akillini. Maana yake aidha kuna uzembe wa makusudi au kuna hujuma za makusudi ambazo zinapelekea sasa hata wagonjwa anapoenda hospitalini wakiwa na vitambulisho vya bima wasihadumiwe ipasavyo kwa sababu zile fedha hazirudi. Hii sioni kama ni hoja kubwa, hivi kuna umuhimu gani mtu kujifunza kujaza fomu mpaka ipelekee ishindikane na halmashauri zipate hasara ya kufikia bilioni mbili na fedha nyininge huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake TAMISEMI iliangalie hili suala kwa undani waone ni nini kinachokwamisha, mbona kwenye Serikali za watu binafsi fomu zinajazwa vizuri? Kwa nini kwenye hospitali za Serikali fomu zinajazwa vibaya, tatizo ni nini? Kama watu wanahitaji

mafunzo, basi wapatiwe mafunzo ili waweze kujaza hizi fomu vizuri kuliko kuendelea kupata hasara ambazo hazileti huduma bora ya afya kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la makato ya mishahara kutowasilishwa katika taasisi mbalimbali. Tunapozungumzia taasisi maana yake kuna *TRA* maana mtu ukilipwa mshahara kuna *portion* inaenda *TRA*, kuna *portion* inaenda kwenye Mifuko ya Jamii na kuna *SACCOS* na vitu kama hivyo inategemea yule mtu anatakiwa akatwe hizo fedha ziende wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna fedha bilioni 1.5 za haya makato mbalimbali hazijawasilishwa na *CAG* kwenye ripoti yake anasema hili tatizo kila mwaka linaongezeka baada ya kupungua. Kwa hiyo, Serikali inachofanya inalipa mshahara wa mtu ule, *take home* anayotakiwa kulipwa lakini kwenye Mifuko ya Kijamii kule ili ile akiba aikute baadaye hiyo fedha haipelekwi. Sasa hii ni hatari, hatari yake ni ipi? mtu anapostaaifu sasa ili alipwe hizo fedha zake za kustaaifu akienda kule anaambiwa michango yako aidha ya mwaka, ya miezi sita, ya miezi mitatu haijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye hii ripoti tunayozungumza leo inayoishia Juni, 2019 unaona *TRA* hazikwenda milioni 228, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hazikwenda milioni 790 na kwenye taasisi nyingine hazikwenda milioni 434 inayofanya jumla ya kuwa bilioni 1.5. Na pia ukiangalia *trend* kutoka mwaka 2015/2016 hayo makato yalikuwa bilioni 1.1 hayakwenda, ilivyofika mwaka 2016/2017 wakapunguza kidogo ikawa milioni 963, ilipofika mwaka 2017/2018 haikwenda bilioni moja lakini leo mwaka 2018/2019 haikwenda bilioni 1.5. Maana yake ni nini? Maana yake Serikali inaendelea kufanya mambo ambayo siyo sawa na cha kusikitisha zaidi kama mnakumbuka juzi wakati ripoti ya *PAC* inawasilishwa hata hizo fedha zinazokwenda huko kwenye Mifuko bado Serikali inachota, bado inawafanya hawa wastaafu waendelee kuteseka, kuna nyingine haziendi lakini hizo zinazokwenda bado zinachotwa. Kwa hiyo, Serikali

iliangalie jambo hili kwa umuhimu wake na kuhakikisha kwamba haliendelei kutokea na walipe haya madeni ili kusudi wastaafu wetu wastaafu kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo lingine kuna malimbikizo mbalimbali ya mishahara na madai mengine ya shilingi bilioni 11 kwenye Halmashauri 29 ambazo *CAG* amezisema, lakini tuna Halmashauri 185. Sijajua akifanya ukaguzi wa kina kwenye Halmashauri zote 185 hali itakuwaje! Ikiwa katika Halmashauri 29 tu madai ni shilingi bilioni 11 ya watumishi, kwa hiyo, nafikiri Serikali hiyo hiyo inayojinasibu kwamba iko vizuri, basi iwalipe watumishi madai yao; na wao ni watu wanastahili waishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GAG* pia amefanya ukaguzi maalum kwenye Halmashauri za Wilaya saba; Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Kondoa, Chemba, Kongwa, Mpwapwa, Handeni na Halmashauri ya Mji, Masasi. Katika ukaguzi huo maalum imebainika ubadhirifu wa shilingi bilioni 6.197. Hizo Halmashauri saba zilizofanyiwa ukaguzi maalum, ukiangalia ubadhirifu mkubwa unatokea kwenye nini; unatokea kwenye miradi ya maji, miradi ya shule na kwenye Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwenye Miradi ya Maji Kongwa kuna mradi wa maji uko Kijiji cha Mkoka na Songambele; mradi mmoja tu una ubadhirifu wa shilingi milioni 348. Huko huko Kongwa ukiangalia kwenye ripoti, unakuta tena kuna ubadhirifu, mabomba yalinunuliwa yenyе viwango tofauti na vilivyomo kwenye *BOQ* hasara ya shilingi milioni 23. Kuna Shule ya Sekondari Kibaigwa, *TEA* ilitoa mabati 260 hayajulikani hayo mabati yako wapi na yamefanya kazi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lengo langu la kusema maneno haya ni nini? Hizi kaguzi maalum zinasaidia sana kuchambua, kutoa na kueleza nani amehusika moja kwa moja. Nashauri wale wote ambao wamehusika katika ubadhirifu huu wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sharia. Asionewe mtu lakini yule ambaye amehusika, basi ahakikishe

anawajibishwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za kiutumishi na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunatembelea kwenye Halmashauri nyingi, kuna tatizo kubwa la miradi ya maji na tatizo kubwa la miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Katika Halmashauri nyingi miradi hii haifanyi vizuri. Unaambiwa hapa labda imewekwa shilingi milioni 800, lakini kwa jicho la kawaida tu ukiangalia shilingi milioni 800 huioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafikiri TAMISEMI na wale wote wanaohusika; Wizara ya Kilimo, Maji na Umwagiliaji waone namna ya kuifuatilia miradi ya umwagiliaji; iliyo mingi haifanyi vizuri, thamani ya pesa huioni. Mtu hata ukiambiwa wakupeleke wanakwambia hata barabara tu haipitiki huwezi kufika huko, lakini ukiuliza hiyo sehemu unaambiwa umewekezwa shilingi milioni 800. Mkurugenzi anakwambia hamwezi kufika kwa sababu hata barabara hakuna. Unashindwa kuelewa hizo pesa ni kwamba zimeenda kutupwa au ni kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, CAGamesema mengi sana, ukisoma kwenye ripoti ya CAG utaona ameeleza mambo mbalimbali yanayohusu Halmashauri zetu na mwisho wa siku ametoa mapendekezo yake namna ya kuyaendea ili kukomesha. Sasa CAG namnukuu kwenye ukurasa wa 362 anasema, "liche ya kujirudia kwa hoja na mapendekezo katika ripoti zangu ni muhimu kutambua kuwa ingawa ofisi yangu, yaani Ofisi ya CAGinatetea utamaduni wa uwajibikaji lakini kisheria haina mamlaka ya kuwajibisha wakaguliwa kwa utendaji duni au matumizi yasiyordhisha ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi madaraka haya yamekabidhiwa kwa Serikali Kuu na Bunge. Maana yake ni nini? CAG anaishia kwenye kukagua, anatuambia pale pana tatizo moja, mbili, tatu; sisi Bunge kupitia Kamati za LAAC pamoja na PAC tunafanya uchambuzi. Tukishafanya uchambuzi tunaleta Bungeni kama tunavyoleta leo. Tukileta

Bungeni tunatoa mapendekezo yetu kwamba tunafikiri kwenye jambo fulani pafanyike moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni nini? Ni kwamba hivi ni nani anayehakikisha kwamba yale maazimio tunayoazimia yanatekelezwa? Tumeazimia maazimio mengi sana; kwenye kamati mbalimbali maazimio yako mengi. Ni nani anayeyahakikisha? Kwa sababu mtu wa TAMISEMI anaamua katika 10 atajibu matatu, mengine akasema naendelea kuyafanyia kazi. Kesho hoja zikija, zinajirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kama Bunge kuna haja sasa, aidha ya kuandaa Kamati Maalum kwa ajili ya kufuatilia haya mapendekezo yetu tunayoyatoa na ikishindikana basi Serikali nayo ione, iwe na kitengo cha kuhakikisha mapendekezo yanayotolewa na Bunge yanatendewa kazi. Huo ndiyo ushauri wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo mengi, nakushukuru. Pia niwahimize wananchi wa Mkoa wa Mtwara, hususan Jimbo la Mtwara Mjini, tunakuja na tuko tayari kabisa watuunge mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Haya jamani watu wanapelekewa salamu naona. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ahmed Salum attachangia pia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza na Mheshimiwa Juma Hamadi Omar ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa naunga mkono hoja. Pili, nilikuwa nataka kwanza nimshukuru sana na kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameonyesha na ametuongozwa kwenye tatizo kubwa hili la ugonjwa wa *Corona*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Corona* tumeishinda na Mungu atujalie. Moja katika sababu kubwa, hata nchi za nje wanamjadili sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, amewezaje kusimamia na kuishinda *Corona* kiurahisi namna ile. Sababu kubwa kabisa, alimtanguliza Mungu mbele, akatoa maombi, tukaomba, Mungu akatusikiliza na *Corona* tumeishinda na sasa hivi tunaendelea kuchapa kazi. Kwa hiyo, Mungu ampe afya, maisha marefu na miaka mitano ijayo atuongoze kama ambavyo anatuongoza sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwenye hoja yenye. *TEMESA* katika Halmashauri zote naamini kabisa ni tatizo kubwa sana katika kukarabati magari. Unaweza ukaiona ni kitu kilicho jificha sana, lakini *TEMESA* unapopeleka gari za Halmashauri, kuna magari mengi sana ya Halmashauri yamekaa tu hayatengenezwi kwa sababu ya gharama kubwa ya *TEMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipeleka gari *TEMESA* ni zaidi ya shilingi milioni 10 au 12. Gharama za kutengeneza gari mara 10 unanunua gari mpya. Sasa unaweza kukuta kama Halmashauri ya Shinyanga Mjini ina gari nyingi, lakini nyingi hazitengenezwi kwa sababu ya gharama kubwa mno ya *TEMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata juzi; nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa amesimamia suala zima la *TEMESA* hapa Dodoma. Suala la *TEMESA* lisimamiwe vizuri sana. Ushauri wangu, ama ifutwe kwa sababu ile iko kwa mujibu wa sheria na ukitengeneza gari nje ya *TEMESA* maana yake ni hoja sasa ya CAG, wanaanza kukuhoji kwa nini umetengeneza nje, sijui nini, kwa nini hukupeleka *TEMESA*, wakati *TEMESA* ni gharama kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna gari ya Kata ya Didia tulipeleka sisi katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, iligharimu shilingi milioni 12; Halmashauri ambayo haina uwezo, haiwezi. Kwa hiyo, unaweza kukuta magari yamekaa tu, wala hayafanyi kazi ya Halmashauri na kuleta tija kwenye

Halmashauri husika. Kwa hiyo, nashauri sana, Waziri Mkuu anisikilize na Waziri husika kwamba suala la *TEMESA* litazamwe mara mbili, ni tatizo kubwa sana kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee sasa Maafisa Ugani. Halmashauri zetu ambazo ziko vijiji tunategemea mapato makubwa sana kutokana na mazao yanayolimwa na wakulima. Wanaoweza kuwasaidia wakulima kupata mazao na kuuza na Halmashauri kuweza kupata mapato vizuri ni Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekaa, wameniomba kama inawezekana; na hii inawezekana ikawa ya nchi nzima, kwamba Maafisa Ugani hawa wakopeshwe pipipiki na wako tayari. Utoke mwongozo kutoka Serikali Kuu wadhaminiwe kwenye mabenki, wapate pipipiki ili waweze kuwafikia wakulima vizuri sana. Hii iende mpaka kwa Maafisa Mifugo, Maafisa wote wa ngazi za Kata. Wakiweza kutoa elimu vizuri, nina hakika kabisa tija itakuwepo, wakulima watalima vizuri, mapato yatakuwa mazuri na Halmashauri itaongeza mapato kutokana na Maafisa Ugani hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niongelee tena suala zima la vibali. Halmashauri yetu ina nafasi 21 za Madereva, natoa mfano tu, lakini sasa hivi tuna madereva 10 na mahitaji ni 11. Tumeomba vibali leo ni zaidi ya miaka miwili. Unaweza kukuta mahali kwa mfano, kila Idara inakuwa na ratiba ya kwenda kutembelea miradi yake, lakini kutokana na upungufu wa madereva, wanaanza kuazimana. Maana yake ni kwamba kazi zinachelewa, hazifanyiki vizuri, unamsubiri dereva yule kesho awepo ili idara hii iende.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Katibu Mkuu tusikilize Mheshimiwa Waziri tusikilize, tunapoomba vibali ambavyo mmetukasimu sisi kama Halmashauri, mtuletee haraka tuajiri madereva na hata nafasi nyiningine ili kazi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupa

fedha kwa ajili ya Hospitali yetu ya Wilaya, shilingi bilioni tatu. Hospitali ile tumeijenga vizuri sana na zimejengwa nchi nzima Hospitali nyingi sana za Wilaya, lakini mpaka sasa hivi bado hajakamilika kwa maana ya kuwa na sifa ya kuwa na Hospitali ya Wilaya. Tumeomba shilingi bilioni moja na nusu na hata Katibu Mkuu wa TAMISEMI alipokuja juzi ametuahidi na hata Waziri mwenyewe Mheshimiwa Jafo alipokuja mwaka 2019 alituahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba hizo fedha tukijenga yale majengo kwa maana ya jengo la utawala pamoja na majengo mengine ili iweze sasa kuwa na hadhi ya Hospitali ya Wilaya tuanze kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wetu. Tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulismamia hili, kwa kweli ni zuri sana. Hivyo hivyo kwenye Hospitali zetu za Kata, Vituo vya Afya; Tinde na Kata ya Samuye. Hili ni kwa nchi nzima. Nafikiri kila wilaya ukienda unakuta tatizo ni hilo hilo kwamba vifaa tiba vimechelewa kuja ili kazi iweze kufanyika wananchi wapate huduma. Tunasubiri vifaa tiba ili hospitali zetu ziweze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Makao Makuu ya Halmashauri Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba kuna baadhi ya Halmashauri kama 37 zihame ziente kwenye Makao Makuu ya Halmashauri zake; mojawapo ilikuwa ni sisi. Mawazo mazuri mno na kweli imeleta tija. Kwa sababu Halmashauri ilivyokaa kule, wamekuwa karibu sana na wananchi, muda wote wako na wananchi kwa sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, limejitokeza tatizo tu kuwa na Makao Makuu ya Halmashauri zetu. Wakuu wa Idara wanakaa hivi, ofisi tunatumia nyngine. Pamoja na kuwa kazi inakwenda vizuri sana chini ya Mkurugenzi wetu dada yangu Mhoja, anafanya kazi nzuri sana. Sasa tumeomba fedha kupitia maombi maalum ya shilingi bilioni moja na nusu, tunaomba sana na nina imani Halmashauri hizo zote zimeomba ikiwemo sisi, tukipewa fedha hizo zitatusaidia sana kujenga majengo hayo, kujenga majengo hayo,

kusimamia kazi na Wakuu wa Idara wafanye kazi kwa raha zote bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niishie hapo tu, yangu ni hayo, yako mengi ya kuongea lakini niwaachie na wenzangu. Naendelea tu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, aendelee, Mungu ampe afya njema, ampe nguvu za kazi, siyo ile nguvu nyingine, ile anayo haina wasiwasi; nasema nguvu ya kufanya kazi Taifa letu liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. Nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu, maelezo aliyotoa Mheshimiwa Spika kwa kirefu kabisa jana; tutazame yale ambayo Kamati imetuongoza ili tuweze kutoa sasa maazimio, kama Bunge tunaazimia nini kwenye taarifa ambayo Kamati imetuletea? Bila hivyo, tutahisi kwamba kuna majibu yatatoka mahali, lakini Mwenyekiti wetu wa Kamati ambaye ni Mbunge ndio atakayekuwa anajibu hizi hoja tunazozileta na siyo Serikali.

Hoja hii ni ya Kamati na taarifa ilioletwa hapa ni ya Kamati na kwa hiyo, hii taarifa ni ya Bunge. Kwa hiyo, atakayekuwa anajibu hoja ni Mwenyekiti ambaye ni Mbunge. Kwa hiyo, tujielekeze kwenye taarifa yetu ya Kamati, nasi tunataka kuiambia nini Serikali. Mheshimiwa Spika, alitoa maelezo kwa kirefu sana, sina haja ya kwenda huko.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Alex Gashaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Amina Mollel, ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Taarifa ya Kamati ya *LAAC*, taarifa ya mwaka unaoishia Juni 30, 2019. Kabla sijaanza kuchangia,

nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijalia afya na uzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwepo ndani ya Bunge hili huu ni mwaka wa tano sasa, namshukuru Mungu kwa sababu kwa miaka yote hiyo nimekuwa na afya njema, sijawahi kuugua na nimekuwa nikihudhuria Vikao vya Bunge na kutekeleza majukumu yangu kwa kadri ambavyo Mheshimiwa Spika amekuwa akinielekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Spika na Ofisi yake kwa maana ya Naibu Spika, Katibu, Wabunge na Watendaji wote kwa jinsi ambavyo kwa kweli wamekuwa wakitupa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yetu kama Kamati hii ya *LAAC*. Kwa hiyo, kwa kipindi cha miaka mitano yote nimekuwa ni Mjumbe wa Kamati hii ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo imefanyika, lakini kwa ushirikiano pia ambao kwa kweli wametupa katika kutekeleza majukumu yetu kama Kamati. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu na ndio maana mara kwa mara pale ambapo Kamati hii imekuwa ikitoa ushauri Serikali wamekuwa wakizingatia na kutekeleza. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama, yawezekana pengine nisipate nafasi ya kuchangia tena; nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Ngara kwa jinsi ambavyo wamenipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa kipindi cha miaka mitano. Ninaamini nimewawakilisha vilivyo katika kipindi hiki kwa ajili ya kuleta hoja zao na kutekeleza majukumu yangu Jimboni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliotangulia kuchangia wamesema mambo mengi katika hotuba hii ya Taarifa ya Kamati. Nijikite kwenye eneo ambalo limeonekana katika Halmashauri zilizo nyingi ni changamoto hasa kwenye upande

wa kuzingatia Sheria za Fedha na Sheria za Manunuzi. Halmashauri nyingi tumekuta kwamba zipo changamoto hizo. Unapokiuka Sheria za Fedha ukakiuka Sheria za Manunuzi kwa kuzingatia kwamba asilimia takribani 40 ya bajeti inaenda kwenye matumizi hasa kwa kutekeleza miradi ya maendeleo, unaweza ukajikuta kwamba kwa sehemu kubwa tunapoteza fedha kwa ajili ya kukosea taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili nataka kuishauri Serikali kwamba katika kuzingatia matumizi ya Sheria hii ya Manunuzi, lazima tuangalie ipo miradi mikubwa ambayo inatekelezwa kwa fedha za mikopo kwa asilimia mia moja, lakini tumeona kwamba masharti wakati mwingine yanakuwa ni magumu kwa upande wa Serikali tunayopewa katika kutekeleza miradi hii. Kumbe tungetumia taratibu nyeingine za manunuzi, hasa zile ambazo tumeona zinatupa tija kama manunuzi kwa kutumia *force account* ambapo tumeona imleta tija na kutekeleza miradi mingi kwa gharama nafuu, tumejikuta kwa baadhi ya miradi ambayo ni miradi mikubwa, pamoja na kwamba tunakuwa tinatekeleza miradi hiyo kwa mkopo, tunawekewa na masharti ya kwamba lazima awepo *consultant*, lazima iwe ni *full contract*, inachukua muda mrefu mchakato na tunajikuta tunaweza tukafanya kitu kilekile kwa gharama kubwa wakati upande wa *force account* tumefanya kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili nikirejea kwa mfano kwenye mradi unaotekeliza katika Jimbo langu la Ngara. Mradi wa umeme ambao unatekelezwa na nchi tatu; Rwanda, Burundi na Tanzania. Ngara iko kwenye eneo la mradi; zipo programu ambazo zinatekeleza miradi kwenye *local area*. Kwa mfano Program ya *LADEP (Local Area Development Plan)*, unakuta ujenzi wa kituo cha afya kwa kutumia masharti yale ambayo tumewekewa inakwenda mpaka kwenye milioni 700, 800 wakati kwa kutumia *force account* tumejenga vituo viwili kwa milioni 400 kila kimoja, maana yake tungakuwa na vituo viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwa sababu tumepata bilioni 12 kwa ajili ya kutekeleza miradi hii kwenye Jimbo langu la Ngara kama *phase one*; tunategemea kupata tena *phase two* ambayo na yenye we itaenda kwenye bilioni takriban 12. Tuone ni namna gani ambavyo tunaweza tukarudi Mezani kufanya *negotiations* ili twende kwa utaratibu wa *force account* kwa sababu Tanzania ndiyo pekee ambayo inarudisha mkopo kwa asilimia 100. Rwanda wao wanarudisha mkopo kwa asilimia 50; Burundi ni *free*, ni *a hundred percent grant*. Sasa kwenye ile *tripartite agreement* unakuta ni *fairground* wakati sisi huku kuna namna ambavyo tunaumia. Na Serikali ingeweza ku-save fedha nyingi ambazo zingetekeleza miradi maeneo mengine; hata kaa ni ndani ya Wilaya ya Ngara, lakini ingesaidia kwamba pengine bajeti ya miaka miwili, mitatu, tungei-save kwa ajili ya fursa hii ambayo tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo urasimu katika kuitisha hati za malipo ya wakandarasi. Kama ambavyo mapendekezo ya Kamati yameeleza, kwamba tunaomba Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani ambavyo badala ya kuendelea na urasimu huu wa kutoka wilayani, mkoani, TAMISEMI, Wizara ya Fedha namna ambavyo tunaweza tukafupisha mchakato huu wa kupeleka hizi *certificates*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye mikataba utakuta kuna mahali inaeleza kwamba unapo-*raise certificate* ndani ya siku 28 inatakiwa malipo yawe yamefanyika lakini unakuta maeneo mengine ni tofauti; *certificate* inakuwa *raised* kwenye ngazi ya halmashauri lakini mpaka kuja kulipwa miezi sita inapita. Kwa hiyo hii inasababisha miradi isiweze kutekelezwa kwa wakati na wakati mwingine unaweza usiione ile *value for money*, hasa unapokuja kuangalia athari zinazojitokeza kutokana na *delays* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine ambapo nahitaji kuchangia ni katika kuboresha mapato ya halmashauri. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, kwamba miezi michache iliyopita

halmashauri ziligawiwa *POS* ambazo zimeboreshwa. *POS* zile inaonekana ni *POS* ambazo mifumo yake haiwezi kuchezewa. Hata hivyo kwenye halmashauri zilizo nyingi bado kuna zile *POS* za zamani ambazo zimeonekana kutoa mianaya ya uvujishaji wa mapato. Tuombe kwamba sasa kuwepo na muda maalum wa *ku-phase out* zile *POS* ambazo ni za zamani ili ziingie *POS* zingine zinazoweza kudhibitiwa katika mfumo ili kuwezesha sasa makusanyo ya halmashauri zetu yaweze kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kwa kipindi cha miaka hii mitano kwa kweli nimejifunza mengi. Na ndiyo maana unawenza ukaona, kama taarifa yetu inavyoeleza, kwamba Kamati hii imefanya mambo makubwa na maboresho makubwa na kufanya halmashauri zilizo nyingi sasa takriban asilimia 95 kupata hati inayoridhisha. Ni halmashauri chache tu ambazo kwa kweli bado zinasuasua, halmahsuri yangu ni mionganini mwa halmashauri ambazo kwa miaka mitano mfululizo imepata hati safi, na hii ni kutohana na uzoefu nilioupatana kutoa ushauri vizuri kwenye halmashauri yangu. Zipo halmashauri zinapzosuasua kama Halmashauri ya Ujiji Kigoma, miaka minne mfululizo hati isiyoridhisha. Halafu unakuta Mbunge humu ndani anasema ye ye ndio mshauri mkuu wa Serikali na kujinasibu, hiyo haikubaliki. Kwa hiyo ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Hayo ndiyo niliyokuwa nayo na ninaomba kuunga mkono hoja ya taarifa ya Kamati. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijalia nikiwa Mbunge kwa muda wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Wingwi ambalo lipo Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunichagua kuwa Mbunge na

kuniamini kwa miaka mitano. Naamini tumeshirikiana vizuri na *Inshallah* naamini kwamba watanipa tena ushirikiano ili tuendelee kushirikiana kwa miaka mitano inayokuja na tutaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niwashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya *LAAC*, wajumbe wenzangu ambao tumeshirikiana takribani kwa miaka miwili na nusu katika Kamati hii ya *LAAC* nikitokea Kamati ya Katiba na Sheria. Kama alivyosema Mheshimiwa *Eng. Chiza pale*, kwamba wakati nahamishwa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria napelekwa kwenye Kamati ya *LAAC* nilikuwa najiuliza huko nakwenda kufanya nini. Lakini nimejifunza vitu vingi na nimesoma mengi na nimeelewa mengi. Na leo tunakwenda kukamilisha ripoti yetu hii ya mwisho ndani ya miaka hii mitano nikiwa nimetoka vizuri na nimejifunza vitu vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ambacho napenda na mimi nikichangie kupitia taarifa hii ya Kamati ni suala la kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye halmashauri. Ni ukweli usiopingika kwamba suala hili linaleta taabu na ukakasi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba nitoe mfano; ukienda kwenye ukurasa wa kitabu cha *CAG* kwenye ukurasa wa 525 utaona baadhi ya halmashauri ambazo zilipelekewa fedha pungufu za maendeleo. Lakini pia ukipitia Ripoti hii ya *LAAC* ukienda kwenye ukurasa wa 19 kwenye kiambatanisho A, utaona jinsi gani halmashauri ambazo zilipewa fedha za ziada. Hili naomba nilitolee mfano ili tuweke kumbukumbu vizuri. Ukienda kwenye huo ukurasa wa 19 kwenye kitabu cha ripoti hii ya Kamati ya *LAAC* utaona kwa mfano Halmashauri ya Musoma iliomba fedha za maendeleo bilioni 1.4 lakini ilipewa fedha kiasi cha bilioni 3.9, ziada ya shilingi bilioni 2.4; ni zaidi ya asilimia 163.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nyingine ambayo naomba niitaje ni Halmashuri ya Lushoto ambayo

iliomba kiasi cha shilingi bilioni 1.8 ikapewa shilingi bilioni 3.1, zaidi ya shilingi bilioni 1.36. Na zipo halmashauri nyingine; Halmashauri ya Longido kwa mfano, iliomba jumla ya shilingi bilioni 3.4 ikapewa bilioni 4.5, ziada ya shilingi bilioni 1.06.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua halmashauri ambazo zilipata fedha pungufu, kwa mfano, Halmashauri ya Babati iliomba shilingi bilioni 251 ikapewa shilingi bilioni 103, pungufu ya shilingi bilioni 148. Halmashauri nyingine ni Halmashauri ya Kiteto ambayo iliomba shilingi bilioni 637 na ilipewa shilingi bilioni 389, pungufu ya shilingi bilioni 247. Ni halmashauri nyingi, zipo halmashauri ambazo zilipewa ziada zaidi ya 26 lakini zipo halmashauri ambazo zilipewa pungufu zaidi ya 15. Hapa nasikitika tunachangia hotuba hii Wizara ya Fedha hakuna Waziri wala hakuna Naibu Waziri na hili ni jukumu la Wizara ya Fedha ambayo ndiyo inayopeleka fedha kwenye halmashauri, TAMISEMI ni wasimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili ni jambo ambalo linaleta ukakasi mkubwa maana sisi ambao tulikuwa kwenye Kamati ndio tumeona maswali ambayo tunauliza tunajibowi, masikitiko ya baadhi ya watendaji, wakurugenzi wa halmashauri wanavyosikiti na kulalamika jinsi fedha ambavyo haziendi wakati kuna halmashauri nyingine zinapewa ziada kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama kuna halmashauri inapewa ziada ya asilimia 163 wakati huu kuna halmashauri nyingine inapewa fedha za maendeleo kwa asilimia 30. Huu tunaweza tukasema si sahihi na hili jambo kimsingi haliwezi kuleta afya wala halileti afya katika maendeleo ya Tanzania kwa sababu Watanzania wote ni wamoja na nchi hii ni moja na kama ni kodi tunalipa wote. Kwa hiyo kama ni hako kasungura kadogo ambapo yupo basi ni vizuri kwamba tumgawe sawasawa kila halmashauri ipate kile ambacho kwamba kinastahiki badala ya kuona kwamba halmashauri fulani ni bora kuliko halmashauri nyingine. Hii haitawenza kuleta afya kwa maendeleo ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba nilizungumze ni suala la madeni kwa watumishi. Ukienda kwenye kitabu cha CAG Ripoti hii ya LAAC, ripoti kuu, utakuta kwamba ukurasa wa 59 kumezungumzwa kwamba kuna watumishi wengi kwenye halmashauri zetu ambaao wanadai na wanadai fedha nyingi zikiwemo za mishahara kwa maana ya malimbikizo ya mishahara, fedha za likizo, pamoja na posho ambazo wanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano watumishi hawakupata *promotion* hasa katika nyongeza ya mshahara. Kwa hiyo wame-suffersana na ni kipindi ambacho tunaweza tukasema watumishi walikuwa kwenye maumivu makubwa. Sasa inapofika mahali kwamba ripoti ya CAG inakuja kuonesha hata zile stahiki zao za msingi kama likizo, mishahara na masuala ya posho pia wamelimbikiziwa madeni, hawalipwi, haya ni maumivu kwa watumishi na ni maumivu makubwa ambayo kimsingi hayaimarishi utendaji wetu bali yanadroofisha. Kwa hiyo ni vyema kabisa Serikali wakaliangalia hili kwa jicho la huruma, wakaliangalia kwa jicho la mbali kuona kwamba watumishi hawa ni watumishi wa umma na ni sehemu ya ujenzi wa maendeleo ya nchi yetu na wanapaswa kuangaliwa vizuri na kuenziwa kwa sababu hawa ndio wanaoendesha taifa. Lakini pia hawa tukumbuke kwamba ndio wakusanyaji wa kodi kuititia mishahara yao. Sasa unapofika mahali unawaumiza katika misingi kama hiyo ya likizo na mambo mengine ni kuwaumiza watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika halmashauri zetu kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi. Na upungufu huu wa watumishi tumekumbana nao katika halmashauri zote ambazo tumezikagua. Si chini ya asilimia 30 ya watumishi kila halmashauri unakuta suala hilo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena unakuta watumishi ambaao ni muhimu katika uendeshaji na usimamizi wa fedha kwenye halmashauri; kwa mfano ukifika kwenye mfumo wa TEHAMA, ukifika kwenye kitabu cha CAG ukurasa wa 39

ameeleza kwa upana na urefu sana suala hili. Ukitu cha CAG kikubwa kile cha ripoti ya jumla amelieleza kwa upana jinsi gani kwenye halmashauri suala la TEHAMA ni changamoto; na wakati mwingine linasababisha hata upotevu wa mapato kwa sababu hata suala la mifumo ya ukusanyaji wa mapato pia linahitaji wataalam hawa wa TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unakwenda halmashauri inahitaji pengine wataalam wa TEHAMA labda watano lakini kuna mmoja na huyo mmoja hana vifaa vyatutende kazi. Sasa utashangaa huyu anafanya kazi kiutamaduni tu kwamba yupo ukifika yupo basi lakini vifaa vyatutende kazi hana; hana gari, hana *laptop*, hana mashine yoyote hata ya ofisi yake pengine kapangishwa kwenye chumba cha Afisa Elimu ndiyo ofisi yake. Kwa hiyo unakuta katika mfumo kama huu hatuwezi kupata ufanisi kwenye suala la ukusanyaji wa mapato kama hatujaboresha watumishi na hatujaajiri watumishi katika vitengo muhimu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Kitengo cha TEHAMA tu, katika mambo ambayo yameathiri sana au yanaathiri sana mfumo wa ukusanyaji wa mapato na mfumo wa matumizi; maana kuna mfumo wa ukusanyaji halafu tunakwenda kutumia hiyo fedha baada ya kuikusanya; ni Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika halmashauri na hili TAMISEMI walichukue vizuri, tumejaribu kuwashauri kwenye Kamati na hapa kupitia Bunge leo tunawashauri, kwamba kama kuna sehemu muhimu ambayo inaweza ikawasaki hata Ofisi ya CAG wakati wa ukaguzi ni halmashauri kuwa na watendaji katika Kitengo hiki cha Wakaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Wakaguzi wa Ndani katika halmashauri wanatakiwa wawe wanne au watano lakini takribani halmashauri zote tulizozikagua kuna mtu mmoja. Bahati mbaya sana zaidi ni kwamba huyo mtu mmoja hana vifaa vyatutende kazi, anategemea msaada wa mkurugenzi. Sasa msaada wa mkurugenzi, mtu ambaye

anatakiwa afanye kazi zake za ukaguzi akiwa huru anategemea msaada wa mkurugenzi; unachotegema ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachozalishwa hapa ni kwamba hakuna ufanisi wa ukaguzi kwa sababu hatimaye huyu Mkaguzi wa Ndani akimkwaza mkurugenzi ambaye ndio afisa masuuli hapa ufanisi utakosekana, hiyo biashara itakuwa haiwezi kwenda. Kwa sababu huyu mtu mkaguzi wa ndani kama anamtegemea mkurugenzi ampe mafuta, anategemea pengine *camera* au gari ya ofisi, pengine ofisi yenye we nayo kapangishwa chumba cha afisa maendeleo, kidogo hapo ufanisi hauwezi kupatikana. Kwa hiyo tuiombe Serikali hili suala iliangalie kwa jicho la huruma, vijana wa kitanzania waliosoma wapo wengi, leo ukitangaza *interview* ya ajira hapa tunaona. Kama umetangaza ajira 15 wanakuja watu 5,000, kwa hiyo vijana wa kuajiriwa wapo. Kwa hiyo Serikali kidogo ifungue mikono katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo napenda kulisema ni kusema kwamba mfumo wetu wa Serikali, mfumo wa vyombo hivi pengine kama Ofisi ya CAG hata hii Kamati yetu ya *LAAC* tunakuta kwamba kuna mapungufu mengi na kuna udhaifu mkubwa ambao mimi binafsi na Kamati tumeubaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tunakuta Kamati inakwenda kukagua sehemu na kuna mapungufu mengi ya wazi lakini Kamati haina uwezo wa kufanya lolote zaidi ya ushauri na kutoa maagizo, maagizo ambayo sasa ufuatiliaji wake, kwa sababu ufuatiliaji wake unaweza kuchukua pengine, Kamati imetoa maagizo leo 2020 kwenye halmashauri fulani, lakini halmashuari hiyo ambayo imepewa maagizo leo inaweza kuchukua miaka 10 haijaja tena kwenye Kamati. Kwa hiyo unakuta maagizo haya kama vile yananning'inia. Halmashauri huko imekaa imejisahau hawatekelezi maagizo mpaka waje washtukizwe sasa kwamba mwezi unaokuja mtakuja tena kwenye Kamati baada ya miaka kumi ndipo vitabu vinafunguliwa watu wanakwenda kutekeleza maagizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Bunge, majukumu ya Kamati kuitia maagizo haya kidogo hapo unakuwa na walakini na ndiyo maana Wajumbe wenzangu wengi wameshauri kwamba sasa kuna haja, wamesemwa kuundwa chombo mimi naafiki kwamba labda kuundwe Kamati nyingine ya kufuatilia maagizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nishauri kitu kingine Serikali wakiangalie kwamba maagizo haya yawe yanafuatiliwa na Sekretarieti ya Bunge kwa maana ya Serkt ya Kamati. Kwa maana ya kwamba sasa Kamati iwe inaandaa *document* maalum ambazo zitaonesha kwamba haya ndiyo maagizo ya Kamati Sekretarieti ya Bunge ikae ifuatilie. Kila baada ya Bunge likirudi sasa iwe angalau siku mbili au tatu sasa Kamati ya *LAAC* kama vile Kamati ya *PAC*, ni sambamba; ziwe zinapata muda wa kufuatilia utekelezaji wa maagizo badala ya kusubiri kwamba pengine baada ya miaka mitano, sita au kumi ndiyo halmashauri inakuja tena kwenye Kamati halafu maagizo hapo yanakuja Mezani. Hili haliwezi kuleta ufanisi, bali kuwe na utaratibu maalum ambaao maagizo haya yanafuatiliwa kwa kina kwa sababu maagizo haya wakati mwingine yanakuwa na athari kubwa kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo haya pia wakati mwingine yanakuwa na watu ambaao wanapaswa kuchukuliwa hatua, lakini mtu huyo yupo maagizo yale hayafuatiliwi. Miaka 10 yupo kazini kumbe huku ameshachukua fedha za umma, siku nyingine ameshastaafu, ameshakufa, hakuna chochote ambacho kinaenda. Kwa hiyo, hili naomba Serikali wangeliangalia kwa kina na kulifanyia kazi. Hii inaweza kabisa ikasaidia sasa Kamati ya *LAAC at least* kidogo ikaonekana kwamba, iko *active* na inafuatilia baada ya kutoa maagizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nikupongeze kwa yote ambayo yamepita, lakini pia tukielekea kumaliza Bunge basi kwa yale ambayo tulikwaruzana hapa na pale, tusameheane na tuwiane radhi

kwa safari hii ambayo tunaenda huko mbele. Tuombeane dua, *insha Allah* 2020 mwezi wa 11 tukutane tena hapa..

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Kamati na nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Amina Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu. Nianze kwanza kwa kuwapongeza Wajumbe wa Kamati pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuyaonesha yale yote ambayo Bunge litaazimia hapo baadaye, ili basi yaweweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze *CAG* kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na ni kwa kipindi kifupi. Kwa kweli, amefanya kazi kubwa nampongeza kwa moyo wa dhati kabisa kwa sababu, yote haya ndio ambayo yanakwenda kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kutokana na uongozi mzuri wa jemedari Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ndio maana *CAG* pia amegundua kwamba, baadhi ya ubadhirifu uliokuwa ukifanywa katika Halmashauri zetu, lakini pia huduma mbalimbali za kijamii zimeboreshwa hivi sasa. Hii ni kutokana na kazi nzuri ya Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Nampongeza sana Rais wetu na Mwenyezi Mungu amjalie kila lenye heri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo zimependekezwa na Kamati hii. Mimi nitachangia katika hoja mbili; hoja ya kwanza ni kuhusu urasimu katika kuitisha hati za malipo ya wakandarasi. Urasimu huu umechangia kwa baadhi ya wakandarasi wengi wao ambao kwa kweli kwa namna moja au nyingine ambao walikuwa wamekopa hata pesa katika mabenki kwa hivi

sasa kwa kweli, wamefilisiwa kutokana na urasimu huu kwa sababu, miradi ile ambayo pia walipaswa waweze kujamiliha haikuweza kukamiliha kwa wakati unaopaswa. Kutokana na mapendekezo ya Kamati basi nami nashauri kwamba, urasimu huu uondolewe, ili basi wakandarasi hawa waweze kulipwa malipo yao, lakini pia miradi ile ambayo ilikuwa inapaswa kukamiliha iweze kukamiliha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Serikali Kuu kutowasilisha ipasavyo ruzuku ya fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu. Tunafahamu kwamba, Halmashauri hizi pesa tayari kutokana na sheria ambayo tuliiptisha hapa makusanyo yote yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa maana hiyo tunatarajia Serikali iweze kutoa pesa kwa muda na wakati uliopangwa, lakini matokeo yake tumeona kwamba, kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikichelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndio ambayo tunaona kwamba, hivi sasa katika baadhi ya Halmashauri Madiwani wengi wameshindwa kulipwa kwa wakati, lakini pia, tunapokwenda mabaraza mengi yatavunjwa mwezi ujao na wengi bado pia, wana mikopo katika mabenki. Kwa mfano mabaraza yanavunjwa mwezi ujao, mikopo katika mabenki yao inakwenda mpaka mwezi Agosti. Tunajiuliza kwamba, hawa Madiwani mikopo hiyo watawezaje kuirejesha kwa sababu, dhamana yao ilikuwa ni Baraza la Madiwani na Halmashauri husika. Kwa hiyo, kutokana na hili endapo kama fedha zingekuwa zinapelekwa kwa muda na wakati unaotakiwa ni dhahiri kabisa kusingekuwepo na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sababu, pesa zote zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali katika Halmashauri ya Arusha *DC* waliuza eneo la Lakilaki kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Eneo hilo ndipo ambapo imejengwa Mahakama ya *ICTR* ambayo ni Mahakama ya Kimbari, mpaka leo hii Halmashauri hii bado haijapewa, inadai zaidi ya shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kutokana na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati hii kuona umuhimu wa kuweza kukamilisha madeni yote ambayo yanapaswa na ili Halmashauri hizi ziweze kuwalipa Madiwani. Pia miradi mingine ya maendeleo ili iweze kukamilika, ni dhahiri kabisa kwamba, fedha hizi zinahitajika na bila hivyo bado kutakuwa na tatizo kubwa kwa sababu, Madiwani hawa watakapoondoka, lakini miradi mingine ambayo ilipaswa ikamilike kwa wakati itashindwa kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uongozi mzuri tumeona kabisa kwamba, *Force Account* imeweza kufanya kazi kubwa katika Halmashauri zetu kutokana na vituo vilivyojengwa kwa shilingi milioni 400 mpaka milioni 500. Kwa hiyo, wakati mwingine endapo basi, mbali ya kuwatumia hawa wakandarasi kama miradi mingine Serikali ikizishirikisha ipasavyo Halmashauri zetu, ni dhahiri kabisa kwamba, hizi *Force Account* zitawenza kuokoa fedha nyngi ambazo zingepotea kwa namna moja au nyngine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kucheleweshwa huku kwa fedha katika Halmashauri zetu kwa namna moja au nyngine, naona kwamba, hata ile 2% kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa sababu, makusanyo ya ndani ni machache inashindwa kukamilika hasa kwa watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, mapendekezo ya Kamati yaliyopendekezwa ni muhimu sana yakazingatiwa ili basi Halmashauri zetu ziweze kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia baadhi ya Halmashauri kama walivyozungumza Wabunge wengine, ni aibu kwa kweli kama kuna watumishi ambao hawajui kutumia hizo mashine. Niiombe Serikali ilishughulikie suala hili ili basi kama kweli hawana ujuzi wa kuweza kutumia hizo mashine, wapo vijana wengi ambao wanamaliza vyuo vikuu na wangeweza kupelekwa huko wakaokoe mabilioni ya fedha yanayopotea, lakini kwa hawa ambao wapo je, Serikali haionti kwamba, kuna umuhimu wa kuwaandalia utaratibu mzuri wakapata mafunzo na waweze kuzitumia vizuri ili fedha za Serikali zisiweze kupotea?

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo, inaunga mkono hoja na naomba mapendekezo haya, kama walivyosema wengine, tusichukue muda mrefu yaweze kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuokoa kwa namna moja au nyingine fedha za Serikali ambazo kwa kweli zinahitajika sana ziende huko kwenye jamii kuweza kukamilisha miradi mbalimbali ambayo haijakamilika, lakini kulipwa kwa madeni mbalimbali ambayo hayajakamilika. Serikali ikifanya hivyo tutakwenda mbele kuelekea uchumi wa kati mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante na Mungu akubariki sana wewe katika safari yako unapokwenda kule Mbeya Mjini, kila la heri. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingu wa rehema, ametusaidia mpaka tunafika mwisho sasa, wengine sasa ni mwaka wa 10 tumekuwa hapa Bungeni, nichukue fursa hii kumshukuru sana yeche.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nishukuru chama changu na kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini kuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na Maliasili. Vilevile nichukue fursa hii kuushukuru uongozi wa Bunge, mwenzangu hapa amezungumza, kukaa pamoja kwa miaka mitano watu mia tatu tisini na kitu sio jambo dogo. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine tumefanya kazi kwa pamoja kwa kupishana kwa kukwaruzana, lakini yote kwa yote ni lengo la kuijenga Tanzania, *nothing is personal*. Naamini tutaondoka hapa tukiwa tumesameheana mwisho wa siku kila mtu ana mraba wake ambao anaamini anatakiwa aufanye bila fitina wala kufanyiana majungu yasikuwa na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi nichukue nafasi hii kuwapongeza wapigakura wangu wa Jimbo la Iringa Mjini, *it was a privilege* kuwatumikia, kuwa-serve. Wameniamini na wamekuwa wakinisikiliza na wamekuwa wakiniunga mkono kwa kiwango kikubwa sana, niwashukuru sana. Vilevile nisisahau kuwashukuru watendaji wa Manispaa ya Iringa Mjini kuanzia Mkurugenzi, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa umma ambao wamefanya kazi kwa uaminifu mkubwa sana, sote kwa pamoja tulikuwa tunajenga nyumba moja. Niwashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, tunaamini kwamba, tunaenda kwenye uchaguzi, Mungu ndio anaamua nani atarudi tena hapa, tuzidi kucombeana yaliyo mema mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema naunga mkono Kamati ya *LAAC* kwa mapendekezo yake, lakini nina ushauri kidogo kwa sababu, tumezungumza mambo mengi sana mpaka miaka mitano hii imeisha, kama wengine hawajaelewa *may be it was not merit for them*. Ukiangalia mwaka 1998 kulikuwa na *reform* ya *Local Government* na kabla ya hapo Mwalimu Nyerere alikuwa amezivunja *Local Government* akazirudisha tena, akavunja tena, baadaye kukafanyika *reform* kubwa ya *Local Government* ambayo ni *D by D*. Tuliamua kuwahuisha wahusika wa maeneo yale, lakini na *ku-decentralise* kwamba, mamlaka iwe kwenye *Local Government* namna ya kukusanya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zilitumika pesa nyingi sana kufanya *reform* ya *Local Government*, lakini kwa bahati mbaya sana ukiangalia Awamu ya Tano baada ya kuingia madarakani ni kama vile tumefuta tena *Local Government* kijanja pamoja na kwamba, *policy ipo*. Kwa hiyo, nashauri kwamba, pamoja na kazi nzuri ambayo *LAAC* wamefanya nadhani tulitakiwa tuingie kwa undani zaidi kuangalia ni kwa namna gani ile *reform* tulivoifanya tunaifanya kazi kwa sababu, watu wengi hapa wanalamika jinsi ambavyo pesa hazirudi na mimi pamoja na kwamba, Halmashauri yangu ni moja ya Halmashauri bora kabisa hapa nchini, inafanya kazi vizuri, lakini nikiangalia tulivyokuwa tunakusanya pesa za ndani wenyewe, tulikuwa tunafanya kazi vizuri zaidi,

tulikuwa tumeponga mikakati mingi ya kufunika lami maeneo mengi, lakini baada ya kwamba hii hela sasa inaenda *Central Government*, hela nyingi hazirudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya *LAA*Cwatakuwa mashahidi, Halmashauri yangu inafanya kazi vizuri sana ni mionganoni mwa Halmashauri bora hapa nchini. Kwa hiyo, nadhani bado *LAA*C walitakiwa waibane Serikali, hivi zile *reforms* ambazo tulizifanya tumeishia wapi kwa sababu sasa hivi ni kama tume-centralise tena? Kwa hiyo, ile nguvu, madaraka walikuwa nayo watu kwenye *local government* inaonekana haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri, sisi Wabunge pamoja na Madiwani, sisi ni *taxpayer representatives*, kazi yetu kubwa, pamoja na kutunga sheria na kuishauri Serikali, lakini kazi yetu kubwa ni *taxpayer representative*, tuna *represent* kodi za wananchi zitumike vizuri. Ndio maana kule Marekani siku za zamani walisema *no taxation without representation* kwamba, hamuwezi mkachukua kodi zetu kama hatuna wawakilishi na sisi hapa ndio wawakilishi, Madiwani ndio wawakilishi kuhakikisha pesa zinazokusanywa na Serikali zile kodi zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninavyozungumza nguvu ya *Local Government* imechukuliwa sana. Unakuta Wakuu wa Wilaya wana nguvu sana kwenye *Local Government*, wanaingilia utendaji kazi, ile mamlaka kwenye *Local Government* haipo, Wakuu wa Mikoa wanaingilia, maamuzi mengine ambayo yanafanywa kwenye *Local Government* yanatenguliwa na Wakuu wa Mikoa kwa kutumia madaraka yao, wakati mwininge hata wanakiuka sheria kwa hiyo, hii yote ina-*contradict.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye *Local Government*saa hizi hata ile *human resources* haipo. Pamoja na kwamba, tutajenga barabara, tutajenga shule, tutajenga hospitali, lakini Taifa halijengwi kwa matofali, Taifa halijengwi kwa lami, Taifa halijengwi kwa vyuma, Taifa linajengwa kwa kuwa na *brain* iliyo nzuri, *sound mind*. Wachina wana methali

moja wanasema kama una mpango wa mwaka mmoja panda mpunga kwa sababu ndani ya mwaka mmoja unaweza ukapanda mpunga na kuvuna na wanasema kama una mipango ya miaka 20 panda miti, ndani ya miaka 20 unaweza ukapanda miti na kuvuna, ila wanasema kama una mpango wa karne moja endeleva watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndio la msingi kuendeleza watu Taifa linajengwa kwa kuendeleza watu. Kwa kujenga watu wawe na *sound mind*, wawe na uwezo wa kufikiri, wawe na uwezo wa kuhoji, wawe na uwezo wa kudadisi. Tumeua hata *capacity building* kwenye Halmashauri zetu; tunalalamika hapa watendaji hawako wa kutosha, kama watu hatuwezi kuwa-*empower* watawezaje kuleta hayo maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana hata haya majengo tunayozungumza kwamba, tutayajenga haya majengo, majengo mengi waliyojenga Wajerumani bado leo yana nguvu kuliko haya majengo tunayojenga leo, majengo waliyojenga Waingereza yana nguvu kuliko leo. Leo wanazungumza kwamba, tutumie *Force Account, it is fine*, lakini majengo hayo yakikaa miaka mitano, miaka 10, unakuta hayafai kwa sababu, tunafanya vitu kienyeji, lakini tuki-*empower* kwenye *mind* watu watakuwa wana-*focus* mbele. Wajibu wetu kulijenga Taifa hili ni kuendeleza watu na kuwaendeleza watu ni kuwa-*empower*. Hii *building capacity* haipo watu wanasukumwa. Tunawezaje kujenga Taifa ambalo watu katika kipindi cha miaka mitano hawajaongezewa nyongeza za mishahara? Hakuna vitendea kazi vya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tutasifiana bure hapa, lakini tukienda kwenye Halmashauri zetu uhalsia tunauona, watu hawana uwezo wa kutosha. Nasema hivi, mimi Halmashauri yangu ni moja ya Halmashauri bora, lakini wengine Halmashauri zenu ziko kiwango cha chini sana, hii *building capacity* haipo, kwa hiyo, tutapongezana hapa, tutasifiana hapa na kibaya zaidi kinachonisikitisha ni pale ambapo Serikali haiko *consistency*. Tume-*focus* zaidi kwenye uchaguzi

badala ya ku-focus zaidi ku-deal na *generation* kwa sababu, angalia Awamu ya Nne imeondoka, tulikuja na maisha bora kwa kila Mtanzania, ari mpya nguvu mpya, tukaja na *big result now*, tukaingia kwenye masuala ya gesi, tukaja na kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulivyomaliza vyote hivi imekuja awamu nyiningine hii sasa kama vile havikufanyika kwa sababu, Serikali hii haijaanza leo hivi vitu tulitakiwa tuendeleze, tuwe tuna, waliofanya nyuma kuna mazuri yale tuendeleze, tuende na atakayekuja mwingine afanye mazuri. Sasa kila siku tunaanza na kitu kipyta kwa sababu, tunawaza uchaguzi kwamba, tuchomoke na hoja ipi ambayo itakuwa *viral* kwa wananchi, lakini nadhani hatuwatendei haki wananchi, kwa sababu, sisi *we are the elite of the nation*. Tunatakiwa hapa tuisimamie Serikali, tuishauri, lakini kikubwa cha kwanza ni kusimamia kodi ya wananchi. Tukijuliza maswali sisi sote ni kweli tunaísimamia hiyo kodi ya wananchi?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ushauri mzuri anaoutoa Mheshimiwa Msigwa, lakini vilevile akumbuke kwamba, pamoja na ushauri huo anaoutoa amekiri juzi kwa kumwomba Mheshimiwa Abrahaman Kinana radhi kwamba, alisema uwongo katika Bunge hili. Kwa hiyo, kama yeye mwenyewe pia angekuwa mkweli kwa kusema ukweli, tungefika mbali sana badala yake amekiri dhahiri kwamba, yeye alisema uwongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Mungu amrehemu, naona hajui analolitenda. Mambo mengine ni *personal/hata* hayakuhusu

kabisa, hebu fanya mambo mengine. Mungu amrehemu tu.  
(*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unajua hiyo lugha ya kurehemu maana yake nini?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko hai mimi na ananiona niko hapa hai, afute hiyo kauli.  
(*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel ngoja niiweke vizuri.

Mheshimiwa Msigwa hii habari ya mtu kurehemu nadhani iko mahali ambapo sio pake; ye ye amezungumza jambo ambalo wewe unaweza kumjibu, lakini usiingie huko kwenye...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *no*, nazungumza hivyo kwa sababu, labda tunatofautiana tafsiri ya rehema.

**NAIBU SPIKA:** Alichokisema sio dhambi, kinachorehemu ni dhambi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *it depend* unatafsiri vipi. *I am a theologian* najua maana ya rehema ni nini.

**NAIBU SPIKA:** Tafsiri ya dhambi tunaifahamu Mheshimiwa; Mheshimiwa Msigwa tafadhalii, tuelewane vizuri.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa usinilazimishe nikubali unayoyataka tu. Hiyo ni *definition* tofaati.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge mpaka tunafika mwisho wa Bunge hatujui Kanuni za Bunge?

Mimi nasikitika sana, yaani unataka ukae humu ndani tunabishana? Yaani kwamba, tuko kwenye mukutano mimi nazungumza na wewe unataka kuzungumza ni kanuni gani mnazosoma Waheshimiwa Wabunge?

Kiti lazima kiheshimiwe, Kiti lazima kiheshimiwe, nasikitika tunafika mwisho mpaka leo hatufahamu. (*Makofi*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joseph Kakunda atakayechangia kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia maoni yangu kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* ambayo ni miongoni mwa Kamati muhimu kabisa katika Bunge letu. Shukrani za dhati ziwaendee wanachama wa Chama cha Mapinduzi na wananchi kwa ujumla katika Jimbo la Sikonge, katika Wilaya ya Sikonge kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa tangu nimekuwa Mbunge kwa kipindi hiki cha miaka mitano ambapo miradi mingi sana imeteklezwa katika kata karibu zote, katika vijiji vyote na maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru sana viongozi wa ngazi mbalimbali, tumekuwa na ushirikiano wenye upendo na mshikamano. Nawashukuru sana viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa, Wilaya, Kata, Matawi hadi Mashina kwa jinsi ambavyo walitoa uongozi wao vizuri na kutusimamia. Pia nawashukuru viongozi wa Serikali kuanzia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Madiwani, wote wakuu wa idara tuendeleze mshikamano na ushirikiano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe pongezi za dhati kwa viongozi wetu wakuu katika nchi hii chini ya uongozi wa jemedari Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi uliotukuka ambao wamekuwa wakituongoza na kwa kuwajali zaidi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika, uzalendo wa Rais hauheshimiki hapa nchini tu bali unaheshimiwa Kimataifa. Ukiangalia hata jinsi ambavyo amesimamia masuala yote yanayohusu kuwafungua macho Watanzania, kuwaonea huruma na kuwaongoza kukabiliana na janga hili la corona utaona kwamba misimamo yake ilikuwa sahihi muda wote na ndiyo maana hata viongozi wa hao yanayojiita Mataifa makubwa sasa wanaanza kumuiga. Waliwafungia watu wao ndani sasa wanaanza kuwatoa nje wakati corona bado ipo. Ahsante sana Rais Dkt. Magufuli na nasema kwamba asingekuwa Rais wetu inawezekana kabisa halmashauri nyingi zingeathirika sana kimapato na hata kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili wa jinsi anavyosimamia nchi yetu Mheshimiwa Rais, ni utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo inagusa huduma kwa wananchi. Miradi kwenye Sekta ya elimu, afya, maji, umeme na mawasiliano kwa uchache. Miradi kwa miaka hii mitano imevunja rekodi ya Kitaifa na hata Kimataifa, miradi ya umeme imevunja rekodi ya Kimataifa lakini miradi mingi katika sekta nyingi imevunja rekodi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kipindi hiki cha miaka mitano ndipo tumeshuhudia zimejengwa hospitali 70 katika wilaya. Tangu tupate uhuru kulikuwa na hospitali 77, mwaka huu 2019/2020 tunaoumalizia mwezi Juni tayari zimepangwa kujengwa hospitali 28 na fedha zimeshapelekwa. Sasa hii maana yake ni kwamba uongozi huu unajali wananchi. Vituo vya afya karibu 360 na sisi kule Sikunge tumepata Hospitali ya Wilaya, kituo cha afya cha Kitunda, Kipiri na Nyawa. Hizi ni kata ambazo ziko mbali na Sikunge zaidi ya kilometra 200 na watu tangu uhuru walikuwa hawapati hizo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tumshukuru na kumsifu Mheshimiwa Rais kwa maamuzi haya kwamba sisi Wabunge tumekuwa tukipeleka maombi, anayasikiliza haraka, anasikiliza wananchi na nawahudumia. Sisi tumepata shule mpya za kidato cha tano na sita mbili, hii ni

rekodi, Kamagi na Kiwele ni rekodi, na miradi mingine mingi sana Mwehe, hatuwezi kuacha kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kuishukuru Awamu ya Tano kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili linadhihirisha kwamba uoga wa sisi Wabunge tuliokuwa nao hapo awali kwamba halmashauri zetu zinanyang'anywa kodi na tozo mbalimbali zinakwenda Serikali Kuu kumbe Mheshimiwa Rais alikuwa na fikra zake katika kuboresha upelekaji wa fedha kwenye halmashauri zikiwa na maelekezo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi hii nadhani mwanzoni tulikuwa tunakosea sana na hatukuwa sahihi tulivyokuwa tunailaumu Serikali Kuu. Fedha nyingi zimepelekwa katika halmashauri na nyingi zimeleta matunda mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kwa sasa kama ambavyo tumesoma katika maoni mengi aliyotoa CAG ni kuboresha usimamizi wakati wa kujenga miradi, kuboresha ukaguzi wa kitaalam ili kuhakikisha kwamba thamani ya fedha iliyotumika inalingana na thamani ya mradi kuboresha ufuatilaji na tathmini wakati na baada ya utekelezaji na ili hayo yafanikiwe, maafisa masuuli wanatakiwa kuongeza umakini na nguvu kubwa katika kuzisimamia idara zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, idara ya kwanza ni ya ununuzi. Idara hii ya Ununuzi ni lazima izingatie mipango ya ununuzi katika kazi zake za kila siku, wazingatie mipango ya ununuzi ya mwaka na vile vile wazingatie kutunza nyaraka katika maeneo maalum ambayo ni *safe areas*. Kama hawana chumba maalum cha kutunza nyaaka, wawe na chumba maalum cha kutunza nyaraka ambazo zitahusika. Nyaraka zote za ununuzi zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi ziweze kupatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara nyingine ni Idara ya Ujenzi, Idara ya Ujenzi katika halmashauri ndiyo ambayo imepewa mamlaka na Sheria ya Ununuzi kwamba kama mradi unaweza ukasimama halmashauri basi mhandisi anatakiwa yeche asimamie viwango vya mradi. Kama

tukikuta mradi hauna viwango, yeye anatakiwa atoe majibu kwanini mradi hauna viwango. Yeye katika *force account* ndiyo *consultant*, mtaalam na mshauri wa mradi ule. *Contractor* watakuwa wamesaini nae mkataba kama ni *contractor* wa kijijini au wa kutoka wapi lakini mtaalam msimamizi au mtaalam mshauri ni mhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara nyingi za ujenzi hazina wahandisi wa kutosha. Wamebaki wachache baada ya wengi kuhamishiwa TARURA. Hili suala Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI anatakiwa alisimamie kuhakikisha kwamba Idara za Ujenzi katika halmashauri zinakuwa na utaalam wa kutosha ili wasimamie viwango vya mradi inayojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara nyingine ni Idara ya Uhasibu, Idara ya Uhasibu imehusika sana katika uzembe wa kupoteza nyaraka za mapato na matumizi na muda mwingi zimekuwa hazipatikani pale zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi. Sasa ninaomba sana Maafisa Masuuli, hususan Wakurugenzi wa Halmashauri, wasimamie vizuri hii Idara ya Uhasibu inayoongozwa na mweka Hazina wa halmashauri kuhakikisha kwamba nyaraka za mapato na matumizi yote makubwa na madogo zinatunzwa vizuri ili zinapohitajika kwenye kukaguliwa na CAG zipatikane kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya mwisho ni Idara ya Mipango na Uratibu. Idara hii inatakiwa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi. Sasa kama idara yenye, maafisa wenye, wawili, mchumi, afisa mipango wawili itafanya kazi zake vizuri katika halmashauri kubwa kama Halmashauri ya Sikunge. Kwa hiyo, huwezi kuimarisha utekelezaji mzuri katika halmashauri kama Idara hizi nilizozitaja hazina *staff* wa kutosha. Nilikuwa nafikiri kama ambavyo wanaajiriwa walimu, walimu 16,000 wataajiriwa hivi karibuni, na hizi idara nazo zinatakiwa zipewe kasma ya watumishi ili waweze kupatikana watumishi wengi zaidi ambaeo wataboresha utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana Wizara yetu ya TAMISEMI isimamie uboreshaji kwenye maeneo hayo ili kupunguza baadhi ya hoja. Hoja nyingi zinahusu idara hizo nne na kama Idara hizo nne zitaboresha utendaji wake, ninaamini kabisa kwamba hoja nyingi ambazo CAG amekuwa akizikuta kwenye miradi zitakuwa zimepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nirejee kuwashukuru tena wananchi wangu kwasababu hata juzi nilivyokuwa kwenye *Eid*wamenipokea vizuri, tumezungumza vizuri na wameonesha dalili za kutabasamu kwamba huenda pengine nikarudi tena hapa mwezi Novemba. Naipongeza Kamati kwa kufanya kazi yake vizuri kujadili Ripoti ya CAG, kufuatilia na kutoa mapendekezo mazuri ambayo mimi nayaunga mkono karibu yote yaweze kupitishwa na Bunge kama Maazimio. Ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ambayo imeniwezesha kusimama hapa na kutoa mchango wangu kwneye Taarifa hii ya Kamati ya LAAC ambayo mimi pia ni mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe lakini na Ofisi ya Bunge kwa maana ya Katibu wa Bunge na Sekretarieti ya Kamati kwa namna ambavyo wamekuwa wakiisaidia Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo kati ya malengo makuu ya uanzishwaji wa halmashauri za wilaya ni kutoa huduma kwa wananchi hasa huduma za kijamii kama vile huduma za kielimu, huduma za afya, maji, miundombinu n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hiki cha miaka mitano, nimeshuhudia nikiwa Mjumbe wa *LAAC* kwamba lengo hili la kutoa huduma limetimizwa kwa kiwango kikubwa sana. Katika kipindi cha miaka hii mitano, ndicho kipindi ambacho tumeshuhudia maeneo yote ya huduma za kijamii kwa mfano elimu katika kipindi hiki ndicho kipindi ambacho madarasa mengi yamejengwa kwa ubora mkubwa wa hali ya juu na kipindi ambacho huduma ya elimu imeimarishwa ukilinganisha na wakati mwagine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote sisi ni mashahidi, wote tuna majimbo, kata, tuna maeneo mbalimbali. Mimi kule kwangu kwa mara ya kwanza nimeshuhudia madarasa ya kiwango cha juu sana hata katika shule ambazo ziko maeneo ya vijiji kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina shule ambazo ziko katika kijiji cha Gengetisa, Mbooga Semembela, Lugululwanzungu kule Mbutu, madarasa yaliyojengwa kwa mpango wa *P4R* ukifika huwezi kuamini ubora wa madarasa yale kama yangeweza kujengwa kwenye maeneo ya vijiji namna ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ishara na uthibitisho dhahiri kwamba huduma hii ya jamii ya elimu katika kipindi hiki imetolewa kwa kiwango kikubwa sana lakini kama wachangiaji wengine walivyosema katika kipindi hiki ndicho kipindi ambacho zahanati nyingi zimejengwa, vituo vyta afya vingi vimejengwa, hospitali nyingi zimeboreshwa, kwa hiyo, kwangu kule sasa hivi *operation* za kawaida wananchi wa jimbo langu hawnaa haja ya kusafiri mpaka Nzega Mjini, vituo vyta afya vimewezeshwa, sasa vina vifaa na vinafanya shughuli za operesheni jambo ambalo hapo nyuma halikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo la kuundwa kwa halmashauri la kutoa huduma hizi za kijamii limetimizwa kwa kiwango kikubwa sana katika maeneo karibu yote katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ambalo ningependa nichangie ni kwamba kwenye eneo la makusanyo ya mapato na matumizi ya mapato tumekuwa tukitumia mifumo ya kiteknolojia/kielektroniki tofati na hapo zamani ambako tulikuwa tunatumia *manual receipts*. Matumizi ya mifumo hii ya kielektroniki kwa kiwango kikubwa sana yameboresha na yameondoa matatizo yaliyokuwepo hapo siku za nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba matatizo hayajaisha lakini kwa kiwango kikubwa sana matatizo yaliyokuwepo ya ubadhilifu, ujanja ujanja na wizi katika mifumo yameondoka kwa kiwango kikubwa. Ushauri wangu katika eneo hili ni kwamba wataalam wa hii mifumo waendelee kufanya ubunifu ambao utasaidia baadhi ya mambo ambayo tunayataka yaweze kufanyika kwa kutumia mifumo na yale mambo ambayo hatuyahitaji yaweze kuzuiliwa na mifumo yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwasababu kuna baadhi ya mambo kama yasipozuiliwa kwa mifumo inakuwa ni ngumu mno kuyazuia kwa mfano, sualala vipaumbele katika matumizi ya fedha zinazokusanywa kwenye mapato ya ndani, *priority* za matumizi pamoja na kwamba halmashauri zina changamoto katika ukusanyaji wa mapato ya ndani lakini pia hata hizo fedha ndogo zinazokusanywa maeneo mengine kumekuwa na changamoto ya vipaumbele kwamba fedha hizo jambo gani kwanza fedha zitumike, lingine lisubiri au lingine lianze lingine lifuate baadae. *Priority*, vipaumbele!

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba katika ule mwongozo wa fedha wa halmashauri za mitaa, ile *financial memorandum* kuwepo na kipengele ambacho kitaje kabisa vipaumbele ambavyo halmashauri inapaswa iviweke pale ambapo inafanya matumizi ya fedha zake za ndani. Kwa mfano, tumeamua kwamba suala la asilimia 10 za akinamama, vijana na walemavu liwe ni jambo ambalo la kipaumbele kikubwa cha kwanza. Lakini tumeamua kwamba asilimia 40 inayokwenda kwenye miradi ya

maendeleo kwa Halmashauri ambazo mapato yake ni chini ya bilioni 5 na asilimai 60 kwa halmashauri ambazo mapato yake ni zaidi ya bilioni 5 tumeamua kwamba hizi pia ziwe kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala pia la stahiki za madiwani. Kwa hiyo mambo kama haya asilimia 10 ya akina mama, vijana na walemavu, asilimia 40 ya kwenda kwenye maendeleo, stahiki za madiwan ziwe ni *first charge*, ni vipaumbele na vitajwe kabisa kwenye *financial memorandum* ili afisa masuuli yeyote anapokusanya fedha za ndani kabla ya kutumia maeneo mengine ahakikishe kwanza awe na *checklist* ahakikishe kwamba...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka ukumbi wa Msekwa, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani zedi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Zedi kwamba akumbuke mwaka jana tulitunga sheria na Bunge tukaipitisha kutoa asilimia 10 kwa Maafisa Masuuli wote nchi nzima ni sheria na sio ombi. Kwa hiyo, sasa anapoendelea kuchangia atambue hilo na kwamba sheria hiii imeshaanza kufanya kazi na inafanya vizuri sana na kila halmashauri wameweza kutekeleza kwa asilimia 100. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, unaipokea Taarifa?

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa lakini nilichokuwa nasema, ni Mjumbe wa LAAC na tumezagua. Bado kuna baadhi ya Halmashauri zinasuasua katika kupeleka asilimia 10 pamoja na kwamba ni sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nasema ni kwamba mifumo itusaidie, ule mfumo wa kielektroniki

ukisetiwa *in such a way* kamba afisa masuuli akishakusanay mapato ya ndani ahakikishe kwamba mfumo umkatalie, yaani *first charge* iwe ni asilimia 10, kinachofuatia iwe ni asilimia 40 kwenye maendeleo. Kinachofuatia ni stahiki za madiwani halafu matumizi mengine yafuate.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akitaka kuanza matumizi mengine mfumo ugome, yaani mfumo wenyewe wa kielektroniki usiweze ku-*transact* mpaka pale ambapo amepeleka kwanza hii asilimia 10, amepeleka kwanza ile asilimia 40 kwenye miradi ya maendeleo na pia amepeleka fedha katika mambo ambayo yametajwa kwamba yamo kwenye *first charge* ndiyo matumizi mengine yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu bila kusaidiwa na mfumo kuna maeneo mengine hata kama ukiweka sheria bado Maafisa Masuuli wengine wanaweza wasitekeleze kwa mfano hili la asilimia 10 juzi tulikuwa na ukaguzi wa halmashauri na tumbaini baadhi ya halmashauri chache pamoja na kwamba ni sheria lakini bado maafisa masuuli unakuta hawapeleki zote. Bado wanapeleka sehemu tu na wana madeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kwamba tumbaini bila kificho chochote kwamba mfumo wa kutumia *force account* una faida ya kwamba unapunguza matumizi ya miradi ukilinganisha na mfumo wa nyuma wa kutumia wakandarasi kwenye miradi mingi. Lakini changamoto kama ambavyo imekuwa ikisemwa na Waheshimiwa wengine ni uhaba au upungufu wa wahandisi kwasababu unapotumia *force account*, hutumii tena mkandarasi inabidi wahandisi wako wa halmashauri wasimamie miradi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali inapeleka miradi mingi kwenye shule, afya na maeneo mengine. Sasa unakuta Halmashauri ina mhandisi mmoja au wawili wanashindwa kuisimamia lakini hii ni changamoto ambayo inatokana na kwamba Serikali inapeleka miradi mingi halafu

wahandisi wa kusimamia kwa sababu ni wachache na tumeamua kwenda mfumo wa *force account* inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, mimi ni Mjumbe wa Kamati, maeneo mengi yameguswa au yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengine nisingependa niyarudie, lakini nakubaliana kwa asilimia 100 ya taarifa ya Kamati yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tu niseme kiujuumla ni kwamba maeneo mengi yaliyokuwa sugu; maeneo ya malipo bila nyaraka kamilifu, ukiukwaji wa taratibu za manunuzi; maeneo mengi kumekuwa na *improvement* kubwa sana ukilinganisha na hali ilivyokuwa hapo nyuma. Kwa hiyo, hii ni dhahiri kwamba Kamati imefanya kazi kubwa sana, Bunge pia limesaidia sana Kamati na Halmashauri pia zimeitikia na kuweza kubadilika. Kwa hiyo, mwelekeo ni mzuri. Mwelekeo ni *very positive*, na ni matumaini yangu kwamba huko tunapokwenda miaka michache baadhi ya maeneo haya matatizo yake sugu yatakuwa yametatuliwa na itabaki kuwa historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii na ninaunga mkono taarifa hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rhoda Kunchela atachangia dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami pia naipongeza Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo imeifanya na imeweza kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipiga kelele sana kuhusiana na suala la hii mifumo ya fedha ya ukusanyaji wa kodi mbalimbali katika Halmashauri zetu kwa maana ya matumizi ya hizi *EFD machine* na mfumo wa *POS* kuelekea huko kwenye TAMISEMI. Niseme tu bado kuna changamoto

kubwa. Tumekuwa tukipiga kelele sana hapa kwamba Halmashauri nyingine ambazo zipo vijijini nyingi hazina hii mifumo ya ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni rai yangu kwamba Serikali ihakikishe kwamba kwenye maeneo ambayo hizi *electronic machine* hazijapelekwa zipelekwe kwa suala zima la kuhakikisha kwamba tunapata pesa na makusanyo ya kodi na pia kuzuia wizi wa kodi za wananchi. Tumeona kabisa kupitia hii ripoti ya *LAAC* wameonesha baadhi ya Halmashauri ambazo zinatumia stakabadhi za mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaelewa kwamba wanakusanya kwa kutumia hizi risiti za mikono na ukizingatia kwenye Halmashauri zetu pesa nyingi ambazo zinakusanywa ni ushuru na kodi mbalimbali na nyingi ni za wakulima na akina mama wajasiriamali ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kwa wakulima, mtu ambaye anasafirisha chini ya tani moja, gunia tano, kumi, gunia mbili, debe tatu wanatozwa ushuru na kodi mbalimbali kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni rai yangu Wizara ya Fedha na TAMISEMI kuhakikisha kwamba wanashughulikia tatizo hili ili hao watumishi wanaohusika na kutumia hizi risiti za mikono waweze kudhibitiwa na Serikali ya chama chako iweze kuwajibisha kwa wizi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingine Kamati imesema zaidi ya shilingi bilioni 258 zilipelekwa mwishoni kwenye hizi Halmashauri. Kwa hiyo, naomba, kuna Halmashauri ambazo hazikupata pesa kabisa. Kuna Halmashauri ambazo zilipelekewa pesa pungufu ikiwemo Halmashauri yangu ya Mpimbwe katika Mkoa wa Katavi, waliomba shilingi milioni 172.9 na wakapewa shilingi milioni 141. Ni pungufu ya zaidi ya shilingi milioni 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, hii Halmashauri iko pembezoni, Shule za Msingi zina hali mbaya. Wananchi,

watoto wadogo wanatembea zaidi ya kilometra 10 au 15 kufuata Shule za Msingi. Miradi mingi katika Halmashauri hii imesimama kutokana na kwamba Serikali yako imeshindwa kupeleka pesa na kukamilisha miradi. Kwa hiyo, naomba kwa sababu Halmashauri hii naifahamu vizuri, mazingira ya barabara, shule, miradi ya maji, Hospitali na Kata mbalimbali katika Jimbo hili, miradi mingi imesimama. Naomba kabisa hebu mwangalie Halmashauri hii ya Mpimbwe. Tumeona Halmashauri nyingine zimepelekewa pesa mpaka ya ziada; mtu anaomba shilingi bilioni moja, anapelekewa shilingi bilioni tatu, ziada ya bilioni mbili. Kwa hiyo, naomba liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo hata Wajumbe wengine wamesema, naomba Madiwani wetu katika Halmashauri zetu wapelekewe fedha, walipwe posho zao. Tunakwenda kuhitimisha Baraza la Madiwani mwezi ujao wa Sita tarehe 10. Pesa zipelekwe, Madiwani wanaishi katika hali mbaya sana na Waheshimiwa Wabunge wamesema watu wana madeni, wana mikopo. Mwalipe pesa zao kwa sababu mnawasabishia hawa Madiwani kupata msongo wa mawazo na hii inaonesha kabisa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmeshindwa hata kutetea llani yetu na kuitekeleza kwa mwaka huu 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru, nikutakie majukumu mema. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kweli nimeamini hili ni Bunge la mwisho maana mpaka Mheshimiwa Rhoda anakubali kwamba hii ni Serikali ya CCM, ni jambo jema. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atakuwa mchangiaji wa mwisho. Huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na

Wajumbe wenzangu ambao wamekushukuru wewe na Mheshimiwa Spika kwa jinsi ulivyotupa miongozo na usaidizi katika kutekeleza majukumu yetu. Pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa sababu kwa kipindi hiki cha miaka mitano waliniamini kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na ninawashukuru kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kipekee nampongeza Ndugu Charles Kichere (*CAG*) kwa kazi nzuri anayoifanya. Ametoa taarifa nzuri ambayo imekuwa ni nyaraka muhimu katika utendaji kazi wa Kamati yetu. Hii taarifa ambayo tumeiwasilisha leo, sehemu kubwa ni mapendekezo au maoni ambayo ameyatoa kwenye taarifa yake, lakini siyo taarifa yake tu na utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema Wabunge wengi ni kwamba baada ya kuingia ameleta mabadiliko katika ofisi yake na ametoa ushirikiano mkubwa sana kwa Kamati yetu. Kwa hiyo, tunampongeza sana Ndugu Charles Kichere kwa kazi nzuri na tunaomba ushirikiano huo uendelee na Kamati yetu ya *LAAC* na Kamati nyingine ya *PAC*. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu hoja hii ambayo tunajadili leo inaihusu Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kwa muundo wa Serikali hii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ipo chini ya mamlaka yake. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo ambayo imewezesha kujengeka kwa nidhamu ya fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Jafo na timu yake pale TAMISEMI kwa jinsi wanavyosimamia mabadiliko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hatimaye tumepata taarifa ambayo haina makandokando mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, nilitaka nitoe maelezo machache kuhusu hoja ya

Mbunge mmoja ambaye alisimama hapa na kusema kwamba kuna upondaji wa *Local Government Reform* unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Bahati mbaya Mheshimiwa Mch. Msigwa hayupo, ningependa tu kumwambia hebu akae vizuri aisome *Local Government Reform Policy Paperya* mwaka 1998, aone ilikuwa na malengo na maudhui gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya *document ile ya Local Govermnet Reform* ni kuhakikisha kwamba huduma stahiki zinapatikana kwa wananchi na kwa wakati muafaka. Sasa hiki kinachofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ni utekelezaji wa *reform*. Tunapoanzisha miradi ya kimkakati katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, sasa hivi kama Jiji la Dodoma kuna Mradi wa Soko na Stendi mpya ya kisasa ambayo wataingiza shilingi bilioni 16 kwa mwezi. Hayo ni maboresho makubwa na hiyo italiwezesha Jiji la Dodoma kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga Vituo vya Afya zaidi ya 355. Hayo ni maboresho makubwa. Kuna madarasa na nyumba za walimu tumejenga nyingi, hayo ni maboresho makubwa na tunatoa huduma kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mch. Msigwa akasome vizuri *ile policy paper* ambayo inaelezea vizuri madhumuni ya *Local Goverement Reform Policy* ambayo ilikuwa inaelezea kinagaubaga kwamba maudhui ni nini na lengo kubwa ilikuwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile amesema kwamba kuna mwingilio mkubwa wa Wakuu wa Mikoa na ma-DC kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ukitu *Regional Administration Act* ya mwaka 1997 unapata kabisa majukumu ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa mamlaka za Serikali za Mitaa. Kazi yao ni kutengeneza mazingira wezeshi ili Mamlaka ya Serikali za Mitaa ziweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo maboresho ambayo leo Mbunge alikuwa anajisifia kwamba Iringa Manispaa

wameyapata, hawesi kuacha shughuli ya *RC* na *DC* wa eneo lile kwamba wana mchango katika maboresho hayo. Kwa hiyo, lazima tusibeze kazi iliyopo ya ma-*DC* na *RC* na wanakwenda pale kisheria na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye mchango wangu kwenye hii taarifa yetu ambayo tumewasilisha, nami nitachangia machache kwa sababu sehemu kubwa kama nilivyo sema, mimi ni Mjumbe wa Kamati, mengi tumeyachangia katika *level* ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema nidhamu ya fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa yameboreka sana. Hata ukiangalia taarifa ya *CAG* inasema kwamba kwenye Halmashauri 185, Halmashauri 176 zimepata hati inayoridhisha, sawa na asilimia 95. Hii utaona ni maboresho makubwa na ni tofauti na huko nyuma tulipotoka ambako kulikuwa na Halmashauri nyingi ambazo zilikuwa zinapata hati zenyе shaka, lakini mwaka huu hati zenyе shaka ni Halmashauri tisa tu, sawa na asilimia tano. Kwa hiyo, kuna nidhamu ya fedha ambayo imejengeka katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maboresho hayo ambayo yamefanyika, kuna changamoto ambazo zipo na tumezitaja kwenye taarifa yetu. Nirudie kama walivyosema baadhi ya Wabunge kuhusu hili suala la *NHIF* kutorejesha fedha shilingi bilioni mbili kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hapa kuna tafsiri mbili; kwanza, kuna uzembe wa Watumishi wa Afya kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutojaza ipasavyo zile fomu na pili, *NHIF* (Bima ya Afya) wajiangalie upya kwamba kwa nini kuna changamoto kama hii katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha ni nyingi na bahati mbaya tulipokuwa tunawahoji Maafisa Masuuli wanasema hata zile fomu ambazo zina makosa madogo ambayo yanaweza yakarekebishwa Bima ya Afya wanasema ukishaleta fomu kwetu, haturejeshi tena kwa ajili ya marekebisho. Kwa hiyo, utakuta Mamlaka ya Serikali za Mitaa

zimekosa fedha hizi shilingi bilioni mbili kwa makosa mengine madogo ambayo yangeweza kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa tunaiomba TAMISEMI ifuatilie suala hili hasa kwa Watendaji wa Afya. Haji akilini kwa Watumishi wa Afya wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa washindwe kujaza fomu hii ipasavyo wakati wa hospitali nyingi za binafsi wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ambao umejionesha kwenye taarifa hii ya CAG. Kwenye Vitengo vya Manunuzi katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kumeimarika kwa kiasi kikubwa lakini bado kuna dosari kama alivyoonesha CAG kwamba amefanya ukaguzi wa kina katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 74, akakuta kuna manunuzi yalifanyika ya shilingi bilioni 32.4 bila kushindanisha katika ufanyaji wa manunuzi hayo; yaani ni manunuzi ambayo yamefanyika tu, Afisa Masuuli ameenda kwa Mzabuni akasema tufanye kazi fulani, bila kuwa na ushindani kama inavyosema Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya CAG kwamba kosa hili lingeweza kurekebishwa endapo Kitengo cha Manunuzi wangeshindanisha manunuzi haya na hivyo hoja kama hizi zisingeweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, akafanya ufuatiliaji wa kina kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 47 akakuta kwamba kuna manunuzi ambayo yalifanywa bila kutumia *Tender Board*. Afisa Manunuzi amenunua moja kwa moja bila kuitumia *Tender Board* ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hii imechukua fedha kama shilingi bilioni 9.2. Hapa Afisa Masuuli angeweza kuzuia hoja hizi kwa kutumia *Tender Board* ambayo ipo kisheria katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Rais TAMISEMI kufuatilia udhaifu kama huu kwa Halmashauri husika na bahati njema taarifa ya CAG ipo wazi kabisa, imezitaja hizo Halmashauri. Kwa nini Maafisa Masuuli hawa waliamua kufanya hivi? Kwa sababu wanaturudisha nyuma.

Hoja kama hizi hazikuwa na sababu ya kuwepo kwenye Taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwenye mikataba. Bado kuna Halmashauri chache zinaonesha dosari katika usimamizi wa mikataba. Kwa mfano, kuna mikataba ya shilingi bilioni 9.5 wamepewa wakandarasi ambao hawastahili na ni kosa ambalo lingeweza kuzuiliwa na Maafisa Masuuli kama wangekuwa makini wakati wa kutoa mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo kuna changamoto katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Kamati za Ukaguzi za Halmashauri. Kuna nyaraka mbili muhimu sana kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa; kuna *Local Authority Financial Memorandum* na *Local Authority Accounting Manual*, zote zinasisitiza umuhimu wa Afisa Masuuli kuandaa *Internal Control System*. Wakurugenzi wa Halmashauri hizi wangekuwa wanaandaa utaratibu wa kuweka *Internal Control* na kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani, hoja nyingine zingeweza kumalizwa kabla CAG hajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI iboreshe Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani, itoe vitendea kazi, iongeze idadi ya watumishi, kwa sababu inatakiwa kwa ikama ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa wawe wakaguzi wasiopungua wanne au watano, basi kuwe na ajira ya makusudio ili kuhakikisha kwamba kitengo hiki kinakuwa na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona hoja nyingine kwamba zile za kiuhandisi ni kwa sababu ya uhaba wa Wahandisi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kuwe na ajira ya makusudi kwa wahandisi wa ujenzi ili kuziba mapengo ya wale Wahandisi ambao wamehamishwa kwenda TARURA baada ya kuanzisha chombo chetu cha TARURA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru vilevile Wakuu wa Mikoa jinsi wanavyosaidia katika kuboresha

utendaji wa hizi Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu wanasisimamia kila inapowasilishwa Taarifa ya CAG katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa wao wana-chair vile vikao na katika kusisimamia vile vikao wanahakikisha kabisa ma-RAS na Wakurugenzi wanakuwa na *timeframe* ya kuhakikisha kwamba hoja za ukaguzi wanazijibu kwa uhakika. Kwa hiyo, nawapongeza Wakuu wa Mikoa kwa jinsi wanavyohakikisha kwamba hoja za ukaguzi zinapungua katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru wananchi wa Nanyamba kwa jinsi walivyonipa ushirikiano na hata sasa hivi ushirikiano ni mkubwa kwa sababu watu wanaozungukazunguka ni wachache, ni kama hawapo vile. Kwa hiyo, hii ni ishara tosha kwamba wana matumaini na mimi, nami nina afya na nguvu tele na nipo imara kuwawakilisha tena kuanzia Novemba mwaka 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa wachangiaji wetu. Orodha niliyokuwa nimeletewa wote wameshachangia. Kwa namna ya kipekee nianze kwa kutambua Waheshimiwa Mawaziri wawili ambao leo wamependeza sana humu ndani; Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, hongereni sana kwa kupendeza. Naona mambo mazuri kabisa haya. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimezungumza mwanzo kwamba tupo na CAG humu ndani ambaye anatusaidia kufanya kazi ya kuangalia kile ambacho kimetengwa na Bunge na kuidhinishwa kwa ajili ya Serikali kikutumia, lakini pia namna kinavyotumika kule. Kwa hiyo, yupo hapa ndani na wasaidizi wake, tutambue tena uwepo wake, tunamshukuru kwa kazi nzuri, nadhani naye

anashuhudia Waheshimiwa Wabunge namna ambavyo wanaonesha amefanya kazi nzuri. Ni jambo jema. (*Makofi*)

Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja wakati akichangia alikuwa amezungumza kuhusu mafunzo kwa Wabunge, pengine akasema tunaweza kufikiri kufanya hayo mafunzo baadaye ili Wabunge wawe wanajua nini cha kuchangia wakati gani kwenye Taarifa za Kamati, lakini pia wakati wa bajeti. Nimtoe tu wasiwasi, mafunzo huwa yapo lakini hutegemea Mbunge kama anataka kujifunza au hapana, kwa sababu hata Bunge hili tulianza kwa mafunzo mwanzoni kabisa.

Pia sababu ya kuangalia Wabunge tupo wengi na wakati mwagine Mbunge anaweza kuwa hajapata fursa ya kuzungumzia jambo ambalo anaona ye ye lazima aseme ili kujihakikishia Novemba yake humu ndani. Kwa hiyo, hapa mbele tukimwacha azungumze haimaanishi hatujaona ametoka nje, lakini tunamwacha azungumze pengine anataka wananchi wake wamsikie. Kwa ujumla wake, Wabunge mmefanya kazi nzuri ya kuchangia kwenye hoja hii ambayo tutaendelea nayo kesho.

Jambo lingine liliojitokeza ni kuhusu madeni ya Waheshimiwa Madiwani. Yupo hapa Mheshimiwa Jafo na Waziri wa Fedha, mengine watayatolea maelezo, lakini nadhani pia kuna mambo tunachanganya kidogo, deni alilolikopa ye ye ambalo halina uhusiano na yale ambayo Serikali pengine inadaiwa kwake, kwa maana ya zile fedha ambazo alitakiwa kulipwa, anaidai Serikali, hilo ni jambo moja, lakini la ye ye kudaiwa na benki kama anadaiwa na benki atadaiwa na benki na benki itauza tu hiyo nyumba. Siyo kwa sababu nyingine, ni kwa sababu anadaiwa. Ni sawa na sisi Wabunge ambavyo tunadaiwa na wengine wamekopa hela nyingi zaidi kuliko Bunge linavyoisha mwezi wa Sita.

Nadhani Mheshimiwa Spika alishatoa maelekezo, kila mtu alipewa barua yake ili ajue anadaiwa kiasi gani. Kwa hiyo, muktadha ni huo huo hata kwa Waheshimiwa

Madiwani. Hakuna namna Baraza la Madiwani litalipia mtu fedha zile ambazo alikopa yeche na ametumia kwa kitu chake ambazo yeche haidai Serikali.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, haya lazima hata sisi tunapozungumza na wenzetu ambao ni Madiwani, nasi ni Madiwani, lazima tuyaweke haya mambo vizuri yasije yakasababisha kwamba anayedaiwa ni Baraza la Madiwani au kama sisi Wabunge hapa tukasema anayedaiwa ni Bunge, hapana. Fedha zilikopwa na yule aliyetia saini huko benki alipoenda kukopa, kwa hiyo, taasisi hakuna namna itaingia hapo.

Hata kama unasema dhamana ilikuwa, hakuna dhamana inayowekwa kwa Taasisi kama Bunge au Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, kama benki ilitoa bila kujua dhamana itakuwa ni kipi, taasisi hizi hazijatoa dhamana popote, kinachotolewa ni utambuzi wa huyu mtu kwamba huyu ni Diwani na huyu ni Mbunge. Kwa hiyo, kila mtu analazimika kulipa madeni ambayo alikopa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 11.25 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 28 Mei, 2020 Saa 8.00 Mchana)*